ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
30. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele

32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tisa – Tarehe 01 Juni, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *(PAC*), kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka 2016/2017

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 44

Kutoweka Huduma ya Ununuzi wa Umeme kwa Simu

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Shihata) (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) lilizindua huduma ya kununua umeme kwa kutumia simu za mkononi kupitia Kampuni ya *Zantel* ambazo zimeyeyuka kama barafu katika jua na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

a) Utaratibu wa watu kununua umeme kwa kupanga foleni katika vituo Shirika kupiga hatua mbele ya Maendeleo au kurudi nyuma.
b) Kwa kuwa wananchi wanaendelea kuteseka kwa muda mrefu kwa kutoweka huduma hiyo, kwa nini Shirika limekaa kimya kueleza wananchi sababu za kutoweka kwa huduma hiyo wakati wananchi hufaidika na huduma hiyo.
c) Kwa kuwa wananchi wamekuwa wakikaa muda mrefu kwenye vituo wakati muda huo ni wa harakati za kiuchumi, kwa nini Shirika la Umeme hawatafuti Kampuni nyengine za simu na kuingia Mkataba wa kuuza umeme zaidi ya Kampuni moja kama ilivyo kwa Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*).

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye vipengele (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, kwanza kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo machache kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Shirika la Umeme liliingia mkataba na Kampuni ya simu ya *Zantel* mnamo mwaka 2014, kwa ajili ya kununua umeme wa TUKUZA kwa njia ya simu. Lengo la hatua hiyo lilikuwa ni kuwarahisishia wananchi kupata huduma ya kununua umeme bila ya usumbufu kwa wakati wote. Huduma hii ilisita ghafla kuanzia tarehe 20 Februari, 2016 kutokana na hitilafu za kiufundi za mawasiliano baina ya mtandao wa *Zantel* na mfumo wa TUKUZA na *ZECO*.

Baada ya kujitokeza hitilafu hizo wataalamu wa pande zote mbili wamekuwa wakishirikiana kwa pamoja kwa ajili ya kutatua tatizo hilo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, baada ya kutokea kwa tatizo hilo, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme lilianza kwa kuwaita waandishi wa habari yaani *Press Conference* na kuelezea chimbuko la tatizo na hatua zinazochukuliwa. Pia taarifa imekuwa ikitolewa katika vyombo mbali mbali vya habari. Aidha, baada ya kumalizika mkataba na Kampuni ya *Zantel* unaoishia mwezi wa Agosti, 2016, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme litakaribisha Makampuni tofauti yatakayokuwa tayari katika utoaji wa huduma hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama tungekuwa tuko darasani, basi Mhe. Jaku Hashim Ayoub ningesema kanikopia katika swali nililopeleka ambalo halijajibiwa kama hili. Lakini kwa kuwa nimebahatika kuuliza swali zuri na swali hili linataka majibu mazuri kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, na kwa kuzingatia kwamba wananchi wetu wengi wa vijijini, hushindwa kusafiri kutoka vijijini kuja kununua umeme mjini, na kwa kuwa Kampuni hii ilionesha mwelekeo mzuri na katika mwelekeo huo wa kuwanusuru wananchi wetu kununua umeme hata saa 6:00 za usiku kwa wanaojua.

Je, wizara ina mpango gani ukiacha huo mwezi wa Agosti wa kuharakisha suala hili ili wananchi waondokane na shida kila siku?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Ahsante Mhe. Spika. Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme tayari imefanya harakati za kuhakikisha kwamba hii huduma inarejea na hatua zilizofikiwa sasa ni kwamba tunasubiri kifaa kutoka Afrika ya Kusini wakati wowote kikifika itakuwa huduma hii imerudia kama kawaida. *(Makofi)*

Nam. 59

Ukosefu wa Matuta Barabara ya Mazizini Mzunguko Fumba

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la matumizi mabaya ya barabara ya kuanzia mzunguko wa Mazizini mpaka Fumba ambapo waendesha vyombo vya usafiri vya moto kama gari, vespa na pikipiki huendesha kwa mwendo wa kasi kupita kiasi na kusababisha ajali na upotevu wa maisha na ulemavu hasa maeneo ya skuli.

a) Je, lini barabara ile itawekwa matuta ili kudhibiti madereva hasa vijana wanaokimbizana na vespa *(t-one*).

b) Kutowekwa matuta barabarani hamuoni kwamba inazidisha ongezeko la ajali za kizembe ambazo waathirika wakubwa ni wanafunzi wa skuli ilimopita barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa wako baadhi ya vijana ambao wanatumia vibaya matumizi ya barabara hususan kuanzia mzunguko wa Mazizini mpaka Fumba kwa kuendesha vyombo vya moto kwa mwendo wa kasi unaoweza kusababisha ajali.

(a) Mhe. Spika, kwa sasa serikali haina mpango wa kuweka matuta katika maeneo hayo, lakini itarejesha alama za barabarani zilizoibiwa na kurejesha michoro ya barabarani ambayo imeanza kufutika, ambayo kwa kiasi kikubwa inawaongoza waendeshaji wa vyombo vya moto.

Aidha, kwa madereva ambao hawafuati Sheria za barabarani, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi la Usalama Barabarani litaongeza usimamizi ili kuwachukulia hatua wote wanaoendesha vyombo vya moto kwa mwendo kasi. Aidha, naomba kutumia fursa hii kuwaomba wananchi wazilinde alama za barabarani ambazo zimekuwa zikiibiwa mara kwa mara.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu la (a) ni kwamba hatutoweka matuta, lakini serikali itaweka vivuko vya watembea kwa miguu yaani *Zebra Cross* katika maeneo yote ya skuli zilizopita barabara, na ninaendelea kuwaomba madereva tena sana na ninawanasihi, wafuate Sheria za barabarani ili kuepukana na ajali za kizembe.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali langu la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa serikali haina mpango wa kuweka matuta katika barabara hizo. Je, ni sheria zipi zinazoruhusu kuwekwa matuta katika skuli ya Bububu na Mwera na ni sheria gani inayokataza kuwekwa matuta kujengwa matuta katika skuli za Kisauni, Mitondooni na Kiembesamaki.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, ni kweli kwamba tatizo la ajali linatukera sana sisi hasa katika wizara yetu. Ndio maana utaona katika mpango wetu ni kuhakikisha kwamba ajali hizi zinapungua kila wakati inavyowezekana.

Mhe. Spika, kuhusu kuweka matuta katika sehemu nyengne, hii inatokana na baada ya kutokea ajali nyingi sana katika barabara hizo, kwa hivyo watu wale wakaja kutuomba na sisi baada ya kufikiria sana tukaona wanahitaji kuwekewa matuta. Lakini sio lengo letu kwa barabara kama hizi nzuri kila siku kuziwekea matuta, kwani inasababisha sana kupunguza mwendo. Mimi nawasihi tena madereza. Juzi niliwapongeza madereva wa Mkoa wa Kusini Pemba na Kaskazini Pemba, kwa sababu ajali kule ziko kidogo, licha ya kwamba barabara zao hazina matuta. Mimi nawaomba sana madereva wa huku Unguja na wao wajitahidi kuhakikisha kwamba hawaendi mwendo wa kasi na wanafuata sheria za barabarani.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa kuwa kuna baadhi ya skuli zimewekewa matuta kwenye njia tunazopita, na kuna baadhi ya skuli kama anavyoeleza Mhe. Mwakilishi wa Chukwani hapa, kwamba barabara nyengine hazijawekwa matuta.

Je, ni lini wizara hii imekaa na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha Polisi wanakuwepo wakati muda wote, kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni wanapotoka wanafunzi kwa Zanzibar nzima.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, sisi katika wizara yetu idara inayohusika na leseni na usafirishaji wa bodi yao, katika hii bodi pia vipo vyombo vya usalama barabarani ambapo Mkuu wa

Traffic pia ni mjumbe wa bodi hiyo. Kwa hivyo, wakati wowote wanakutana na kuangalia utaratibu wa kuhakikisha kwamba ajali zinapungua sana nchini kwetu. Kama ulivyosema bado Jeshi la Polisi lina Askari kidogo, kwa hivyo itakuwa tabu kwao kuweka kila sehemu Askari wa kuweza kuwaongoza watoto wanapotoka skuli. Lakini wanafanyakazi hiyo pale nafasi inaporuhusu.

Mhe. Spika, mimi naendelea kutoa wito wangu kwa wananchi wote kwamba tuendelee kufuata sheria za usalama barabarani, na tutajadiliana zaidi katika mpango wetu mkakati ili kuhakikisha kwamba ajali hizi zinapungua. Vile vile natoa pongezi sana juzi Mhe.Waziri hapa alitetea sana kuhusu kuruhusiwa zile pesa bilioni 18 kwa ajili ya kuweka *CCTV*, yaani *camera* za kuangalia mambo yote yanayotokea katika barabara zetu, au kitengo kile kitatusaidia sana katika kudhibiti ajali na vile vile kuwadhibiti madereva wazembe.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri kuhusiana na suala la matuta. Ni kwamba kweli hizi rangi za zebra pamoja na alama zinapowekwa barabarani, huwa zinafutika kutokana na michanga au miti zinafichwa na huzioni.

Mhe. Spika, nilikuwa nina swali dogo kwa Mhe. Naibu Waziri. Nilikuwa nataka kujua tu ni kitu gani kitakachowafanya labda kwa upande wa wizara, kuweza kuwaza au kufikiria yaani mnahitaji idadi ya wananchi wangapi wafe, waumie, wazee, vijana, walemavu ili nyinyi kama serikali au wizara yako mtachukua mawazo angalau ya kuweka matuta maeneo kama Dunga Mitini, na maeneo yale ya katika swali la msingi alilouliza Mhe. Mwanaasha kwa upande wa Mazizini, ili kupunguza hizi ajali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, najua yeye inamuuma sana kuona kwamba ajali hizi zinatokea. Hata sisi kama wizara na serikali hatupendi kuona watu wetu wanakufa, ndio maana tunasema kwamba tunawasihi sana waendesha vyombo vyote vya moto barabarani kutii sheria, watii sheria bila ya kushurutishwa. Nilisema kabla kwamba huu mpango wa kufunga *CCTV camera* utasaidia sana kuhakikisha kwamba wale madereva wazembe hawatapata mpenyo wa kukimbia mikono ya sheria.

Kwa hivyo, mimi namwambia tena kwamba tutaangalia uwezekano, iwapo tutaona kwamba ajali nyingi zinatokea sehemu hizo, licha kwamba tutaweka *traffic* wa kuangalia kuwapitisha wale watoto, lakini vile vile tutahakikisha kwamba tunaweka matuta ili kuhakikisha kwamba hizi ajali zinapungua au zinatokomea kabisa.

Mhe. Spika, lakini kama nilivyosema awali kwamba bado mimi nawasihi sana madereva tuendelee kuangalia kwamba wao pia katika hizi ajali wanaathirika. Kama nilivyosema hapo kabla, Mkoa wa Mjini na Magharibi peke yake kulikuwa na ajali 450 katika ajali zote zilizotokea 619. Kwa hivyo, nawasihi sana madereva hasa wa mjini, nilisema mwanzo Kusini Pemba, Kaskazini Pemba ajali ni chache licha ya kwamba hakuna hizo *zebra crosses*, hakuna vile vile matuta. Nawasihi tena kwamba waepukane na uendeshaji wa uzembe ili kuwaokoa wananchi wetu na vilema vya maisha, ajali na vifo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 81

Kuimarishwa kwa Michezo Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Mchezo wa Mpira wa Miguu (*Football*) ni miongoni mwa mchezo mkubwa unaopendwa na watu wengi hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Hali hii imechangiwa na jamii yenyewe kuweka nguvu kubwa katika kuukuza, kuushabikia na kuutangaza mchezo huu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha michezo mengine kama vile kuvuta kamba, kufukuza kuku, karata, bao nk.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mchezo wa mpira wa miguu (*Football*) ni miongoni mwa mchezo mkubwa unaopendwa sana hapa Zanzibar na Dunia nzima. Pia napenda kumfahamisha kuwa kuvuta kamba na kufukuza kuku ni michezo ya burudani ambayo ipo chini ya Sheria ya Utamaduni.

Mhe. Spika, Karata na Bao ni michezo ambayo inaratibiwa na kuendeshwa chini ya Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo, Sheria Nam. 5 ya mwaka 2010.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na Baraza la Taifa la Michezo tayari imeshaanza kuimarisha michezo hii kwa kuvipatia vyama 19 vifaa vya michezo na itaendelea kufanya hivyo kwa vyama vya michezo vilivyosalia.

Mhe. Spika, pia imeanza kuimarisha miundombinu ya michezo kwa lengo la kuwapatia viwanja vya michezo vya Kitaifa na Kimataifa (*Mao Tse Tung*), (Gombani na Amaan) pamoja na kuanzisha ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya. Sambamba na hilo imeanza kuvipatia mafunzo mbali mbali vyama vya michezo yanayohusu utawala, ukocha na uamuzi wa michezo katika daraja tofuati.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nashukuru Mhe. Spika, pamoja na majibu mzuri ya Mhe. Naibu Waziri wa habari naomba kuuliza swali moja lenye vifungu "a" na "b".

Kwa kuwa michezo ni ajira, na Serikali inatafuta kila aina ya mipango kupunguza wimbi la ajira vikundi hivi vya sanaa vina matatizo ya vifaa na matumizi ya kujiandaa na mazoezi na sare za kuchezea katika sherehe tofauti tofauti.

a) Je, Serikali imewatengea fungu la kujiandaa na vifaa hivyo.
b) Hivi vikundi bado havina mtaji wa kujiendeleza, Je, Serikali imewawekea mitaji ya kujiendeleza ili iendee kila siku na isikatishe kwa kila msimu, je Serikali imewawekea fungu hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba michezo ni ajira kwa vijana, au kwa wachezaji tofauti hapa nchini kwetu na duniani kwa jumla, lakini pia nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali imewatengea fungu wanamichezo hawa na vifaa vya michezo, kwa mfano ni juzi tu timu zetu za michezo ya riadha zimekwenda kwenye mashindano Tanzania Bara ya Afrika ya Mashariki na Kati. Mhe. Rais katoa vifaa hivi kwa michezo, wanamichezo wetu wamefanikisha vizuri na wamekuja hapa wametuletea medali tofauti na kuimarisha michezo, pia na kuitangaza Zanzibar kwamba hii michezo inathaminiwa, na yeye Mhe. Rais pia anaithamini michezo hii.

Mhe. Spika, naomba ajeree swali lake la (b)

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Ningeomba tu Mheshimiwa kusema kitu kwamba swali "b" nalirudia lakini lile swali la kwanza lilikuwa lile la vile vikundi ambavyo viko chini havijawa kama na michezo ya mpira au miguu.

Lakini hilo tuliache, mimi nauliza hili swali la pili, nilikuwa nauliza kwamba hivi vikundi havina mtaji wa kujiendeleza, Je, Serikali imeweka mtaji wa kuviendeleza vikundi hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Naomba niungane na Mhe. Mwakilishi kwamba hivi vikundi vyetu ni kweli havina mtaji, lakini hili nilichukue kutoka kwake kwamba ni ushauri na nimuahidi kwamba tutaufanyia kazi kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Habari, Utalii na Michezo ili nikwambie Mhe.Mwakilishi hili tutalifanyia kazi na tutatenga kifungu maalum cha vikundi hivi ili kiuviinua na kuvipa mitaji navyo vionekane kwamba vinashiriki. (*Makofi*)

Mhe. Makame Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, wachezaji wa mchezo wa bao walifanya sherehe hapa Unguja, Je, kwa kutambua thamani yao wachezaji wale Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba mchezo wa karata na bao unaimarika hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ni kweli kwamba michezo hii ya karata na bao imeimarika sana hapa kwetu Zanzibar, kwa hivyo nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba Wizara na Serikali kwa jumla imejipanga vyema michezo hii kuimarisha na haya mashindano kila mwaka atakuwa ni shuhuda, kuna wananchi wetu kutoka Pemba ambao wanashughulikia Michezo ya karata na bao, wanakuja Unguja kufanya mashindano haya huu ni uthibitisho kwamba michezo hii tunaimarisha na tunaipa kipaumbele kwa Taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nikushukuru sana Mhe. Spika. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri yasiyo na uhakika, naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa umekiri kuwa mtatoa ruzuku kwa vikundi hivi vinavyoshiriki michezo, lakini tukiiona bajeti yako afadhali ya jana kuliko leo na hapa ndipo Baraza hili linapopitisha bajeti. Je, ni kifungu gani unachokiweka kwa wananchi ili tuone michezo imekuwa kwa haraka.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa namna ya umahiri anaouonesha katika kujibu maswali. Hii inaonesha wazi kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo anafuatilia kwa kina sehemu zake anazozifanyia kazi.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba ukiitizama bajeti yetu ukiilinganisha mwaka jana na mwaka huu takriban inalingana, lakini aelewe wazi kwamba bajeti ikisimamiwa ipasavyo basi maendeleo yanaweza kuwa mazuri zaidi kutoka mwaka jana kushinda mwaka huu. Wizara yangu imejipanga vizuri kuisimamia bajeti ambayo italetwa hapa katika kutekeleza yale ambayo yameainishwa katika vifungu vya bajeti, hivyo fungu lililowekwa kwa BTMZ kuweza kuvisaidia vyama vyote vya michezo vikiwemo hivi vyama vya bao na michezo mingineyo itasimamiwa na utaratibu utawekwa na matumaini mazuri yatapatikana, kama tulivyosema na kama lilivyoelezwa suala lililopita kwamba sherehe mwaka jana imefanywa na mafanikio yalionekana. Hivyo fungu lililokuwepo litatumika na litasimamiwa vizuri kuhakikisha michezo hii ya bao, kufukuza kuku na michezo mingine inapewa kipaumbele, na bajeti yetu inasimamiwa ipasavyo. Ahsante sana (*Makofi*)

Nam. 18

Ukosefu wa *Dispensary* kwa Wananchi wa Bungi

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi) - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga mji mpya wa Tunguu, lakini kumekuwa na tatizo la huduma za afya, kwa kuwa kuna Tunguu *Dispensary* pekee inatumiwa na watu wa Binguni, Tunguu, Jumbi na Bungi.

Je, Wizara haioni umuhimu wa kujenga *dispensary* nyengine kwa wananchi wa Bungi kwa sababu wapo wananchi wengi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama hivi ifuatavyo: -

Mhe. Spika, Shehia ya Bungi ina wastani wa wakaazi 2,400 (Sensa ya 2012) ambao kwa sasa wanapata huduma za Afya kwenye kituo cha Afya Tunguu kwa upande wa Kaskazini na Unguja Ukuu kwa upande wa Kusini. Vituo hivi viko umbali wa kilomita 3 hadi 4 kutoka kijiji cha Bungi, Kituo cha Unguja Ukuu kina hadhi ya daraja la pili (*PHCU+*). Ambapo kinatarajiwa kutoa huduma za ziada zikiwemo huduma za uzazi, maabara, madawa na meno. Huduma mbili kati ya hizi yaani maabara na madawa tayari zimeshaanza kutolewa.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein wakati akiomba ridhaa kwa wananchi na kuzinadi sera za CCM katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Bungi aliahidi katika ilani ya CCM kuwa katika kipindi chake cha miaka mitano hospitali kuu ya rufaa itajengwa katika eneo la Bungi la Binguni, yenye uwezo mkubwa wa kimataifa ambayo itahudumia eneo lote la Wilaya ya Kati na Mkoa wa Kusini pamoja na Zanzibar

Mhe. Spika, hatua iliyofikia hadi sasa ni upatikanaji wa kiwanja, uwekaji wa uzio, ramani pamoja na kutayarisha makisio ya gharama za ujenzi wa hospitali hiyo. Sera ya afya ya mwaka 2011 inasisitiza kutoendelea na ujenzi wa vituo vipya na badala yake ni kuviimarisha vilivyopo kuvifanyia matengenezo stahiki, kuongeza vifaa na kujenga nyumba za wafanyakazi ili vituo vilivyopo viweze kutoa huduma kwa masaa 24.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri na hasa katika ujengaji wa hii hospitali ya rufaa itakayojengwa Mkoa wa Kusini hapa Binguni, lakini bado kuna tatizo la huduma kwa wananchi wote japokuwa masafa yaliyotajwa ya kilomita 3 mpaka 4 lakini huduma nyengine huwa hazipatikani kabisa katika eneo hili na hupelekea watu kupelekwa Mnazi Mmoja.

Kwa kuwa binadamu hawezi kusubiri wakati anahitaji huduma hasa wazazi na watoto, ni utaratibu gani utakaotumika baina ya sasa mpaka hospitali kubwa ya rufaa itakapojengwa ili huduma hizi za afya kwa Mkoa wa Kusini Unguja, ziweze kusogezwa kwa karibu zaidi ili wananchi waweze kufaidika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Serikali kama ilivyoahidi kupitia agizo la Mhe. Rais la kujenga hospitali ya rufaa katika kituo hicho bado inasisitiza kwamba uwezo huo upo, na kwamba hospitali itajengwa na tunawaomba wananchi wanaohusika na kituo hicho kwa maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba wanapata shida ya kufuata hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini tunawaomba na tunawanasihi sana katika kipindi cha miaka mitano hii iliyopo basi tunawahakikishia kwamba tutakuwa tayari tumeshajenga kituo chengine cha hospitali ambacho tumeieleza mwanzo na kuweza kutoa huduma ipasavyo. Wakumbuke kwamba kutafuta kuna kazi na kujenga kuna kazi, wao ni wananchi halisi wa nchi hii, tunaamini ni wazalendo, kwa hivyo tunaomba wavumilie hili lakini huduma zitatolewa kwa masaa 24, tunaamini wataridhika.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Namshukuru Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri ni vituo vingapi ambavyo havijamaliza kujengwa katika Wilaya za Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Nakuomba kwa heshima kubwa unipe nafasi ili nikupe kwa maandishi (*Makofi*)

Mhe. Maryam Thani Juma: Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Umetueleza kuwa hatua iliyofikiwa ni upatikanaji wa kiwanja, uwekaji wa uzio, ramani na kutayarisha gharama za ujenzi huo. Je, ni lini ujenzi wa Hospitali hiyo utakamilika ili wananchi waweze kufaidika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya ambaye ameanza kazi kwa umahiri na kuvizungukia vituo vyote 134 vilivyokuwepo Unguja na Pemba na hilo ni miongoni mwa jukumu lake kuu ambalo analifanya, naomba nimpongeze sana kwa majibu hayo mazuri.

Sasa naomba kumjibu Mheshimiwa aliyeuliza swali kuhusiana na suala la Hospitali ya Binguni itakayojengwa ambayo itakuwa ni Hospitali ya rufaa. Katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 176 kifungu (c) miongoni mwa ahadi alizotoa mgombea wakati huo kwa Chama cha Mapinduzi ni kwamba Zanzibar itajengwa Hospitali ya rufaa ya aina yake katika eneo la Binguni, na hayo bahati nzuri alizungumza huko huko katika mkutano uliofanyika Bungi katika jimbo la mwenye kuuliza swali la msingi Mhe. Simai Mohamed Said na alitumia dakika takriban 20 kuizungumzia hospitali hiyo tu.
Hivi sasa tayari ramani imeshakamilika kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri, kiwanja tayari, uzio unaendelea kufanyiwa kazi na tumeshatumwa, imeundwa kamati ambayo inahusisha Wizara ya Fedha, Mhe. Waziri wa Fedha yupo hapa, Wizara ya Afya pamoja na Tume ya Mipango kwa ajili ya kuzungumza na wafadhili kuhusiana na hospitali hiyo. Kwa hiyo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa aliyeuliza swali kwamba madamu ni ahadi ya Mhe. Rais aliyoitoa ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi, ahadi hiyo itakamilika kabla ya 2020, CCM haina kawaida hata siku moja.

Katika ilani iliyopita CCM ilikamilisha ahadi zake zote kwa asilimia zaidi ya 100. Kwa hiyo, haina kawaida ya kwamba kutokamilisha ahadi yoyote inayotolewa ndani ya ilani, hiyo ndio *priority number one*. Kwa hiyo, ahadi hiyo itakamilishwa ndani ya miaka hii minne iliyobakia mpaka 2020. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umekwisha, lakini kabla hatujaendelea naomba nitoe tangazo moja tu la wageni ambalo tunalo hapa, na ni wageni wa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na Mwakilishi wa Jimbo la Amani (Maalim Rashid). Wageni ni Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Amani ambao pia ni viongozi wa jimbo wakiongozwa na Mwenyekiti wao Dkt. Khamis wa Shehia ya Kwa Wazee, naomba unyanyuke kama upo. Ahsante.

Mwisho wa tangazo la wageni, sasa naomba nichukue nafasi hii nimkaribishe Mhe. Naibu Spika ili aje aongoze tuendelee na shughuli yetu. Mhe. Naibu Spika, tafadhali.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, jana tulimaliza wachangiaji na tukasema kwamba leo litakalofuatia tutampisha Mhe. Waziri kwa ajili ya kuja kufanya majumuisho, lakini nimeombwa na Mheshimiwa mmoja ambaye jana hakuwepo Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa hiyo nitampa nafasi aweze kuchangia na baadae tutamkaribisha Mhe. Waziri. Mhe. Mattar karibu.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya mwisho na mimi niweze kupeleka ushauri wangu katika wizara hii. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na salama tukaanza asubuhi yetu hii mambo yetu kwa vizuri sana. Pia naomba nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein katika ziara yake aliyoifanya Kisiwani Pemba ya kwenda kuwapongeza wana CCM pamoja na kuwafariji wana CCM wale ambao wamehujumiwa na kuvunjiwa haki za binadamu, na wenzetu hawa wa Chama cha Upinzani cha *CUF*. Nampongeza sana kwa moyo wake huo wa kwenda kuwafariji wananchi wa Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nampongeza Mhe. Rais kwa kauli yake madhubuti aliyoitoa kwa vyombo vinahusika kwamba sasa viache kulala na

badala yake viweze kuchukua hatua zinazofaa kama vile Polisi na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Naibu Spika, pia natumia fursa hii kumpongeza Rais kwa kumteua Waziri wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) waziri shupavu ambaye ameanza vizuri sana katika wizara yake hii muhimu sana. Namshukuru sana na nampongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Waziri inayosema mpango wa kuratibu sheria Serikali ya Mapinduzi. Kule ingawa imeeleza kwamba ni programu lakini mimi natumia Kiswahili chetu mpango, kama alivyotaka mwalimu wetu tutumie maneno ambayo yanawezekana tuyabadilishe. Mimi natumia mpango wa kuratibu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, nampongeza sana kwa sehemu hii.

Pia naipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia waziri huyu pale ambapo ameiweka sehemu hii kuona kwamba mawasiliano yanapatikana kwa wale wenzetu ambao wako nje ya Zanzibar. Lakini nipongeze zaidi katika eneo hili pale ambapo zile jumuiya zilizoko nje ya Zanzibar zinazofanya kazi na Serikali yetu ya Mapinduzi kuleta mandeleo. Nazipongeza sana jumuiya hizi, jumuiya zenyewe naomba nizitaje ikiwemo Jumuiya ya *Diaspora*, Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Washington DC, Jumuiya ya Wazanzibari waishio nchi za Scandinavia, Jumuiya ya Wananchi wanaoishi Canada (*ZACADIA*) lakini pia siisahau Jumuiya ya Watu wa Finya wanaoishi kule Tanzania Bara, katika kutekeleza majukumu yao itaendelea kuchangia maendeleo ya Zanzibar, naipongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, nakuomba sana katika Baraza lako tukufu tuendelee ule utaratibu ambao Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alikuwa akiutumia, namuomba sana waziri huyu na yeye aige mfano huo. Mhe. Karume Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema alikuwa na utaratibu wa kwamba shughuli zote za maendeleo zinazofanywa Zanzibar (Unguja) anahakikisha kwamba pia zinakwenda Pemba. Sisemi kwamba maendeleo kama haya hayapo yanaendelea vile vile katika uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein lakini nahimiza zaidi. Kusema hivyo ni kutokana niliposoma kitabu hiki pale nilipoziona hizi huduma zinazoletwa na jumuiya zetu hizi zilizo nje ya Zanzibar, naona zimejionesha humu kwamba zinafikia ama maskuli yaliopo hapa Unguja au hospitali zilizopo Unguja. Huduma kama hii inahitajika kwa kule Kisiwani Pemba, ukitizama huduma za elimu hawa madaktari bingwa pia wanahitajika.

Naomba sana sana wataalamu kama hawa wanapokuja basi wafikishwe katika hospitali zetu kule Pemba ili waweze kupunguza matatizo ya afya. Kwani kama tunavyojua kwamba matatizo ya afya ni makubwa sana, jambo dogo mtu anapandishwa ndege Unguja au kwenda Tanzania Bara au kwenda India. Ni imani yangu kwamba mabingwa hawa wanaokuja kutoka nje wakifika kule ikiwa kuna utaratibu mzuri basi wakaweza kupunguza kwa kuwasaidia wale wanyonge ambao uwezo wao kwenda India au kwenda Tanzania Bara kutibiwa huenda ukaondoka. Kwa hivyo, naomba sana sana wenzetu hawa wanapofika kuleta misaada yao basi na wao waziri katika uratibu wake aweze kutuletea mabingwa hawa au wachangiaji hawa wa maendeleo kule Kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichangie katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri kupitia ofisi yake iliyopo Pemba kwamba Mdhamini wetu aliyeko kule Mama shupavu kabisa, ni mwanamke lakini amekazana sana katika kutekeleza majukumu yake.

Nampongeza Mdhamini Bibi Jokha kwa kile kitendo ambacho kuwa ameweza kuwaweka Wadhamini walioko Pemba na kuwaeleza mabadiliko ya tabia nchi pamoja na maradhi ya kipindupindu kwa kuchukua hatua zinazofaa. Hili ni jambo muhimu sana, mabadiliko ya tabia nchi tunaona yanavyotuathiri kipindi kama hiki tulikuwa tunategemea tuwe na mvua za Mchoo, lakini mvua leo zimeruka kutokana na mabadiliko kama haya. Ni dhahiri kwamba watakapolifanyia kazi jambo hili watendaji walioko Kisiwani Pemba mabadiliko haya yanaweza yakakaa sawa tukishirikiana kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika Ofisi hii ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba kuna jambo pia naona nilishauri, kuhusu jengo. Jengo la Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kweli halina hadhi yake imekuwa kama ni nyumba ya mtu tu hivi, ukifika ukaambiwa kama hii ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kweli unaweza ukashangaa.

Mhe. Naibu Spika, tunasema twende na wakati, ofisi tunasema zikae katika ofisi zinazofanana na hadhi yake. Mimi naishauri sana serikali mambo kama haya tutaweza kuona kwamba tunatekeleza kwa vitendo. Naishauri serikali jengo lile livunjwe lote badala ya kufanyiwa ukarabati. Serikali kwa nguvu zake zote za ndani hata ikiwezekana kuchukua mkopo lakini lile eneo tulitumie vizuri kwa kujenga ofisi ya kisasa kabisa. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tutaweza kuokoa pesa zetu na tutaweza kusaidia hata zile ofisi zinazopanga.

Mhe. Naibu Spika, Mdhamini wa Pemba kule katika kikao chake aliagiza kwamba ofisi zilizoko kule kwenye majengo ya kupanga warudi katika majengo ya serikali, lakini yako wapi majengo ya serikali, asilimia kubwa pale Chake Chake yamekodiwa majengo ya watu binafsi. Tutakapoitumia ardhi yetu vizuri hii kwa kujenga majengo yetu kama ya ghorofa tunaweza kuzikusanya ofisi zetu zile tukainusuru fedha yetu hii ambayo inakwenda mikononi mwa wafanyabiashara na sisi fedha zile tukaweza kufanyia mambo mengine ya maendeleo. Nashauri sana pale ambapo uwezo utapatikana basi majengo haya tuweze kuyabadili sura yake ili yaweze kuleta picha nzuri kwa nchi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi nipongeze tu hotuba yake ambayo ameitoa juzi lakini nisisahau kuona yale ambayo tunayapanga basi tuyatekeleze kila inapobidi, tusiwe tunayaweka kwenye vitabu na baadae tukayarudia kwa mwaka wa pili au tukaendelea kuuliza maswala yale yale.

Nampongeza sana Mhe. Waziri na mimi hotuba hii naiunga mkono mia juu ya mia bila ya mabadiliko yoyote. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema, amani, umoja na mshikamano nchini mwetu.

Pili, sina budi kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho juu ya hotuba yetu ya Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa wewe mwenyewe binafsi pamoja na wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia. Lakini kama tujuavyo Mhe. Naibu Spika, kwamba chombo hiki kinatokana na wanasiasa, wanasiasa ambao wanatokana na ridhaa ya wananchi. Kwa kuwa msingi huo, na kwa kuwa nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, Katiba, kanuni na miongozo mbali mbali. Naomba nikumbushe Mhe. Naibu Spika kwamba niliombe sana Baraza lako hili tukufu na hasa Waheshimiwa Wajumbe kwamba turudi tutafakari na tujikumbushe kwamba sisi viongozi tuliopo humu tumechukua dhamana, dhima na ahadi kwa Mwenyezi Mungu katika kuwaongoza wananchi wa Zanzibar. Na kama tunavyojua kwamba wengi wetu humu tumetokana na Chama cha Mapinduzi, na sote ni mashahidi kwamba Chama chetu cha Mapinduzi kabla ya kurudi tena madarakani tulikwenda kwa wananchi kunadi ilani yetu. Ilani yetu ya uchaguzi ndio mkataba unaotupa nguvu ya kutawala, kuongoza na kuendelea kushika

dola, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe turudi twende tukaisimamie Katiba yetu, turudi twende tukaisome na tuielewe vizuri ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu hiyo ndio iliyotupa nguvu ya kushika dola.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi kuwakumbusha wenzangu kwamba ukirudi katika ukurasa 193, kifungu 126 na 127 cha ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi naomba kuwakumbusha kwamba tulipewa jukumu la kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar tuendelee kubaki wamoja, tuendelee kubaki ndugu tunaofanya kazi kwa msingi wa kujitolea katika kuimarisha umoja na mshikamano wetu. Kwa msingi huo naomba sana Mhe. Naibu Spika, tuendelee kufanya wajibu wetu huo kutimiza wajibu wetu huo ni kutimiza matakwa ya kanuni, ni kutimiza matakwa ya ilani tuliyokwenda kuinadi mbele ya wananchi wetu.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, naomba pia niwakumbushe wajumbe wenzangu ukisoma ukurasa 187, kifungu 120 na 121 cha ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tulikwenda tukaahidi mbele ya wananchi kwamba tukipewa ridhaa tutaongoza nchi hii kwa msingi wa kidemokrasia haki na utawala bora, yanayoendelea sasa hivi ni kutimiza ahadi na ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuongoza jamii na katika kuiongoza Zanzibar yetu.

Mhe. Naibu Spika, ukiendelea pia katika ukurasa 210, kifungu 149 (e) tulipewa dhamana Chama cha Mapinduzi kwa Tanzania yote kwa jumla kwamba diplomasia yetu katika mahusiano yetu na nchi nyengine za kimataifa tutakwenda katika mfumo wa diplomasia inayozingatia uchumi pamoja na kuendeleza siasa yetu kama vile ambavyo tumeahidi.

Mhe. Naibu Spika, nimesema niyaseme haya kwa ujumla kuonesha jukumu letu ni nini sisi kama Chama cha Mapinduzi, chama ambacho kimeshika dola na kimepewa ridhaa ya wananchi wetu. Nimekumbusha hili makusudi ili tuendelee kubaki katika mstari ule ambao tunapaswa katika kuongoza jamii iliyotupa ridhaa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa naomba kwa mara nyengine tena, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa kunipa fursa hii kuyakufanya majumuisho ya hoja na michango pamoja na mapendekezo na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, shukurani za pekee zimuendee Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Tunguu aliyewasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wake Mhe. Omar Seif Abeid.

Pia nawashukuru wajumbe wote wa kamati hii kwa kushirikiana nao vizuri tangu wakati wa matayarisho hadi wakati wa kuwasilisha na kupitisha hotuba hii. Niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba sisi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tuko tayari kushirikiana nao kwa kila hali katika kufanikisha wajibu wetu wa kiserikali.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru pia wajumbe waliokuwa hawajachangia lakini imeonekana wazi kuwa wameunga mkono hoja yetu tuliyowasilisha jana. Kutochangia kwao ni dhahiri kwamba wameifahamu vyema hotuba yetu na hivyo tunawashukuru sana Kamati ya Kudumu ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa wananchi wa kuchaguliwa wa Jimbo la Konde kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuongoza na kutushauri nasi tunakubaliana kushirikiana nao.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya wachangiaji wote ni wachangiaji 13 pamoja na mchangiaji wa mwisho Mhe. Shehe Hamad Mattar wa Baraza lako tukufu. Waliochangia hotuba yangu ya bajeti kati ya hao wachangiaji 11 wamechangia kwa kusema na wachangiaji 2 wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwatambua mmoja baada ya mwengine kati wajumbe waliochangia katika hotuba hii.

1. Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi)
2. Mhe. Ali Suleiman Ali maarufu Shihata au Mjomba
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy
4. Mhe. Suleiman Sarahan Said
5. Mhe. Miraji Khamis Mussa
6. Mhe. Suleiman Makame Ali
7. Mhe. Hassan Khamis Hafidh (*Diaspora*)
8. Mhe. Rashid Makame Shamsi
9. Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Masharubu)
10. Mhe. Bihindi Khamis Hamad
11. Mhe. Abdalla Ali Kombo alichangia kwa maandishi
12. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha na yeye kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, hoja walizozitoa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa michangio ilijitokeza dhahiri katika masuala makuu kama ifuatavyo:-

Kwanza walijilenga zaidi katika programu ya kusimamia shughuli za Mhe. Rais na kuimarisha mawasiliano ya Ikulu na programu ya ushirikiano wa kikanda, kimataifa na uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Mambo muhimu yaliyozungumzwa ni mambo sita nayo ni kama ifuatavyo:

1. Utoaji wa huduma kwa Mhe. Rais
2. Kutunza amani na utulivu
3. Ziara zinazofanywa na Mhe. Rais ndani na nje ya nchi
4. Uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za serikali
5. Sera ya *Diaspora* na mchango wao, na
6. Utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Rais nazipokea pongezi zote zilizoelekezwa katika wizara yetu na zilizoelekezwa kwake yeye. Mimi nakubaliana nanyi Waheshimiwa Wajumbe kwamba, amefanya kazi kubwa Mhe. Rais ya kuwatumikia wananchi wetu katika kuwaletea maendeleo. Juhudi na umahiri wake wa kusimamia mshikamano, umoja, amani na utulivu katika nchi yetu ni jambo linaloonekana wazi na hakuna mtu anayeweza kukataa jitihada hizo za Mhe. Rais.

Pongezi na salamu zenu kwa Mhe. Rais nimezifikisha jana jioni mapema baada ya kumaliza kikao chetu cha jioni. Mhe. Rais amefarajika sana kwa pongezi zenu na kumuunga mkono, yamemtia moyo katika kufanikisha majukumu yake haya ya kikatiba na kisheria. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kutoa ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wajumbe nikianza na Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) kwa niaba ya Kamati.

Kwanza nampongeza sana kwa hotuba yake nzuri iliyochanganua mambo kwa ufasaha kabisa. Nakubaliana naye kuwa utaratibu wa bajeti ya Mfumo wa *PBB* ni mpya na una changamoto yake. Namuahidi kwamba serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji ili waweze kuuelewa vizuri mpango huu wa bajeti.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Simai Mohammed pia alisisitiza nia njema ya kukuza taswira ya Mhe. Rais na mawasiliano kwa kutumia njia za kisasa, ahadi yetu

kwamba Rais kuanzia mwezi ujao ataonekana zaidi kidijitali kuliko sasa hivi ilivyo analogi. Hoja yake hii pia imeeleza kulichukua na yeye katika kamati tunamuahidi kwamba wazo lile tumelichukua na tunalifanyia kazi kwa matendo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia uzito wa hoja hii katika bajeti yetu tumeingiza miongoni mwa vipaumbele vya wizara kwa kutumia njia mbali mbali za mawasiliano ikiwemo mitandao ya kijamii mfano *twitter*, *face book* na mengineyo inayokwenda katika mfumo wa *social media*.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na maoni ya kamati kuhusu umuhimu wa Mhe. Rais kukaa na wafanyabiashara na wawekezaji kuzungumza na kubadilishana mawazo kuhusu maendeleo ya nchi yetu. Utaratibu huu upo anakutana nao kila mwaka na kila itakapobidi kama kuna jambo la dharura Mhe. Rais yuko tayari kukutana na hawa, yaani hawa ni wadau muhimu katika kuendeleza maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara la Zanzibar ambalo hutoa fursa kwa wafanyabiashara na wawekezaji kubadilishana mawazo. Aidha, Mhe. Rais amekutana na Wajumbe wa Jumuiya ya wafanyabiashara wa *ZATU* na wengineo.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na maoni ya kamati kwamba zawadi zinazotolewa na Mhe. Rais ziwe na asili ya Zanzibar na jambo hilo ndilo linafanyika. Zawadi zote anazotoa Mhe. Rais ni zile zawadi ambazo zina asili ya Zanzibar, jambo la kuongezea ni faraja kuona zawadi zile sasa tunaziambatanisha na hati za waliozitengeneza ili wanakokwenda waweze kuonekana na kutangaza majina yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa programu ya ushirikiano wa kikanda, kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, kamati imeshauri serikali kuhusu uwasilishwaji wa ripoti za wanaoshiriki mikutano ya kimataifa. Tunapokea ushauri huo na kiutaratibu serikali imetoa maelekezo kwamba Waheshimiwa Mawaziri ripoti zao wanatakiwa kuziwasilisha katika Baraza la Mapinduzi na Makatibu Wakuu wanatakiwa wawasilishe ripoti hizo kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, wakurugenzi na watendaji wengine wanapaswa kupeleka ripoti hizo kwa Katibu Mkuu wa wizara husika.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kuwa na mshikamano na mashirikiano mazuri na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Kufanya hivyo ni matakwa yetu ya kikatiba na sheria za nchi, tutafanya hivyo ili kutimiza wajibu wetu huo wa kikatiba.

Kuhusu uhusiano kati ya Zanzibar na Comoro hususan katika suala la Kampuni ya Hairu**,** naomba kulitolea maelezo kwamba, Mhe. Rais alitembelea nchini Comoro mwezi Septemba, 2014. Katika maeneo aliyotembelea ilikuwa ni pamoja na eneo la uendelezaji wa mradi wa samaki unaosimamiwa na Kampuni ya Hairu iliyotoka Sri Lanka. Zanzibar ilivutiwa sana na mradi huo na kufanya mazungumzo na uongozi wa kampuni hiyo ili kuja kuendeleza mazungumzo kwa lengo la kuwekeza hapa Zanzibar. Ujumbe wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulitembelea Comoro pia nchini Sri Lanka. Hatua iliyofikiwa hadi hivi sasa ni kutiliana saini makubaliano ya awali (*MoU*) na hatua zaidi zitaendelea kuchukuliwa kukamilisha utekelezaji huo kwa njia ya ubia na serikali (*PBB*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu utunzaji wa majengo na kuendeleza ufukwe wa Ikulu ya Mnazi Mmoja, tumepokea ushauri huo wa kamati na tunaufanyia kazi. Vile vile kuhusu kuimarisha Ikulu ya Mkokotoni na Chake Chake, Pemba nao tumeupokea.

Mhe. Naibu Spika, ofisi yangu tayari imeshapewa barua kwa watendaji wa Mahakama wanaokaa katika eneo la Ikulu ya Chake Chake ili nyumba hizo zifanyiwe matengenezo. Naomba niahidi kwamba katika kipindi kisichozidi siku saba tayari wakaazi wale watakuwa wamehama katika majengo hayo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Simai pia alitoa mchango wake binafsi ikiwemo kuweka mazingira mazuri ambao tumeupokea. Aidha, amezungumzia kuhusu kutunuku medani kwa watu mashuhuri, nalo hilo pia tumelipokea, kwa mujibu wa Sheria Nam. 5 ya mwaka 1993 Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametoa mamlaka hayo na uwezo kisheria kuweza kuwatunuku watu medani kama hizo kila pale atapoona kuna haja au sababu ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata au Mjomba) tunamshukuru sana kwa mchango wake mzuri wenye hekina na busara, namuahidi kwamba ofisi yangu itatekeleza wajibu wake katika kumsaidia Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Aidha, kwa upande wa *Diaspora* tutaendelea kuimarisha uhusiano uliopo kwa kuzingatia umuhimu wao katika maendeleo ya nchi yetu. Tunakubaliana na

wazo la Mhe. Mjumbe kwamba ziara za Mhe. Rais za nje ya nchi zina umuhimu mkubwa na zinahitaji kufuatiliwa kwa umakini. Kama ilivyo kawaida yetu ziara hizo huwa tunaziripoti katika hotuba zetu za bajeti na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nadir Abdul-latif tunamshukuru sana kwa kutupongeza na mchango wake tumeusikia na tunaufanyia kazi.

Kuhusu ofisi zetu za ubalozi zinazofanya kazi katika kuwahudumia wana *Diaspora* kwa bahati nzuri ofisi yangu inapokea ripoti za kila robo mwaka kutoka katika balozi zetu na inaonekana kwamba kuna hatua za kuimarisha kwa mashauriano, mashirikiano pamoja na kufanya kazi kwa pamoja baina ya ofisi zetu za ubalozi pamoja na wana-*Diaspora* wanaoishi huko Ughaibuni.

Aidha, tunapokea pongezi zake za dhati za uanzishwaji wa Idara ya Ufuatiliaji wa tathmini na sera na maamuzi ya serikali na tunamhakikishia kwamba idara hiyo itafanya kazi zake kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa mchango wake mzuri. Aidha, ushauri wake katika maeneo mbali mbali tumeuchukua na tunaahidi kuufanyia kazi. Tunakubaliana naye kuwa Mhe. Rais wetu ana nia nzuri kwa wananchi wake; ni muadilifu, mtu mkweli, muaminifu na sio mbaguzi wa aina yoyote. Aidha, kama nilivyosema ni mwenye kuwatakia mema wananchi wake wote.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa (*Father*) kwa mchango wake, tunamuomba na kumhakikishia kwamba, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi itaendelea kuifanya Zanzibar iweze kushiriki katika mikutano mbali mbali ya kikanda kwa mujibu wa fedha zitakazopatikana. Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, kuhudhuria mikutano kuna gharama kubwa kwa serikali, na serikali imeweka hata utaratibu mzuri katika kufanikisha hilo.

Aidha, kwa uratibu wa ofisi yangu inapokea barua zote za mialiko katika ngazi ya mawaziri, makatibu wakuu na wataalamu na kuzipeleka katika sekta husika. Kwa mwaka huu mikutano yote ya wataalamu ambayo imetajwa katika kitabu hiki tuliyoiambatanisha ilikuwa ni mikutano iliyoratibiwa na kusimama na sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Naibu Spika, naomba kueleza kuwa suala la kuwatambua wana-*Diaspora* ni changamoto kubwa, sio tu kwa Zanzibar bali ni kwa Tanzania na nchi zote za Afrika walio na watu hawa wanaoishi Ughaibuni.

Hivi sasa kuna mradi unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia wahamiaji ambalo limeandaa *database* kwa ajili ya kuwatambua *Diaspora* wa Tanzania. Hata hivyo, kama tulivyoeleza, wana-*Diaspora* wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu, namshukuru sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa kutoa ufafanuzi na uelewa wake mpana katika eneo hili la *Diaspora* kwa Zanzibar kuhusu sera ya *Diaspora* kama nilivyoeleza katika mchango wangu wa hotuba ya serikali kuwa maandalizi yamekamilika na yamefikia hatua nzuri katika kuleta sura hii ya wana-*Diaspora*.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumtoa wasi wasi Mhe. Miraji Khamis Mussa kuwa hakuna mgongano wowote kati ya Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050 na Dira ya Zanzibar 2020. Aidha, dira zote zinalenga katika kufikia kiwango cha uchumi wa kati katika kipindi kilichotajwa. Lengo kubwa ni kuondokana na umasikini katika nchi zetu.

Kuhusu Sera ya Mambo ya nje Jumuiya ya Afrika Mashariki imo katika hatua za awali za maandalizi. Hata hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatumia sera ya kidiplomasia ya kiuchumi katika mahusiano yake na nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Suleiman Makame Ali kwa mchango na ushauri wake. Hata hivyo, tunaomba kumuarifu kuwa Mhe. Rais amekuwa na desturi za kufanya ziara kisiwani Pemba, hata jana ametoka kufanya ziara hiyo katika kisiwa cha Pemba. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru sana mwana - *Diaspora* mwenzetu Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa pongezi, mchango na ufafanuzi alioutuoa kuhusu michango ya Diaspora katika nchi yetu. Namuahidi kuwa serikali itaharakisha sera ya *Diaspora* ili iweze kuanza kazi mara moja. Ushauri wangu kama ofisi, itifaki kwa watendaji wa Ikulu na mazingira na nyumba pamoja na wafanyakazi kuvaa nguo za unadhifu nalo tumelipokea na tutalifanyia kazi mapema. (*Makofi*)

Aidha, faida za *Diaspora* zimeelezwa wazi zaidi ya kile kituo kilichopo *EACROTANAL* lakOni pia wajasiriamali wetu wamepata nafasi ya kutanua wigo na kujitangaza walipokwenda katika kushiriki maonesho yaliyofanyika Dar es Salaam na maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana naye kuwa hakuna mradi wa barabara kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika hapa Zanzibar. Mradi mkubwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliolengwa kwa upande wa Zanzibar ulikuwa ni Mradi wa *RoRo* ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari tumeutekeleza sisi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wake kuhusu ahadi za Mhe. Rais. Tutaendelea kuzifuatilia na kuhakikisha kuwa zinatekelezwa. Naomba kumuhakikishia kuwa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi haina nyumba Makunduchi wala Paje ingawa hapo awali zilikuwepo nyumba za mapumziko zilizokuwa zikimilikiwa na Shirika la Utalii.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ikimiliki nyumba nyingi maeneo ya pwani; Makunduchi, Jambiani, Paje, Uroa, Chwaka, na Bwejuu maeneo haya yote nyumba hizi zilikuwa zinamilikiwa na serikali chini ya usimamizi wa Shirika la Utalii. Kwa hivyo, niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi nzuri ya kumhoji Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni, na Michezo atakapowasilisha bajeti yake juu ya nyumba hizi, zile ambazo zimeuzwa utaratibu uliotumika, nani aliyeuziwa kama utaratibu umekamilika ama mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Kamisheni ya Kiswahili utaratibu wake wa ajira kwa mujibu wa makubaliano ya mfumo wa uajiri katika *East African Community* itakuwa kwa wafanyakazi wa ngazi ya *general staff* ambao hawajaanza kuajiriwa, matangazo ya ajira hii yatatoka katika vyombo vya habari.

Mhe. Naibu Spika, natoa wito kwa Baraza hili na wananchi zitakapotangazwa nafasi hizi wale wote ambao wana sifa zitakazotajwa kutumia nafasi ya kwenda kuomba nafasi hizi mishahara yao ni mikubwa, wataalamu wapo. Katika nafasi hizi hakuna nafasi za kuchukuliwa na mjomba, ni nafasi ambazo zinahitaji ushindani watu wetu wepo wenye sifa wajitokeze wende wakashindane na wenzao ili waweze kupata nafasi hizi kama ambavyo wanapata wengine waliopata nafasi ya kuwa na *head quarter* ya Kamisheni katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Yussuf Hassan kwa mchango wake, tunakubaliana naye kuwa bajeti ya *GSO* ni ndogo. Hata hivyo, tunawashukuru wenzetu wa Idara ya Usalama wa Taifa ambao wamekuwa wakifanya kazi

pamoja na kitengo chetu hiki kwa kuwasaidia fedha za kufanyia kazi baadhi ya vitendea kazi na mengine.

Ahadi yetu kwamba, wizara yetu tutahakikisha tunashirikiana na wenzetu hawa katika kuona kuwa tunawasaidia nyenzo ili kutimiza wajibu wa kiserikali katika kuwalinda wafanyakazi wetu katika masuala ya uajiri, upekuzi wa majengo na kuhakikisha kwamba tunaajiri watu waliokuwa waaminifu na utiifu kwa serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la ziara, naomba kumuhakikishia Mhe. Yussuf Hassan kwamba uhusiano wetu na Comoro ni uhusiano mzuri na uhusiano wa kidamu ambao umedumu kwa miaka ya dahari na dahari. Nimhakikishie kwamba hatuwezi kuvunja uhusiano na wenzetu wa Comoro kwani ni watu ambao tumechanganya damu.

Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoeleza kwamba Mhe. Rais amefanya ziara mara kadhaa nchini Comoro, kwa lengo la kuimarisha uhusiano wetu. Vile vile Mhe. Rais wa Comoro alitembelea Zanzibar wakati wa kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi yetu Matukufu mwaka 2014.

Kuhusu heshima ya kiitifaki aliyopewa Mhe. Rais hivi karibuni na wadhifa huo na Mkuu wa nchi kuanzia mapokezi yalifanywa na *Governor* wa Ngazija, msafara wa magari yake pamoja na sehemu stahiki aliyopangiwa wakati wa shughuli ya kuapishwa Rais Mteule wa Comoro.

Mhe. Naibu Spika, yapo maneno ambayo yanasemwa mtaani ya watu ambao wanahombomba. Mimi mwenyewe binafsi nilikuwa shahidi katika shughuli hii ambayo tumekwenda juzi na Mhe. Rais ya kwenda kushiriki sherehe ya kuapishwa kwa Rais mpya Mhe, Kanali Azali Assoumani wa Comoro. Mhe. Rais amewekwa pahali panapostahiki, hata kama angekuja Rais Obama angekaa bega kwa bega na pahali alipowekwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wanaosema (hombomba) hawakuyajua mazingira yaliyoko Comoro, wala hawayajui mazingira halisi ya Comoro. (*Makofi*)

Mazingira aliyowekwa Rais ilikuwa ni ngazi ya tatu kutoka ngazi ya chini; ngazi ya kwanza ilikuwa imekaa familia ya Rais Mteule, ngazi ya pili walikuwa wamekaa marais wastaafu wa Comoro, ngazi ya tatu walikuwa wamekaa viongozi mashuhuri waliotoka dunia nzima ndipo pahali alipokaa Rais wetu. Kwa hiyo, kusema kama Rais amewekwa eneo lisilostahiki ni kujitekenya wewe mwenyewe ukacheka wewe mwenyewe. (*Makofi*)

Niwathibitshie kwamba Rais amekaa sehemu salama na mazingira halisi ya uwanja wa Comoro nendeni mkauone, uwanja wa wenzetu ni mdogo, tunajua yamesemwa haya kwa kuzingatia maendeleo fursa na upeo mpana uliopo katika uwanja wetu wa Amani na Uwanja wetu wa Taifa. Watu wamechukua uzoefu wa shughuli zetu zinapokuwa nzuri, zinavutia katika viwanja vyetu hivi viwili vinavyofanya shughuli kila siku za kitaifa.

Kwa bahati mbaya uwanja wa wenzetu mdogo haukuwa na nafasi ya kuingiza gari ndani, kwa sababu ***kitch*** imekutana na ukuta au uzio wa uwanja husika. Hivyo, niwathibitishie kwamba Mhe. Rais hajabezwa hata kidogo, amepata heshima inayostahiki nchini Comoro. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ripoti za Bango Kitita. Naomba kumuhakikishia Mheshimiwa Mjumbe kuwa hakuna udanganyifu wa aina yoyote unaofanyika. Watu wote wanawakilisha taarifa za Bango Kitita ni wateule wa Mhe. Rais, kama kuna mtu anaongopa basi mimi nina hakika Mhe. Rais hasiti kuchukua hatua kwa mtu atayekuwa amefanya kosa kama hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuarifu Mhe. Yussuf Hassan kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa na utaratibu mzuri wa safari za nje zinazofaywa na viongozi. Utaratibu wa serikali uko wazi kabisa, viongozi wakubwa wanawasiliana na kuomba kuwa ziara yake ya nje angependa kwenda na waziri wangapi na waziri wa taasisi gani, na hivyo ndio utaratibu ambao unatumika hadi hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, fedha za serikali inataka kujitegemea, suala la kuona kwamba kwa nini bajeti imepungua kuna baadhi ya mafungu yamepungua ni jambo la wazi kwamba maamuzi ya serikali yetu ni kuona kwamba tunakwenda katika bajeti inayojitegemea na kujitosheleza. Katika bajeti hii utaona hakuna eneo ambalo tumeweka utegemezi mkubwa kutoka kwa wahisani na washirika wa maendeleo.

Naomba sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu watukubalie maombi yetu ya serikali kuwa na bajeti ndogo inayojitosheleza tuweze kuipanga vizuri tutumie kwa maslahi ya wananchi wetu ili tupige hatua za maendeleo. Ni bora hichi kidogo tulichokuwa nacho kuliko kingi ambacho tunakitegemea kwa wahisani watakaotupa masharti ambayo hayaendani ya utamaduni wetu. (*Makofi*)

Sote ni mashahidi miaka ya mwishoni 2010 hapa kuna masharti mabaya mabaya yametolewa na wahisani lakini masharti waliopewa na Serikali ya Uingereza wakati ule chini ya Waziri Mkuu bwana Cameron.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kumuomba tu Mhe. Yussuf Hassan alitaka ufafanuzi kuhusu ujenzi wa Ikulu ya Micheweni kama alivyoeleza hapo awali. Jambo hili la Ikulu ya Micheweni imeanza kujengwa mwaka 2004 lina changamoto nyingi. Lakini ninachomthibitishia kwamba katika bajeti yetu hii tumetenga shilingi 500 milioni tunaanza na umuhimu wa kujenga nyumba kwa ajili ya walinzi na wasaidizi, baadae tutakamilisha jengo hili ili tuone kwamba katika miaka mitano hii Mhe. Rais jengo hili atalitumia na atalifungua katika kipindi hicho ambacho tunakilinda. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, aidha namshukuru sana Mhe. Bihindi Hamad Khamis kwa michango yake, ufafanuzi pamoja na pongezi alizotupa. Tumuahidi kwamba jengo hili la Micheweni tutalikamilisha na tutalifungua kama vile ambavyo nimeahidi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mwisho naomba sana kuwaasa, kuwakumbusha wana CCM na viongozi wenzangu mliomo ndani ya ukumbi huu, kwamba nchi yetu tumeamua kwenda katika mfumo wa demokrasia, na kama tumekwenda katika mfumo wa demokrasia lazima tukubaliane kuwa na utamaduni wa kuvumiliana. Lakini sote lazima turudi katika kusimamia sheria, Katiba na kanuni zinazoongoza nchi yetu.

Kikawaida katika nchi ambazo zinapata mfumo wa demokrasia mnapomaliza harakati za Uchaguzi Mkuu na kufanya siasa za katika majukwaa, jukwaa pekee la siasa linalobaki linakuwa ni mabunge kama lilivyo Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Naomba sana sisi ni miongoni mwa watu waliopata bahati ya kutumia fursa, jukwaa na membari hii kufanya siasa za nchi yetu. Tutumie fursa, dhamana, haki na bahati hii ambayo tumeipata katika kufanya siasa za kujenga umoja, mshikamano na maendeleo kwa nchi yetu na niwaombe sana tusikubali kuondoshwa katika mstari wetu, sisi kama Chama cha Mapinduzi tumepewa dhamana ya kuongoza dola. (*Makofi*)

Na kama tumepewa dhamana ya kuongoza dola maana yake sisi tuna ilani ambayo ndio mkataba kati yetu sisi na wananchi tunaowaongoza. Wenzetu wanafanya haya kwa makusudi kuranda nje, kupiga kelele, kufanya fujo, kufanya na mambo mengine mabaya. Dhamana yao na dhamira yao ni moja tu,

kutaka kutuondosha katika *proper track* ambayo tunayokwenda nayo sasa hivi tuwafuate wao.

Naomba tusikubali kuondoka katika mstari wetu, tubaki katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu na wanafanya hili kwa kutambua kwamba muda wa kampeni umekwisha, muda wa kufanya siasa umekwisha. Eneo pekee ambalo linapaswa kufanya siasa kikatiba na kisheria ni majukwaa kama haya. (*Makofi*)

Sisi tuliopata fursa hii tutumie fursa hii kutetea maslahi ya wananchi wetu, kutetea maslahi ya wanyonge, kuharakiza maendeleo ya nchi yetu ili tupige hatua kutoka hapa tulipo ili tupate Zanzibar bora, Zanzibar yenye neema huko tunakokwenda. (*Makofi*)

Naomba sana twende tukaisome ilani ya Chama cha Mapinduzi, twende tukasome Katiba, twende tukatimize ahadi ambazo tumewaahidi wananchi wetu.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza lako hili linaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu nyengine za miongozo. Nimesikiliza sana michango ya Wajumbe wote 13 waliochangia na nimefarajika sana kwenye moyo wangu kwamba hakuna Mjumbe hata mmoja aliyeonesha dhamira ya kuipinga hoja ya bajeti yetu ya Makadirio na Mapato ya Afisi ya Rais. Kwa msingi na kwa mujibu wa kanuni ya 98 (6)(c) na (d).

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kabisa kwamba hakuna Mjumbe aliyepata nafasi ya kupiga buti katika bajeti yetu. Haya ni matakwa ya kanuni. Hakuna mtu aliyeonesha dhamira ya kutaka kupiga buti. (*Makofi*)

Naomba tu Mhe. Naibu Spika, usimamie kanuni tupate kupitisha bajeti yetu aje Mhe. Haroun Ali Suleiman apitishe bajeti yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tunakushukuru sana, na kwa maneno ya vijana nimekusoma! (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza lako limeijadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na shughuli yetu naomba kidogo niwatambulishe wageni ambao wapo hapo juu, na wageni hawa ni wa Mhe. Haroun Ali Suleiman Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi.

Wageni hao wanatoka katika Jimbo la Makunduchi wadi ya Muyuni na jumla yao ni 15. Naomba wasimame kama wapo ili muwasalimie Wajumbe. Ahsanteni sana mnaweza kukaa na karibuni sana. (*Makofi*)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU - AO 1	**OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**	
Kifungu PA0101	Programu Kuu ya Kusimamia shughuli za Mhe. Rais na Kuimairisha mawasiliano Ikulu	
Kifungu SA010101	Programu ndogo ya Umma na wadau kwa jumla kuwa na uelewa kuhusu shughuli zinazotolewa na Mhe. Rais	Shs. 2,667,003,000/-
Kifungu SA010102	Programu ndogo ya Kuimarisha mawasiliano baina ya serikali na wananchi	Shs. 200,351,000/-
	Jumla ya Kifungu:	**Shs. 2,867,353,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii nilimuuliza Mhe. Waziri ziara aliyofanya Waziri Mkuu pamoja na Makamu wa Rais, je, Zanzibar walitoka viongozi gani katika misafara hiyo, lakini naona alipotoa majumuisho sikupata ufafanuzi wowote. Sasa naomba anieleze viongozi walioshiriki katika misafara hiyo miwili na kama tunavyojua kwamba katika awamu iliyopita Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete anapofanya ziara kama hizi anakuwa katika *delegation* yake anakuwa na viongozi wanaotoka huku Zanzibar. Kwa hiyo, naomba idadi ya viongozi waliotoka katika misafara hiyo ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, nimesikiliza hoja ya Mhe. Mjumbe, na mimi nimefanya majumuisho na nimelisema hili, kwamba suala la safari ni mawasiliano ya viongozi wakuu, wanaposafiri anamjuilisha kiongozi mkuu mwenzake kama nasafiri nahitaji kutoka na huyu. Sasa pale ambapo kiongozi atakuwa amesafiri hakufanya mawasiliano maana yake hawezi kusafiri na mtu, msingi ni kwamba viongozi hawa Waziri Mkuu na Mhe. Makamu wa Rais wamesafiri hakuna Mjumbe aliyetoka Zanzibar kwa sababu hakukuwa na mawasiliano waliyowasiliana na upande wa pili wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jambo la msingi hili jambo la utamaduni matakwa mazuri ya uimarishaji wa Muungano wetu, si jambo ambalo masharti au Katiba ni jambo ambalo lipo limedumu kwa muda mrefu na mimi naamini hatukupata mualiko kwa sababu maalum, kila hali itakaporuhusu, kila fursa itakapotokea hatuna sababu ya kunyimwa mualiko. Tulikuwa tukipata mialiko hiyo kwa kipindi chote cha Muungano wetu, naamini serikali ndio zimeanza kule Awamu ya Tano hapa Awamu ya Saba katika kipindi cha pili. Namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba kila fursa itakapotokea imani yangu kwamba tutapata mualiko viongozi wa Zanzibar tutashiriki ziara hizo za kimataifa na viongozi hawa wakuu wa nchi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mimi nataka labda anithibitishie katika ziara zinazokuja hili litafanyika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, lazima tujue utaratibu wa kuendesha serikali. Utaratibu wa

kuendesha serikali uko wazi mimi natamani sasa hivi kwenda Geneva, lakini taratibu niombe nipate ruhusa na suala la mualiko ni yule mwenye ile shughuli yake kukualika. Sasa ukinambia mimi nikupe *commitment* kwamba Rais ataalikwa siwezi kufanya kitu hicho, imani yangu kwamba Mhe. Rais na Viongozi Wakuu kila watapoona kuna fursa na haja watatoa hii mialiko na tutapata nafasi ya kwenda.

Kwa hiyo, sisi hatuwezi kuji-*commit* kwamba Rais wa Jamhuri atatualika, imani yetu, matarajio yetu na mapendekezo tu, na kwa sababu hili jambo lipo, ni utamaduni wa siku nyingi, tujenge imani tu kwamba tutapata mialiko na tutashiriki ziara hizo. (*Makofi*)

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri *concern* yangu hajaelewa kwa vile msafara unaotoka ni wa Tanzania na Zanzibar ni miongoni mwa Tanzania, nafikiri tumefahamiana. Sasa kama Zanzibar ni miongoni mwa Tanzania na safari zile zinakuwa ni nje ya nchi lazima huku watu watoke na hili suala vile vile tumo katika kuimarisha huo Muungano wenyewe. Sasa tukianza kutengana sasa hivi huo Muungano tutakuwa tunauimarisha? Mhe. Mwenyekiti lakini tuendelee.

Kifungu PA 0102	Programu Kuu ya Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Uratibu wa Zanzibar wanaoishi nchi za nje	
Kifungu SA010201	Programu ndogo ya Kuiwakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kikanda na kimataifa	Shs. 264,673,000/-
Kifungu SA 010202	Programu ndogo ya Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya Diaspora	Shs. 239,847,000/-
Jumla ya Kifungu:		**Shs. 504,520,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PA 0103 Programu kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu

Kifungu kidogo SA010301 Programu ndogo ya kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu Shs. 1,122,435,000/-

Kifungu kidogo SA010302 Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Shs. 300,778,000/-

Kifungu kidogo SA010303 Programu ndogo ya Kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba Shs. 663,113,000/-

Kifungu kidogo SA010304 Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma Shs. 40,000,000/-

Jumla ya Kifungu: Shs. 126,326,000/-

Jumla Kuu: **Shs. 5,498,200,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU A02 OFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu PA 0201 Programu kuu ya usimamizi wa majukumu ya Kikatiba na Kisheria Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu.

Kifungu kidogo SA020101 Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake Shs. 109,200,000/-

Kifungu kidogo SA020102 Programu ya Tathmini ya uwajibikaji na utendaji kazi wa taasisi za umma Shs. 35,360,000/-

Kifungu kidogo SA020104	Programu ndogo ya ukuzaji ufanisi wa kitengo cha TEHAMA	Shs. 31,930,000/-
	Jumla ya Kifungu:	**Shs. 176,490,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PA0202	Programu Kuu ya Utumishi na Utawala Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	
Kifungu SA020201	Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	Shs. 1,179,210,000/-
Kifungu SA020202	Programu ndogo ya Uimarishaji uwezo wa ofisi katika kusimamia sera, sheria, utumishi wa umma na uhifadhi wa nyaraka	Shs. 136,300,000/-
	Jumla Kuu ya Fungu A 02	**Shs.1,492,000,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio haya.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tayari ameshatoa hoja. Sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kukubaliwa)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe nimshukuru sana Mhe. Waziri na basi tumtakie heri na mafanikio katika utekelezaji wake na kazi zake za kipindi cha 2016/2017.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe tuna muda wa kutosha kabisa kumsikiliza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima, hekima na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa ushindi wa kishindo alioupata katika Uchaguzi wa Marudio uliofanyika mwishoni mwa mwezi wa Machi mwaka huu. Ushindi huo alioupata Dkt. Shein ni dalili tosha ya imani ya wananchi waliyonayo juu yake, hasa katika umahiri wake wa kuiongoza na kuiletea maendeleo Zanzibar.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, mapitio ya utekelezaji wa ahadi zake yanaonesha kwamba, chini ya uongozi wake mahiri, Serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wa Zanzibar wakati wa uchaguzi Mkuu kama zilivyoainishwa katika ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha kwanza cha awamu ya saba chini ya uongozi wake, yamepelekea kukua kwa uchumi wa nchi yetu, kiasi cha kuwavutia Wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini na Washirika wa Maendeleo kuendelea kuiunga mkono Serikali yetu.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wake Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi wa kishindo alioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015. Ushindi huu unadhihirisha upendo, imani na msimamo wa wananchi wa Tanzania kwa Mhe. Magufuli na kwa Sera na Ilani za chama cha Mapinduzi.

Kuna ishara na dalili kadhaa zinazoonesha kwamba, kwa kipindi kifupi chini ya uongozi wake, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanza kutekeleza kwa kasi kubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu, kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pongezi zangu za dhati zimwendee Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza shughuli mbali mbali za Umma na kusimamia vyema utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Kuteuliwa kwake na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mara ya pili kushika nafasi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni ishara tosha ya juhudi ya kazi nzuri na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha kwanza cha miaka mitano iliyopita.

Hotuba yake aliyoitoa kwenye Baraza lako Tukufu wakati akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya mwaka 2016/2017 ni kielelezo cha ukomavu wake katika uongozi na imeonekana mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka huu. Ni dhahiri kwamba mafanikio tuliyoyapata yamechangiwa, pamoja na mambo mengine, na miongozo na maelekezo anayotupa, ambayo yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu tuliyopangiwa na Serikali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua tena kuwa Waziri wake Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ninaahidi kuwa mtiifu kwake na wananchi wote wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Machano Othman Said, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala. Pia nampongeza Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mwakilishi wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote walioteuliwa katika Kamati hii. Aidha,

nawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wote walioteuliwa kwenye Kamati mbali mbali za Baraza lako Tukufu.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti na Makamu wake kwa ushauri, maelekezo na ushirikianao mzuri iliyotupatia wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Barazani hotuba hii ya Bajeti. Wizara yetu itaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati hii wakati tukitekeleza malengo yetu kwa mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Baraza letu Tukufu. Mimi naamini ushindi uliopata unatokana na rekodi ya busara na hekima uliyonayo. Pia nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa kushika dhamana hiyo. Vile vile nampongeza Mhe. Shehe Hamad Mattar, Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani kwa kuchaguliwa kushika nafasi ya Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nampongeza pia Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed, Mwakilishi wa Jimbo la Donge kwa hotuba zake mbili muhimu ikiwemo ya Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/2016 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017 pamoja na hotuba ya mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naishukuru familia yangu kwa msaada wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Shukurani za pekee ziende kwa wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kwa mara ya nne na kwa kura nyingi niendelee kuwatumikia katika kuwaletea maendeleo, na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa, ambao unanipa faraja ya kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo. Nawaahidi sitowaangusha na nitakuwa karibu nao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri, Mhe. Khamis Juma Maalim; Katibu Mkuu, Ndugu Asha Ali Abdulla; na Manaibu Makatibu Wakuu, Ndugu Yakout Hassan Yakout na Ndugu Kubingwa Mashaka Simba

kwa ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu, ambao pamoja na mambo mengine, umewezesha kuandaliwa kwa hotuba hii.

Pia napenda kuwashukuru Wenyeviti, Makamishna, Wajumbe wa Bodi, Watendaji Wakuu wa Kamisheni, Tume na Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa utendaji na ushirikiano walioanza kunionesha na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi nilionayo. Nawashukuru Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao wamefanya kazi kubwa katika kukamilisha Hotuba hii na kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kutoa pole kwa wananchi wenzetu waliopoteza ndugu zao kutokana na majanga mbali mbali yaliyotokea katika kipindi hiki, yakiwemo kipindupindu na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbali mbali hapa nchini. Tunawaombea Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *Ameen*.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumaliza utangulizi huu napenda kutoa pongezi kwa Wawakilishi wote waliochaguliwa katika uchaguzi mkuu wa marudio tarehe 20 Machi, 2016. Pongezi nyingi kwa Wawakilishi waliopata uteuzi wa Mhe. Rais pamoja na Mawaziri na Manaibu Mawaziri katika wizara mbali mbali. (*Makofi*)

MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

Mhe. Naibu Spika, kimuundo, Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Taasisi zinazojitegemea 14 na Idara 8 zilizo chini ya Wizara moja kwa moja kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa sita hadi saba. Taasisi 14 zinazojitegemea chini ya Wizara hii ni:

i. Kamisheni ya Utumishi wa Umma;
ii. Tume ya Utumishi Serikalini;
iii. Chuo Cha Utawala wa Umma;
iv. Mahkama;
v. Tume ya Utumishi ya Mahkama;
vi. Afisi ya Mwanasheria Mkuu;
vii. Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;
viii. Ofisi ya Mufti;
ix. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana;
x. Tume ya Kurekebisha Sheria;
xi. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;

xii. Tume ya Maadili ya Viongozi;
xiii. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na
xiv. Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki.

Mhe. Spika, Idara nane ambazo zipo chini ya Wizara moja kwa moja ni:

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
iii. Idara ya Miundo na Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi;
iv. Idara ya Mipango ya Rasilimaliwatu;
v. Idara ya Serikali Mtandao *(e-Government)*
vi. Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa
vii. Idara ya Utawala Bora; na
viii. Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina majukumu yafuatayo:

i. Kuandaa na kusimamia mipango, sera, sheria na tafiti zinazohusiana na Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma, na Utawala Bora;
ii. Kusimamia shughuli za utawala, uendeshaji na utumishi katika Ofisi;
iii. Kusimamia utawala bora;
iv. Kusimamia shughuli za mhimili wa Mahkama;
v. Kusimamia shughuli za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;
vi. Kusimamia shughuli za Mkurugenzi wa Mashtaka;
vii. Kusimamia shughuli za Tume ya Kurekebisha Sheria;
viii. Kusimamia utekelezaji wa Katiba za Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
ix. Kusimamia Utumishi wa Umma;
x. Kusimamia utunzaji, uhifadhi, na utumiaji wa Nyaraka na Kumbukumbu;
xi. Kusimamia Serikali Mtandao *(e-Government);*
xii. Kujenga uhusiano na ushirikiano mzuri na vyombo vya kitaifa na kimataifa;
xiii. Kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Mufti;
xiv. Kuratibu na kusimamia shughuli za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana;
xv. Kusajili na kusimamia Taasisi zisizo za Kiserikali; na
xvi. Kusimamia shughuli za Ofisi ya Hakimiliki.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa maelezo ya muhtasari wa mapato na matumizi na mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Muhtasari wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya TZS. 18,662,428,919 Kati ya fedha hizo, TZS. 11,370,350,169 zilipangwa kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na TZS. 7,292,078,750 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 jumla ya TZS. 12,183,520,472 (65%) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, TZS. 9,277,672,955 (82%), kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na TZS. 2,905,847,517 (40%) kwa matumizi mengineyo. Vilevile, Wizara ilikadiriwa kutumia ruzuku ya TZS. 1,354,500,600 na hadi kufikia Machi 2016 imepokea TZS. 920,392,402 (68%). Aidha, kwa kazi za maendeleo TZS. 1,700,000,000 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, TZS. 600,000,000 ni Mchango wa Serikali na TZS. 1,100,00,000 ni msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2016, TZS 422,719,000 (25%) zimepatikana, ambapo TZS. 65,000,000 (11%) ni Mchango wa Serikali na TZS. 357,719,000 (33%) zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ofisi pia ilikadiria kukusanya TZS. 150,000,000 ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi 2016, fedha zilizokusanywa ni TZS. 176,507,923 (118%) (*Viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).*

Mapitio ya Utekelezaji wa Malengo kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia Mafungu tisa ambayo ni G01 - Ofisi Kuu; G02 - Mahkama; G03 - Afisi ya Mwanasheria Mkuu; G04 - Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; G05 - Tume ya Kurekebisha Sheria; G06 - Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu; G07 - Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; G08 - Kamisheni ya Utumishi wa Umma na G09 -Tume ya Utumishi Serikalini.

G01 -Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika**,** Fungu la G01 linahusisha Programu tano ambazo ni Progaramu ya Usimamizi wa Rasilimali watu na Miundo ya Taasisi, Programu ya Usimamizi wa Nyaraka na Mawasiliano ya Serikali, Programu ya Utawala

bora na Haki za Binadamu; Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini; na Programu ya Mipango na Utawala. Vile vile katika fungu hili kuna Programu ndogo 10.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 utekelezaji wa programu za Fungu G01 ni kama ifuatavyo:

Programu G0101: Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Mifumo na Miundo ya Taasisi

Mhe. Naibu Spika, programu hii inatekeleza programu ndogo mbili ambazo ni Maendeleo ya Rasilimaliwatu na Maendeleo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi.

Programu ndogo: *Maendeleo ya Rasilimaliwatu*

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kuendeleza mipango ya upatikanaji wa watumishi wenye sifa watakaopelekea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 programu hii, ilitayarisha Muongozo wa Mpango wa Miaka Mitano wa Rasilimali watu na Muongozo wa Urithishaji Uongozi *(Succession Plan)* na kuwasilishwa katika Wizara, Idara na Taasisi za Umma kwa utekelezaji. Mapitio ya Ikama "*Norminal Roll*" ya mwaka 2015/2016 yamefanyika na Ikama ya mwaka 2016/2017 kwa Wizara zote imeidhinishwa. Aidha, vikao vya Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vimefanyika na vilijadili masuala mbali mbali yanayohusu watumishi na utumishi wa umma.

Mhe.Naibu Spika, uratibu wa upatikanaji wa fursa za mafunzo umefanyika, ambapo watumishi 46 kutoka taasisi mbali mbali wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali katika nchi za Korea, Japan, Indonesia na mtumishi mmoja amepatiwa mafunzo ya muda mrefu nchini India. Vile vile, mtumishi mmoja alishiriki katika Mkutano wa Jumuiya ya Uongozi na Utawala wa Umma Afrika (*AAPAM*) uliofanyika nchini Zambia.

Mhe. Naibu Spika, kazi za kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Watumishi kwa njia ya kielektroniki imeendelea na tayari Wizara zote zimeshaingiza taarifa za Watumishi wao katika Mfumo huo.

Programu ndogo: *Maendeleo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi*

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kuimarisha mfumo wa miundo ya kiutumishi na maslahi ya watumishi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, programu hii imefanya mapitio ya posho za safari za ndani na nje ya nchi, posho za mazingira maalumu, posho za Maafisa Sheria, Makatibu wa Mawaziri na Watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waliohamishiwa Tanzania Bara ili ziendane na gharama za maisha.

Mhe. Naibu Spika, Wizara saba zimetayarisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja yenye azma ya kuimarisha huduma kwa wananchi. Aidha, Mapendekezo ya Muundo wa Serikali na Majukumu ya Taasisi yaliandaliwa na kuwasilishwa katika kamati ya Makatibu Wakuu na kujadiliwa.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho ya mishahara kwa Watumishi wazoefu wa muda mrefu kuanzia miaka 15 na mazingatio maalumu ya marekebisho kwa walimu wenye uzoefu wa miaka 30 yamefanyika. Vile vile, kwa kushirikiana na Bodi ya Mishahara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zoezi la kufanya tathmini ya majukumu ya kazi na kupanga madaraja linaendelea, ambapo tayari taarifa zimekusanywa kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

Programu G0102: Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali

Mhe. Naibu Spika, programu hii inatekeleza programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi na Uendeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

Programu ndogo: *Usimamizi na Uendeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano*

Mhe. Naibu Spika, lengo la Programu hii ndogo ni kuendeleza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika utoaji wa huduma na shughuli nyengine za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, programu hii imeziunganisha Taasisi 53 za Serikali katika kituo kikuu cha taarifa *"Data Center".* Aidha, ushajihishaji umefanyika kwa Taasisi 11 za umma ili kuweka mifumo yao ya taarifa katika kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa.

Mhe. Naibu Spika, uratibu wa utekelezaji wa mpango wa awamu ya pili wa Serikali mtandao katika masuala ya kodi *(e-Tax)* na huduma za afya *(e-health)* ulifanyika na tayari utiaji sahihi makubaliano ulifanyika kwa mradi wa e-health. Kwa upande wa mradi wa *e-tax* tathmini ya kitaalamu inaendelea na makubaliano yanategemewa kufikiwa mwaka huu wa fedha na kuanza utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, anuani za barua pepe kwa Watendaji Wakuu wa Serikali zimetayarishwa na kusambazwa kwa wahusika ili watumie anuani hizo wanapofanya mawasiliano yanayohusu shughuli za Serikali. Utaratibu huu pia utaendelea kwa watumishi wa ngazi nyengine.

Programu ndogo: *Uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa*

Mhe. Naibu Spika, programu hii ndogo ina lengo la kuhifadhi na kusimamia Nyaraka na kumbukumbu za Taifa kwa matumizi ya Serikali na jamii kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia programu hii, vifaa vipya vya kielektroniki vimefungwa katika jengo la kuhifadhia nyaraka ili kuendelea na kazi ya kuzihamisha Nyaraka katika Mfumo wa kieloktroniki. Aidha, majalada 175 yameshahifadhiwa katika mfumo huo.

Mhe. Naibu Spika, ukaguzi wa kumbukumbu zilizopo katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali umefanyika pamoja na kutoa mafunzo mafupi ya Utunzaji na Usimamizi bora wa Kumbukumbu kwa Taasisi 18 za Serikali. Vile vile, katika utoaji wa huduma kwa jamii, Watafiti wapatao 401 wamepatiwa huduma, ambapo kati yao, 355 ni Watanzania na 46 ni wageni. Aidha, Jengo la ofisi ya Idara ya Nyaraka Pemba linaendelea kufanyiwa matengenezo ili liweze kutumika kuhifadhia Nyaraka.

Programu G0103: Utawala Bora na Haki za Binadamu

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya programu hii ni kuimarisha misingi ya utawala bora katika utendaji wa taasisi za umma.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 Programu hii imeweza kutoa elimu ya uraia vijijini kwa kuendesha mikutano saba ya Kamati za Ushauri za Shehia za Unguja na mikutano sita Shehia za Pemba. Pia iliandaa na kurusha hewani vipindi 22 vya redio, vipindi nane vya televisheni na maelezo baada ya habari vyenye mada zinazohusu maudhui tofauti ya kuimarisha misingi ya utawala

bora. Kwa Pemba vipindi 9 vya redio vilirushwa hewani kupitia Redio Jamii ya Mkanyageni.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo ya walimu wanaofundisha elimu ya uraia yalitolewa katika kituo cha kufundishia walimu Bububu. Aidha, vitabu vya sera ya utawala bora katika Vyuo vya Elimu ya Juu vilisambazwa ili viweze kutumika kama ni rejea kwa wanafunzi wa vyuo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, rasimu ya ripoti ya mwaka ya Utawala bora yenye kuonesha tathmini ya hali halisi ya utawala bora imewasilishwa kwa wahusika wengine ili kupata maoni yao. Vile vile, kikao cha ushirikiano baina ya taasisi za SMT na SMZ zinazoshughulikia masuala ya utawala bora kilifanyika katika ngazi ya Wataalamu na Makatibu Wakuu, kwa lengo la kukuza ushirikiano na kubadilishana uzoefu.

Programu G0104: Usimamizi wa Masuala ya Dini

Mhe. Naibu Spika, lengo la Programu hii ni kuratibu na kusimamia shughuli zinazoihusu Ofisi ya Mufti, kwa kutoa fatwa na kutoa miongozo kuhusu masuala ya dini.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, Madrasa 85 na Misikiti 35 imesajiliwa Unguja na Pemba na vyuo vya Qur-ani 52 na misikiti 35 vimetembelewa kwa lengo la kushauriana na kutoa nasaha na ushauri juu ya maendeleo ya taasisi hizo. Aidha, migogoro ya misikiti mitano imepokelewa, migogoro minne imetatuliwa na mgogoro mmoja unaendelea na hatua za kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya masuala 142 yanayohusiana na ndoa, talaka na mirathi yamejibiwa, migogoro 55 ya ndoa imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi na vipindi 85 vya masuala na majibu ya mambo mbali mbali yanayohusiana na dini vimerushwa kupitia *ZBC Redio*.

Mhe. Naibu Spika, ushirikiano na Taasisi za kidini za ndani na nje ya nchi umeimarishwa kupitia Taasisi ya "*Friends of Zanzibar"* kwa kufanya mkutano uliohusu kusisitiza umoja, mshikamano, amani na utulivu. Mkutano huo uliwashirikisha Mamufti na Makadhi kutoka Angola, Zambia, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda na wenyeji Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na *UNDP* mikutano inayosisitiza umuhimu wa amani na utulivu kabla na baada ya uchaguzi imefanyika katika

wilaya zote za Unguja na Pemba kwa kuwashirikisha wahusika mbali mbali. Maktaba ya Kiislamu inaendelea kuimarishwa kwa kuongeza upatikanaji wa vitabu muhimu kwa ajili ya maktaba hiyo.

Programu G0105: Mipango na Utawala

Mhe. Naibu Spika, programu hii inatekeleza programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala; Mipango, Sera na Utafiti; na Uratibu wa Masuala ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Pemba.

***Programu ndogo**: Uongozi na Utawala*

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kutoa huduma za kiofisi, kusimamia Watumishi na kuratibu shughuli za Ofisi kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia programu hii, vikao vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji, Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi, pamoja na vikao vya Washirika wa Maendeleo vimefanyika, ambapo vilijadili masuala mbali mbali kuhusiana na ajenda zilizowasilishwa. Aidha, Ripoti za Ukaguzi za Julai – Septemba na Oktoba – Disemba 2015/16 zimewasilishwa kwenye Kamati ya Ukaguzi ya Wizara na kujadiliwa na ripoti ya mwaka ya upatikanaji wa fedha (*Financial Statement*) imeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, huduma mbalimbali za kiutawala na uendeshaji zimetolewa zikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la ofisi.

Mhe. Naibu Spika, uratibu wa masuala ya upatikanaji wa habari umefanyika kwa kurusha matangazo ya TV, kutoa mafunzo kwa Kamati ya uhariri wa taarifa za mtandao, kuchapisha na kusambaza vipeperushi vya Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria.

Mhe. Naibu Spika, masuala mtambuka yameratibiwa kwa kuendesha mafunzo maalumu kwa maafisa wa wizara juu ya masuala yanayohusu shughuli za Watu Wenye Ulemavu na mapambano dhidi ya UKIMWI na mazingatio yake katika mipango ya kazi.

***Programu ndogo**: Mipango, Sera na Utafiti*
Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kuimarisha shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na usimamizi wa Programu/Miradi ya Ofisi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia programu hii, mipango ya bajeti na ripoti za utekelezaji zimeandaliwa na kuwasilishwa sehemu husika. Misingi ya kuweka mfumo imara wa ufuatiliaji na tathmini imewekwa kwa kuwaelimisha watendaji juu ya kuandaa na kuutumia mpango wa bajeti inayotumia programu (*PBB*) na Mpango wa Ufuatiliaji Utendaji *(Performance Management Plan).*

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, uratibu wa uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya umefanyika na tayari taarifa maalumu iliwasilishwa katika ngazi husika Serikalini na maoni yaliyotolewa yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, uratibu wa Miradi ya Wizara umefanyika kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko ya Utumishi wa Umma na Programu ya Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria, pamoja na Mradi wa Kuhuisha Nyaraka (*Digitization*) na Mradi wa Uimarishaji wa Serikali Mtandao.

Mhe. Naibu Spika, rasimu za Sera ya Msaada wa Kisheria Zanzibar *(Zanzibar Legal Aid Policy),* Sera ya Malipo ya Utumishi wa Umma na Sera ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa zimetayarishwa na zipo katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, Sheria nne zimefanyiwa mapitio ambapo nyaraka zake zimetayarishwa kwa ajili ya kuwasilishwa rasmi katika vikao vya Makatibu Wakuu. Sheria hizo ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria ya Adhabu, Sheria ya Mwenendo wa Madai na Sheria ya Ushahidi.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo Wakuu wa Taasisi za sekta ya Sheria na sekriterieti ya programu ya mabadiliko katika sekta ya sheria yamefanyika. Mafunzo mengine ni kuhusu uzingatiaji na ushughulikiaji wa masuala ya jinsia katika vyombo vya sheria, utunzaji wa kumbukumbu, mafunzo ya vinasaba (*forensics*) kwa wahusika wa masuala ya jinai, usimamizi wa mikataba, usaidizi wa sheria na mafunzo ya utekelezaji sera.

Programu ndogo: *Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Pemba*

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kuleta ufanisi katika uratibu wa shughuli zote za ofisi Pemba zikiwemo kutoa huduma, kusimamia watumishi na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Ofisi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia programu hii, mpango kazi na ripoti za utekelezaji wa shughuli za Ofisi Kuu Pemba imeandaliwa na

kuwasilishwa kunakohusika. Aidha, Taarifa za Watumishi ziliingizwa katika mfumo wa kompyuta na maandalizi ya *''nominal roll''* yamefanyika;

Mhe. Naibu Spika, shughuli za dini, utumishi wa umma, utawala bora, uendeshaji mashtaka, usikilizaji wa kesi, ukaguzi wa hesabu za Serikali, udhibiti wa rushwa na uhujumu uchumi zimeratibiwa na kusimamiwa.

TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inazo taasisi tatu zinazopokea Ruzuku ambazo ni: Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Chuo cha Utawala wa Umma na Afisi ya Hakimiliki. Utekelezaji kazi katika taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Kamisheni ya Wakfu ni kusimamia mali za wakfu, mali za amana, mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi kitaifa, Hijja, Zakka, Sadaka na Misaada ya kheri.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, Tirka 580 za mirathi zimefunguliwa na tirka 414 zenye thamani ya TZS. 8,353,759,733 zimefungwa na warathi kupewa haki zao. Katika usimamizi wa mirathi mizozo 35 imeshughulikiwa, kati ya hiyo, mizozo sita imepatiwa ufumbuzi, mizozo 26 inaendelea kupatiwa ufumbuzi na kesi 43 zimesimamiwa katika mahkama mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika, nyumba 236 za Wakfu zimekaguliwa, ambapo matokeo ya ukaguzi huo yalionesha Nyumba 10 zilihitaji matengenezo ya haraka na TZS. 25,875,000 zilitumika kwa matengenezo hayo. Aidha, kodi yenye thamani ya TZS. 285, 437,500 ya nyumba za wakfu, TZS. 69,594,000 za mashamba na TZS. 51,347,550 za nyumba za amana zimekusanywa na fedha hizo tayari zimegawiwa kwa wanufaika.

Mhe. Naibu Spika, mahusiano na ushirikiano na taasisi mbalimbali za kidini ndani na nje ya nchi umeimarishwa ambapo, Zakka na misaada ya kheri yenye thamani ya TZS. 277,772,000 imekusanywa. Kati ya misaada hiyo, misaada yenye thamani ya TZS. 273,312, 500 imegawiwa kwa wahitaji Unguja na Pemba. Aidha, watu 20 kutoka Wilaya saba za Unguja wamenufaika na zakka.

Mhe. Naibu Spika, sala, mabaraza ya Iddi na shughuli za Hijja zimeratibiwa. Taasisi 16 za Zanzibar zimehudumia jumla ya mahujaji 1,518 kati ya 2,581 waliopelekwa kwa Tanzania nzima (*angalia Kiambatanisho 7).* Katika tukio la ajali ya Mina Watanzania zaidi ya 20 walifariki, kati ya hao Wazanzibari ni watatu. Mungu awalaze pahala pema peponi aamin na awape subra waliofiwa na jamaa zao.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni kwa kushirikiana na umoja wa taasisi za hijja Zanzibar na taasisi za kifedha zikiwemo *PBZ Islamic Banking***,** ZIC-Takaful na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wamo katika hatua za mwisho za kuanzisha mfuko wa hijja ili kuwawezesha waislamu wengi zaidi kuweza kuhiji.

Chuo cha Utawala wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Utawala wa Umma kina jukumu la kusimamia mafunzo na mendeleo ya Rasimaliwatu katika Utumishi wa Umma na jamii kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, Chuo kimetoa mafunzo kwa Watumishi 759 Kutoka Taasisi za Serikali, Mashirika na Taasisi zisizo za Serikali katika fani za Utawala, uandishi wa ripoti, Uandishi wa Miradi na Uhudumu. Idadi hii inajumuisha Watumishi wapya 111 kutoka taasisi mbali mbali za Serikali waliopatiwa mafunzo elekezi.

Mhe. Naibu Spika, mitaala minane ilipitiwa na kufanyiwa marekebisho na mitaala mipya sita iliandaliwa kwa ajili ya mafunzo ya Shahada ya kwanza katika fani ya Menejimenti ya Rasilimali Watu na Utunzaji kumbukumbu. Aidha, Wanafunzi **1,995** katika ngazi ya Msingi, Cheti na Stashahada walifanya mitihani yao kwa muhula wa Julai – Disemba, 2015 ambapo miongoni mwao Wanafunzi 1,290 walimaliza Chuo na kutunukiwa vyeti. Vile vile, Ujenzi wa Ghorofa ya kwanza ya Jengo la Chuo umefikia hatua ya uezekaji.

Afisi ya Hakimiliki

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Afisi ya Hakimiliki ni kusimamia matumizi halali ya hakimiliki ili kuhakikisha hali, hadhi na maslahi ya wabunifu na wasanii yanaimarika.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, kazi za hakimiliki zipatazo 120 za makundi tafauti zimesajiliwa na taarifa zake kuingizwa katika mfumo wa

taarifa wa kielektroniki - *WIPOCOS (WIPO Software for Collective Management of Copyright)* kwa ajili ya kutunza kumbukumbu (*Kiambatanisho nam. 8 kinahusika).*

Mhe. Naibu Spika, mirabaha yenye thamani ya TZS. 48,846,750 ilikusanywa na utaratibu wa kuigawa kwa wenye hakimiliki wapatao 1,237 umekamilika na inatarajiwa kugaiwa mwezi Julai 2016. Aidha, Ofisi inaendelea kukabiliana na changamoto za ugumu wa ulipaji wa mirabaha kwa baadhi ya watumiaji hasa vituo vya utangazaji.

Mhe. Naibu Spika**,** tani moja za vinasa sauti na picha haramu zilikamatwa na kuangamizwa katika ukaguzi uliofanyika katika maeneo ya Mkoa wa Mjini/Magharibi na Kaskazini Unguja na Mikoa yote ya Pemba. Vile vile, vipindi 17 vya televisheni vilitayarishwa na kurushwa hewani kupitia ZBC kwa lengo la kuwaelimisha watumiaji na wamiliki wa kazi za hakimiliki na jamii kwa jumla juu ya haki za wabunifu na wasanii. Tunaipongeza kwa dhati *ZBC* (Televisheni na Redio) kwa kazi nzuri wanayofanya.

TAASISI ZINAZOJITEGEMEA

Mhe. Spika**,** Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inazo taasisi tisa zenye mafungu yanayojitegemea. Kila Fungu lina programu mbili. Programu ya kwanza ni ile inayohusu utekelezaji wa Kazi za Msingi *(Core function)* za taasisi na programu ya pili inahusu utawala na uendeshaji wa ofisi. Fedha zilizomo katika programu hizi zinasimamiwa na Wakuu wa Taasisi husika.

G02: Mahkama

Programu: Upatikanaji wa haki na Usimamizi wa shughuli za Utawala wa Mahkama

Mhe. Naibu Spika, programu ya Kuimarisha upatikanaji wa haki ina lengo la kusimamia utoaji na upatikanaji wa haki kwa kusikiliza na kutolea maamuzi kesi za madai na jinai katika ngazi mbalimbali za Mahkama.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 jumla ya mashauri mapya 172 yamepokelewa na Mahkama Kuu na kufikisha idadi ya mashauri 353 yakijumuishwa mashauri 181 yaliyokuwepo awali, ambapo mashauri 16 yametolewa uamuzi. Aidha, Divisheni ya Mahkama ya Kazi imepokea mashauri mapya 12 na kufikisha mashauri 23 yakijumuishwa na mashauri 11

yaliyosajiliwa kabla. Tayari Mahkama hiyo imetoa uamuzi kwa mashauri manne.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Mahkama za Mkoa, mashauri mapya 159 yamepokelewa na kufikisha mashauri 380 yakijumuishwa na mashauri 221 yaliyosajiliwa kabla. Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 26. Vile vile, Mahkama za Wilaya zilipokea mashauri mapya 2,112 na kufikisha mashauri 4,616 yakijumuishwa na mashauri 2,504 yaliyosajiliwa kabla. Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 1,608. Vile vile, Mahkama za Mwanzo zilipokea mashauri mapya 6,282 na kufikisha mashauri 9,065 yakijumuishwa na mashauri 2,783 yaliyosajiliwa kabla. Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 5,795.

Mhe. Naibu Spika, Mahkama ya Kadhi ya Rufaa imepokea mashauri mapya 36 na kufikisha mashauri 70 yakijumuishwa mashauri 34 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 15 kati ya hayo yametolewa uamuzi. Mahkama za Kadhi za Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,057 na kufikisha mashauri 2,090 yakijumuishwa mashauri 365 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 365 yametolewa uamuzi.

Mhe. Naibu Spika, Mahkama ya Rufaa ya Tanzania ilipokea mashauri 20 na kufikisha mashauri 26 yakijumuishwa mashauri sita yaliyosajiliwa kabla. Hakuna uamuzi wa mashauri uliotolewa. Kwa upande wa Mahkama ya Watoto ilipokea mashauri mapya 12 na kufikisha mashauri 40 yakijumuishwa mashauri 28 yaliyosajiliwa kabla. Mahkama hiyo imetoa uamuzi wa mashauri 6.

Mhe. Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Mahkama imepokea na kusajili jumla ya mashauri 9,863 kutoka Mahkama zote kwa kipindi cha Julai-Machi, 2015/2016 ambapo idadi ya mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 7,853 (*Viambatanisho nam. 5a&b vinahusika).*

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kugharamia uendeshaji wa ofisi chini ya programu ya utawala na uendeshaji, jengo la Mahkama Chake Chake Pemba limefanyiwa matengenezo makubwa, kazi ambayo imekamilika. Vile vile, Jengo jipya la Mahkama ya Watoto limejengwa Mahonda Mkoa Kaskazini Unguja, kupitia Mkakati wa Mabadiliko ya Mfumo wa Sheria kwa Watoto.

Mhe. Naibu Spika, Mahkama imeanzisha mfumo wa kusimamia kesi kwa njia ya kielektroniki *(Computerized Case Management System)*. Mfumo huu umeanza kwa majaribio katika Mahkama Kuu Vuga ambapo utaendelea kwenye Mahkama nyengine kadiri utendaji wake utakavyoruhusu. Lengo kuu

la mfumo huu ni kuweka utaratibu bora zaidi wa kumbukumbu na taarifa na kuongeza kasi ya uendeshaji wa kesi katika Mahkama.

G03 – Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Programu: Mageuzi ya utoaji wa huduma za sheria na Usimamizi wa shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kuishauri Serikali kwa mambo ya kisheria ikiwemo kuandaa mikataba ya kitaifa na kimataifa, kutayarisha miswada ya sheria, kusimamia mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali na kuandaa hati na nyaraka za kisheria. Kiambatanisho nam. 6 kinaonesha Miswada iliyoshughulikiwa kwa mwaka 2015/16.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia programu hii, Rasimu za miswada ya sheria nne zimetayarishwa kwa lengo la kupata sheria mpya ambazo baadhi yake zimepitwa na wakati na nyengine hazikuwepo hapo kabla. Aidha, Kanuni za sheria, matangazo ya kisheria *(Legal Notice)* zimeandaliwa na kuchapishwa.

Mhe. Naibu Spika, Mikataba 50 ya Wizara na Taasisi za Serikali na Hati za Maelewano (*MOU*) yaliyoingiwa na Serikali zimesimamiwa. Jumla ya kesi 60 za madai zilizofunguliwa dhidi ya Serikali zimesikilizwa. Magazeti Rasmi ya Serikali kuanzia mwaka 1910 hadi mwaka 1955 yamekusanywa na kuwekwa pamoja. Lengo ni kukusanya magazeti rasmi hadi kufikia mwaka 1963.

Mhe. Naibu Spika**,** katika kutekeleza masharti ya kifungu cha 11 cha Sheria Namba 6 ya 2013 ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Maafisa Sheria 15 kutoka Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wameteuliwa kuwa Mawakili wa Serikali ili kushirikiana na Wanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutekeleza majukumu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, Mawakili wa Serikali, Mahakimu, Maafisa Sheria wa taasisi mbalimbali za Serikali na watendaji kutoka taasisi za fedha nchini wamepatiwa mafunzo kuhusiana na utakasishaji wa fedha haramu. Aidha, Kupitia Programu ya Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria, Wanasheria wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Maafisa Sheria kutoka Wizara na taasisi za Serikali wamepatiwa mafunzo yanayohusiana na masuala ya mikataba na utatuzi wa migogoro.

G04 – Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Programu: Uendeshaji na usimamizi wa kesi za jinai kiraia na Kukuza mipango na uendeshaji wa Ofisi.

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kusimamia mashtaka yote ya jinai Zanzibar isipokuwa Mahkama za Kijeshi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia programu hii, Kesi za jinai 8,274 zilifunguliwa katika mahkama za Unguja na Pemba, ambapo kesi 7,409 zimeshatolewa uamuzi na kesi 865 zinaendelea.

Mhe. Naibu Spika, Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti *(Zanzibar Law Resource Centre)* kimeendelea kutoa mafunzo ya Uandishi wa Sheria *(Legal Drafting),* Cheti na Stashahada ya Sheria kwa wanasheria na watendaji wengine wa Serikali na taasisi binafsi. Aidha, Wanasheria wanne wapya ambao watafanya kazi za uendeshaji mashtaka katika mahkama za Unguja na Pemba wameajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu ya Utawala na Uendeshaji, ujenzi wa nyumba mbili za Waendesha Mashtaka zilizopo Makunduchi, Wilaya ya Kusini na Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini A Unguja, uko katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, Ofisi ndogo ya uendeshaji wa mashtaka imeanzishwa katika Wilaya ya Kati (Mwera).

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Programu: Mapitio ya Sheria za Zanzibar na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kufanya mapitio ya sheria zenye mapungufu katika utekelezaji wake kiuchumi, kijamii na kisiasa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizo.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, programu hii imekamilisha Mapitio ya sheria nne ambazo ni; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 7/2004, Sheria ya Usajili wa Ndoa na Talaka za (Waislam) sura ya 91/1936, Sheria ya Ufungaji na Usajili wa Ndoa (za Wasiokuwa Waislamu) sura ya 92/1915 na Sheria ya Usuluhishi sura ya 27/1931.

G06: Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Programu: Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma na Utawala na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kufanya ukaguzi wa mazingira, ukaguzi wa kompyuta, ukaguzi wa maeneo hatarishi *(Risk based Audit)*, ukaguzi yakinifu *(Value for Money)* na mafunzo ya muongozo wa ukaguzi *(Regulatory Audit Manual).*

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, kupitia programu hii Majalada 1'689 ya wastaafu pamoja na fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini yamekaguliwa, ambapo majalada 854 kwa ajili ya malipo ya Wizara ya Fedha, majalada 816 kwa ajili ya malipo ya Mfuko wa Hifadhi ya jamii (*ZSSF*) na majalada 19 kwa ajili ya fidia.

Mhe. Naibu Spika, Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2014/2015 katika Taasisi za Serikali umefanyika, ambapo Wizara zote za Serikali, Mashirika,Taasisi pamoja na miradi ya maendeleo inayogharamiwa na Washirika wa Maendeleo ilikaguliwa. Aidha, Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/14 zimewasilishwa katika Baraza la Wawakilishi na kutolewa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha uwezo wa Ofisi kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi, jumla ya wafanyakazi 50 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika masuala ya ukaguzi yakinifu, tathmini ya kutambua maeneo hatarishi ya ukaguzi na ukaguzi unaoendana na viwango vya ukaguzi vya kimataifa. Aidha, muongozo maalum wa ukaguzi *(Regularity Audit Manual)* umepitiwa na kurekebishwa.

G07: Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Programu: kupunguza vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi na utawala na uendeshaji

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya Rushwa, Kuchukua hatua za Kinga dhidi ya Rushwa na kufanya uchunguzi wa vitendo vya Rushwa.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia program hii, Tuhuma 51 za makosa yakiwemo ya kuomba na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya ofisi,

matumizi mabaya ya mali za umma, kukwepa kulipa kodi, rushwa katika zabuni, na rushwa katika uchaguzi zimechunguzwa. Kati ya tuhuma hizo, 29 uchunguzi wake umekamilika na majalada manne yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, hatua za udhibiti wa kuziba mianya ya rushwa katika maeneo ya utowaji wa huduma zimechukuliwa kwa kushirikiana na taasisi za Serikali zikiwemo Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi na Hoteli ya Bwawani.

Mhe. Naibu Spika, elimu ya kuhamasisha kukataa kutoa na kupokea rushwa imetolewa kwa jamii na katika Taasisi za Serikali kupitia vipindi 12 vya redio. Vile vile, semina 14 za kuitambulisha Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, athari za rushwa na namna ya kushiriki katika kuzuia rushwa zimefanyika.

G08: Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Programu: Usimamizi wa Mifumo ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma na Utawala na Uendeshaji

Mhe. Naibu Spika**,** programu hii ina lengo la kuimarisha mifumo ya uendeshaji na Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 Programu hii, imetoa mapendekezo ya Miundo ya Taasisi kutoka Taasisi nne za Umma na Muundo wa Mshahara kutoka taasisi moja ambao ulifanyiwa kazi. Aidha, ukaguzi maalum wa kuangalia masuala ya mishahara na maposho katika Wakala Tendaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar 34 umefanyika na ziara za kuangalia utekelezaji wa masuala ya kiutumishi katika wizara sita zimefanyika. Aidha, Rufaa mbili na malalamiko saba yamepokelewa, kufanyiwa uchambuzi na kutolewa uamuzi (angalia viambatanisho nam 12 & 13).

Mhe. Naibu Spika, vikao 18 vya kawaida na vitatu vya dharura juu ya masuala ya Utumishi wa Umma vilifanyika kujadili na kutoa uamuzi. Aidha, ziara sita za kufuatilia na kuangalia utekelezaji wa majukumu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma, ikiwemo Maadili na Miiko ya Kiutumishi, Uajiri na Mafunzo zilifanyika. Aidha, watumishi wawili wamehudhuria Mkutano wa Jumuia ya Uongozi na Utawala wa Umma Afrika (*AAPAM*), nchini Zambia.

G09: Tume ya Utumishi Serikalini

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini ambayo ina lengo la kusimamia uajiri na kuimarisha maadili ya haki za watumishi serikalini.

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kusimamia uajiri na kuimarisha maadili na haki za Watumishi Serikalini.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016 kupitia programu hii, nafasi za ajira 225 zilitangazwa, kufanyiwa usaili, na kutolewa kibali cha ajira kwa Unguja na Pemba. Aidha, malalamiko matatu yaliwasilishwa na kufanyiwa kazi ambapo malalmiko mawili yametolewa maamuzi na lalamiko moja linaendelea kufanyiwa kazi *(angalia Kiambatanisho nam. 10).*

Mhe. Naibu Spika, watumishi 14 wameongezwa muda wa utumishi na ajira za mkataba kwa watumishi 23 zimeidhinishwa. Watumishi wanne wamepewa ruhusa ya likizo bila ya malipo, 40 wamestaafu kazi kwa hiari, watatu wamestaafishwa kwa maradhi na 316 wamestaafishwa kazi kwa kufikia umri wa lazima.

Mhe. Naibu Spika, watumishi 220 wamethibitishwa kazi, 21 wamebadilishwa kada na wanne wameacha kazi kwa hiari. Aidha, makosa ya kinidhamu kwa watumishi watatu yamewasilishwa na kujadiliwa, kati ya hayo mawili yameshatolewa maamuzi ambapo watumishi wawili wamefukuzwa kazi na shauri moja linaendelea kufanyiwa kazi (*angalia Kiambatanisho nam. 9).*

MUELEKEO WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 sasa naomba kutoa ufafanuzi wa muelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Vipaumbele vya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

Kuimarisha mfumo wa uingizaji wa taarifa za watumishi uliounganishwa na mfumo wa malipo (*Data base system*);

1. Kuimarisha ufuatwaji wa misingi ya utawala bora katika utendaji wa shughuli za Serikali;
2. Kuimarisha mfumo wa uhuishaji wa nyaraka na kumbukumbu za taifa;
3. Kuimarisha huduma za Serikali Mtandao, ikiwemo kuanzisha Tovuti ya Serikali;
4. Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa kesi (*case management system*); na
5. Kuimarisha miundombinu ya Mahkama, ikiwa pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la Mahkama Kuu, Mwanakwerekwe na Mahkama ya Mkoa Mfenesini.

Mhe. Naibu Spika, vipaumbele hivi vinaendana na malengo ya Mipango Mikuu ya Taifa (Dira 2020 na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar), pamoja na Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu na Sera za Kisekta. Pia vipaumbele vimezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa Mwaka 2015 – 2020; Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi 2010 – 2020; na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi tarehe 5 Aprili, 2016.

Malengo Makuu ya Ofisi kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi hii imejipangia malengo makuu yafuatayo:

1. Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;
2. Kuimarisha miundombinu katika vyombo vya sheria na utumishi wa umma;
3. Kuweka miundo ya taasisi na kusimamia mipango endelevu ya upatikanaji wa rasilimaliwatu wenye sifa;
4. Kuimarisha utendaji kazi katika utumishi wa umma;
5. Kuimarisha uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za Taifa;
6. Kuimarisha mawasiliano ya Serikali; na
7. Kuimarisha maadili na misingi ya utawala bora katika utendaji wa shughuli za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jumla ya Programu 21 na Programu Ndogo 26. Programu tano na Programu ndogo 10 zinatekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu

Mkuu na Programu 16 zinatekelezwa katika Taasisi Zinazojitegemea. Kati ya Programu hizo 16, nane ni za utekelezaji kazi za msingi za taasisi na nane zinahusu uendeshaji wa ofisi hizo. Melezo ya programu hizo ni kama ifuatavyo:-

G01 Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kuchukua fursa hii kutoa maelezo ya Muelekeo wa programu zinazosimamiwa na Ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Programu: Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Mifumo na Miundo ya Taasisi

Programu ndogo: Maendeleo ya Rasilimali Watu

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kufanya mapitio ya Ikama (*norminal roll*) na kuidhinisha nafasi za kazi, kuthibitisha taarifa za watumishi waliofikia umri wa kustaafu na kuratibu mafunzo yanayotolewa na washirika wa maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha TZS. 234,475,200.

Programu ndogo: Maendeleo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kukamilisha kazi ya mapitio ya majukumu ya watumishi na kuwapanga watumishi katika madaraja yao kwa mujibu wa muundo mpya wa utumishi, kusimamia utekelezaji wa mkataba wa utoaji wa huduma na kusimamia utekelezaji wa muongozo wa upimaji kazi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 275,246,000.
Programu: Uimarishaji wa Kumbumbu na Mawasiliano ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Programu ndogo: Usimamizi na Uendeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuendelea na uratibu wa mradi wa "*e-government*" awamu ya pili (*e-Tax na e-health*) kuandaa Tovuti kuu ya serikali, kukamilisha kazi ya kuziunganisha Taasisi za Serikali katika kituo kikuu cha taarifa "*Data Center*" na kutoa anuani za barua pepe kwa watumishi wengine wa umma.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 526,033,800.

Programu ndogo: Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuzihuisha nyaraka chakavu na kuziingiza katika mfumo wa kielektroniki, kufanya tathmini ya kumbukumbu zinazozalishwa na taasisi za Serikali na kufanya ukaguzi wa nyaraka na kumbukumbu katika Wizara na taasisi za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 372,300,000.

Programu: Utawala Bora na Haki za Binaadamu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuandaa ripoti ya mwaka ya Utawala bora, kuendelea kuingiza (*mainstream*) masuala ya Utawala Bora katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuzifanyia kazi changamoto zilizojitokeza katika ripoti ya Utawala Bora, kuelimisha wananchi juu ya dhana nzima ya Utawala Bora na kushajihisha mashirika ya kibiashara na Wawekezaji kuheshimu na kuchangia katika majukumu yao ya kijamii (*Corporate Social Responsibility*).

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 225,644,600
Programu: Usimamizi wa Masuala ya Dini

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kufanya mapitio ya sheria ya Mufti, kusajili na kutembelea Misikiti 95 na Madrasa 195, kuendesha mikutano miwili ya Baraza la Ulamaa na vikao sita vya Kamati ya kuandama kwa Mwezi na kukuza mahusiano kwa jumuiya za kidini za kitaifa na kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 482,112,000

Programu: Mipango na Utawala

Programu ndogo: Uongozi na Utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuendelea na usimamizi na kuwaendeleza watumishi kwa kuwapatia fursa za kujenga uwezo wao kitaalamu na kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa ofisi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 1,581,592,400.

Programu ndogo: Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga Kuandaa Mipango ya Bajeti na mapitio ya utekelezaji wake, kuandaa Mpango mkakati wa Wizara wa miaka mitano na Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini, Kukamilisha Sera ya Malipo ya Watumishi wa Umma, Sera ya Msaada wa Kisheria Zanzibar na Sera ya Usimamizi wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Aidha, kuchunguza uwezo wa rasilimali watu uliopo katika Utumishi wa Umma na kuandaa mikakati ya utekelezaji wa mapendekezo ya tafiti mbali mbali zilizofanywa katika sekta za Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 368,029,600

Programu Ndogo: Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuendelea na kuratibu shughuli za Wizara kwa Pemba, kusimamia shughuli za uendeshaji na utawala na kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha TZS. 696,846,400.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Fungu G01 lenye programu tano zilizoelezwa hapo juu limepangiwa kutumia jumla ya TZS. 7,891,395,000, zikiwemo TZS 4,882,300,000 za matumizi ya kawaida, TZS 1,268,900,000 za Ruzuku na TZS 1,740,195,000 za Maendeleo. Fedha hizi zitasimamiwa na Katibu Mkuu. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika Viambatanisho vilivyomo katika Hotuba yangu hii na Kitabu cha Bajeti ya Serikali.

G02: Mahkama

Programu: Upatikanaji wa Haki na usimamizi wa shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kusikiliza na kutoa uamuzi wa kesi za madai na jinai katika ngazi mbalimbali za Mahkama, kuimarisha mfumo wa kisasa wa uendeshaji wa kesi kwa njia ya kielektroniki na kuanza ujenzi wa Mahkama Kuu, Mwanakwerekwe na Mahkama ya Mkoa Mfenesini.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya TZS. 5,232,400,000 na mapato ya TZS. 301,776,000.

G03: Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Programu: Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria na Usimamizi wa shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake, kuandaa miswada,

kanuni, matangazo ya kisheria na muongozo wa mikataba ya Serikali na kuiwakilisha Serikali mahakamani kwenye kesi za madai.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha TZS. 1,068,600,000.

G04: Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Programu: Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai, Kiraia na Usimamizi wa shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuendesha na kusimamia kesi za jinai na kutoa huduma za uendeshaji wa ofisi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya TZS. 1,704,399,440.

G05: Tume ya Kurekebisha Sheria

Programu: Mapitio ya Sheria za Zanzibar na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kufanya mapitio ya Sheria sita ambazo ni; Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mufti namba 9/2001, Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 99/1919), Sheria ya Urithi wa Ardhi (Sura ya 101/1926), Sheria ya Udanganyifu wa Mazao (Sura ya 109/1934), Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi 15/1986 na Sheria ya Usalama na Afya Kazini namba 8/2005, kutoa elimu kwa Umma juu ya Sheria zinazofanyiwa mapitio na kuimarisha ushirikiano wa ndani ya nchi na kimataifa na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 508,500,000.

G06: Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Programu: Udhibiti wa Rasilimali za Umma

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kukagua hesabu za serikali na Taasisi zake zote kwa kutumia mfumo wa ukaguzi unaozingatia matokeo ya malengo ya bajeti ya mfumo wa programu (*PBB Audit*), kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbalimbali za ukaguzi, kupitia na kurekebisha muongozo wa ukaguzi (*Regulatory Audit Manual*) na kutoa ushauri na taaluma kwa wadau kupitia semina, warsha na makongamano.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 2,244,800,000.

G07: Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Programu: Kupunguza vitendo ya rushwa na uhujumu wa uchumi na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuendelea kutoa elimu kwa Umma juu ya vitendo vya rushwa, kuwajengea uwezo watumishi wa Mamlaka ya Rushwa katika kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi, kuendelea kufanya uchunguzi wa vitendo vya Rushwa, na kuazimisha Siku ya Rushwa duniani.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 936,300,000.

G08: Kamisheni ya Utumishi Wa Umma

Programu: Usimamizi wa mifumo ya Rasilimali watu katika utumishi wa umma na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kushughulikia Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi, Miundo ya Utumishi na Miundo ya Mishahara itakayowasilishwa, Kuaandaa na kusambaza Nakala 1000 za Muongozo wa Ukaguzi wa Afya na Usalama Kazini, nakala 600 za Muongozo wa masuala ya Ajira katika Utumishi, pamoja na kutoa uelewa wa

nyenzo hizo kwa Maafisa Utumishi, Unguja na Pemba, kufanya Uchunguzi na Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Rasilimali Watu katika Taasisi za Umma, pamoja na kupokea na kushughulikia Malalamiko na Rufaa zitazowasilishwa Kamisheni na Kuanzisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma (*Monitoring and Evaluation Framework*).

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 809,200,000.

G09: Tume ya Utumishi Serikalini

Programu: Usimamizi wa Uajiri, Haki na nidhamu kwa watumishi Serikali na usimamizi wa shughuli za utawala

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kuajiri Watumishi Serikalini, Kuthibitisha watumishi, kupandisha daraja na kubadilisha kada. Vile vile, kuidhinisha nyongeza za muda wa utumishi, ajira za mikataba na kuidhinisha likizo bila malipo na kustaafisha kazi, kusikiliza rufaa na kutoa maamuzi ya malalamiko ya watumishi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 417,900,000.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, katika juhudi za Serikali za kuimarisha Utawala Bora, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, ametekeleza ahadi yake aliyoitoa ya kuunda Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kumteua Ndugu Assaa A. Rashid, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, kuwa Mwenyekiti wa Tume hiyo. Hatua zinazoendelea sasa ni kuijenga Tume hiyo kwa kuipatia Watumishi waliobobea kwa mujibu wa mahitaji, vitendea kazi na samani za ofisi.

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni; kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Rasilimali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma, kupokea malalamiko na tuhuma, kufanya uchunguzi kuhusu uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Viongozi wote wa Umma na Viongozi wa kisiasa wanaotajwa ndani ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam 4 ya mwaka 2015, kuanzia mwaka huu wa fedha watawajibika kuwasilisha mbele ya Tume, Fomu za Tamko la Mali na Madeni yao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya Tume kukamilisha maandalizi yanayohitajika, utaratibu wa ujazaji na uwasilishaji wa Fomu za Matamko utaelezwa. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Viongozi wote wa Kisiasa, tukiwemo sisi Wawakilishi wa Wananchi, na Viongozi wote wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali wanawajibika kujaza fomu za tamko la mali na madeni yao. Serikali inawaomba viongozi na wananchi kwa ujumla kuipa ushirikiano Tume hii ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kulithibitishia Baraza lako Tukufu kwamba Tume ya Maadili ya Viongozi inaahidi kutekeleza Sheria ya Maadili ya Viongozi No. 4 ya mwaka 2015 na Kanuni zake pamoja na maelekezo ya Baraza lako Tukufu kwa kuongeza kasi ya utekelezaji katika uendeshaji wa shughuli za Serikali na kuongeza uwazi kwa kusimamia sheria, kanuni, miongozo na taratibu za uwajibikaji wa viongozi ili wawajibike kwa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Tume imepanga kuimarisha uwezo wa Ofisi kwa kuipatia nyenzo za kufanyia kazi, kutayarisha Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Maadili ya Viongozi, kutayarisha Mfumo wa usajili wa malalamiko kwa njia ya kieloktroniki ili kuwezesha utendaji wa kazi wa Tume, kupokea na kusajili ‘Tamko la Rasilimali na Madeni’ kutoka kwa Viongozi wa Umma na kuyafanyia kazi, kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi na kuchunguza tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadiili ya Viongozi wa Umma. Aidha, Tume itatoa elimu kwa umma, Viongozi na wahusika mbalimbali kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

Mhe. Naibu Spika, ili Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/17, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 120,000,000.

TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamisheni imepanga kuendesha tirka 1,150 zenye thamani ya TZS 8,000,000,000, kukaguwa nyumba 301, kukusanya kodi ya TZS 682,824,492 katika nyumba za Wakfu, TZS 477,812,160 katika nyumba za Amana na kuzifanyia matengenezo nyumba 30, kukusanya Zakka TZS 12,000,000, Sadaka na Misaada ya kheri yenye thamani TZS 700,000,000 na kuigawa kwa wanaostahiki, kusimamia Sala na Baraza la Idd kitaifa na kuratibu shughuli za Hijja.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha ruzuku ya TZS 555,207,000.

Chuo cha Utawala wa Umma

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Chuo kimepanga Kuimarisha mafunzo ya kujenga uwezo kwa watumishi wa Umma kutoka katika Taasisi za Serikali, Mashirika na Watu binafsi ikiwemo mafunzo elekezi ya awali kwa Watumishi wapya, kuendesha mafunzo ya muda mrefu kwa Watumishi wa Umma na wahusika wengine katika fani mbali mbali katika ngazi ya msingi, Cheti, Stashahada na Shahada ya kwanza.

Mhe. Naibu Spika, ili kukiwezesha Chuo cha Utawala wa Umma kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha ruzuku ya TZS. 538,000,000.

Afisi ya Hakimiliki

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Hakimiliki imepanga Kusajili kazi 1,576 za Hakimiliki na kufuatilia, kukusanya na kugawa mirabaha yenye thamani ya TZS. 65,000,000.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha Afisi ya Hakimiliki kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha ruzuku ya TZS. 175,693,000.

SHUKURANI

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Naomba pia niwashukuru kwa dhati wahusika na washirika mbali mbali wa maendeleo kwa ushirikiano mzuri walioutoa kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake.

Miongoni mwao ni: *UNDP*, Jumuiya ya Ulaya (*EU), UNICEF, UNFPA*, Shirika la Kimataifa la Mali za Ubunifu (*WIPO*), Jumuiya ya Uongozi na Utawala wa Umma Africa (*AAPAM*), Benki ya Dunia, African Muslim Agency, Benki ya Maendeleo ya Kiislam (*IDB*), na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Tunawashukuru pia Save the Children, Wizara za Wakfu za Oman na Qatar. Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inazishukuru nchi ya China, India, Korea, Japan, Indonesia, Saudi Arabia, Oman, Uturuki na Egypt.

Mhe. Naibu Spika, wizara inatoa shukrani kwa Vyombo vya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora vya Jamhuri ya Muungano. Vile vile, tunatoa shukrani kwa Chama cha Wanasheria Zanzibar (*ZLS*), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (*ZLSC*), na Chama cha Wanasheria Wanawake (*ZAFELA*); Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji, Jumuiya na Taasisi mbali mbali za kidini; wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Masheha na wananchi wote kwa jumla. Navishukuru sana na vyombo vyetu vya habari kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutoa elimu na kutangaza matukio mbali mbali yaliyohusu shughuli za ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla naomba niwashukuru wote waliosaidia Ofisi ya Rais Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi, pia nawashukuru watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia naomba kuwambia washirika wetu kwamba Wizara itaendelea kuithamini sana michango yao kwa hali na mali, pamoja na ushirikiano wanaotupa kila tulipokuwa tunahitajia ninachoweza kusema kwao ni ahsanteni na tunathamini sana na kuwashukuruni wote, kwa niaba ya Ofisi ya Rais Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma pamoja na Utawala Bora na Serikali kwa ujumla tunaomba mzipokee shukurani zetu ahsanteni sana na mungu awabariki.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwakumbusha kuwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayo dhima ya

kuhakikisha kuwa masuala yanayohusu ufikishwaji wa huduma kwa wananchi pamoja na upatikanaji wa haki zao kwa wakati yanasimamiwa ipasavyo, utekelezaji wa mikakati ya mabadiliko ya utumishi wa umma na mikakati ya mabadiliko katika sekta ya Sheria unalenga kuongeza ufanisi katika kufikisha malengo ya Mkuza dira 2020 pamoja na malengo ya maendeleo endelevu duniani.

Mhe. Naibu Spika, naomba Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimae waidhinishe Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Boara jumla ya Shs. 20,813,495,000/= kwa matumizi ya mwaka wa fedha 2016/2017 kati ya fedha hizo Shs. 19,073, 300,000/= Kwa Matumizi ya Kawaida na Shs. 1,740,195,000/= kwa kazi za Maendeleo. Naomba pia Baraza lako liikubalie Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ichangie Shs. 501,144,000,000/= kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (Kiambatanisho nam 2 na 3)

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis (Makamu Mwenyekiti Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika. awali ya yote hayo napenda kutumia fursa hii adhim kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma, kwa kutuwezesha kuwa na afya njema, pamoja na hekma na busara katika kutekeleza majukumu yetu tuliyopangiwa ya kuitumikia jamii ya Wazanzibari. Pia, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa uwezo wa kuchangia na kutoa maoni ya Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha, 2016/2017.

Mhe. Spika, natumia nafasi hii pia kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, na Katibu Mkuu wake ndugu Asha Ali Abdulla pamoja na watendaji wengine wa Ofisi yake kwa kushirikiana nasi bega kwa bega katika kuipitia Bajeti ya Wizara hii.

Mhe. Spika, sina budi kukiri mbele yako kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara kubwa zilizo katika mstari wa mbele kutekeleza kwa kiasi kikubwa yale yalioahidiwa katika Bajeti iliyopita na ndio wizara iliyobeba taasisi muhimu za nchi, hivyo si vyema kutowapongeza kwa juhudi zao hizo.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awaongezee uwezo na hekma katika kutekeleza yale waliyojipangia kuyatekeleza katika Bajeti hii ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (*UWT*) kwa kunichagua na kuwa Mwakilishi wao; lakini pia, nikishukuru chama changu cha *CCM* kwa kuniteua katika Nafasi za Wanawake kwa kuwakilisha Watu wenye ulemavu. Nawaahidi kuwa kazi walionipa nitaitekeleza kwa umakini na ujasiri wa hali ya juu.

Mhe. Spika, Bajeti ya serikali ni waraka muhimu katika mustakbali wa Taifa lolote Duniani, na ni nyenzo kuu inayotarajiwa kuakisi utekelezaji wa mipango ya Kitaifa na ambayo inalenga kuliendeleza Taifa katika maendeleo endelevu kwa mujibu wa shabaha na matarajio yaliyowekwa katika Mipango ya Nchi mahsusi.

Mhe. Spika, Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni chombo cha utekelezaji wa Mpango mpya wa Maendeleo wa mwaka 2016-2020, ambao ni mrithi wa Mpango wa zamani wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (*MKUZA II*), ambao umemaliza muda wake 2015.

Aidha, ni chombo cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya mwaka 2015-2020 na Dira ya Maendeleo ya 2020 na Maendeleo endelevu ya Dunia. Hivyo, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa Bajeti inayopangwa inakwenda sambamba na mipango hiyo ya Kitaifa.

Mhe. Spika, kwa upande wa Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala imeundwa na Wajumbe wenye uwezo na umahiri mkubwa wa kuchambua na kuelewa majukumu waliyopewa, hivyo imeweza kutumia nafasi hiyo kutoa ushauri wao juu ya kutafuta ufanisi na utekelezaji wa Bajeti hii ambayo imelenga kuboresha mahitaji ya msingi ya Wananchi zikiwemo huduma muhimu za kijamii.

Mhe. Spika**,** Wajumbe waliounda Kamati hii ni kama wafuatao:-

i. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
ii. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Makamo Mwenyekiti
iii. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
iv. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
v. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Mjumbe
vi. Mhe.Shamata Shaame Khamis - Mjumbe

vii.	Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf	-	Mjumbe
viii.	Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Mjumbe
ix.	Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu, na
x.	Ndg. Ali Alawy Ali	-	Katibu.

Mhe. Spika**,** Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kiungo muhimu cha utendaji katika Serikali ikiwa na muundo wa Taasisi 14 zinazojitegemea na Idara 09 zilizochini ya Wizara hii. Kupitia mfumo wa utekelezaji wa Bajeti wa *PBB (Program Based Budget*) Wizara hii imekua na program mbali mbali ambazo zimeainishwa kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS – KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Spika, Kwa kawaida Katiba inakuwepo kwa matakwa ya watu na kwa madhumuni ya kujenga jamii au nchi iliyoimara ili kuhakikisha kwamba nchi hiyo au jamii hiyo inatawaliwa kwa misingi ya serikali yenye kulinda na kuheshimu demokrasia. Misingi ya demokrasia ya ukweli ndiyo inayoleta utekelezaji mzuri wa harakati za kimaendeleo na kusimamia majukumu ya kila taasisi na kila raia. Aidha, sheria hutungwa kwa kusimamia haki na wajibu wa kila mmoja miongoni mwa jamii na kuhakikisha kuwa haki inapatikana na kulindwa kwa misingi ya kidemokrasia.

Mhe. Spika, Kamati yetu imechunguza kwa kina na kuona kwamba makadirio ya matumizi yaliopangwa katika Idara hii, kuna haja ya Serikali kuwapatia Bajeti hiyo ili kuweza kukamilisha malengo yao na kufikia hatua ya maendeleo endelevu kama ilivyo kadiriwa katika dira ya maendeleo ya 2020.

MAHKAMA

Mhe. Spika, Mahkama ni mhimili mmoja wapo wa Nchi ambao unategemewa katika kusimamia Sheria na Haki za Wananchi wa Zanzibar. Katika kutekeleza jukumu la upatikanaji wa Haki na kuimarisha Utawala wa Sheria. Kamati yetu inaipongeza Mahkama kwa kuanzisha mfumo mpya wa kielektroniki wa kusimamia kesi *(Computerised Case Management System)* kwa lengo la kuweka utaratibu bora wa kumbukumbu na taarifa ambao utaongeza kasi ya uendeshaji wa kesi katika Mahkama zetu. Mfumo huu kwa sasa umeshaanza kufanya kazi katika Mahkama kuu Vuga kwa majaribio ya awali.

Aidha, Kamati yetu inashauri kwamba Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Mahkama watafute njia mbadala ya kuweka kipimo cha kibaiolojia cha DNA katika kusaidia kupatikana kwa Haki dhidi ya vitendo vya Udhalilishaji.

Mhe. Spika, aidha, suala la mrundikizo wa kesi Mahkamani umekuwa mkubwa katika Mahkama zetu za Zanzibar na kusababisha kesi nyingi kupitwa na wakati, na hivyo kupelekea kutosikilizwa kwa wakati unaofaa. Kamati yetu inaomba Idara ya Mahkama kuhakikisha kuwa kesi zilizopo Mahkani katika Mahkama zote za Unguja na Pemba zisikilizwe kwa haraka ili kuacha kucheleweshwa kwa kesi hizo na hatimaye kupoteza Ushahidi au wahusika wa kesi hizo kuacha kuzifuatilia kabisa.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Mhe: Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto (Mhe. Maudline Cyrus Castico) wakati akijibu suali lililoulizwa kwa Wizara yake kuhusu "***Kesi za Udhalilishaji***" siku ya tarehe 26-05-2016, alisema:

"..takwimu kutoka Mahkamani zinaonyesha kuwa mnamo mwaka 2014, jumla ya kesi 96 zilifunguliwa zinazohusu ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, kati ya hizo kesi 5 zilitolewa uamuzi na kesi 24 zimetupiliwa mbali, na kesi zilizobali zilikuwa zinaendelea.

Pia, kuanzia Januari hadi October 2015, jumla ya kesi 49 zilifunguliwa na kati ya hizo ni kesi 2 tu zilipatiwa hukumu na 47 zilikua zinaendelea. Katika Mahkama ya Watoto, jumla ya kesi 64 zilifunguliwa kwa mwaka 2015; kati ya hizo kesi 55 zilitolewa uamuzi na kesi 9 zinaendelea".

Mhe. Spika, hali hii inasikitisha sana na inavunja moyo kuona kuwa ni kesi chache zinazopatiwa hukumu na hili sio jambo zuri katika upatikanaji wa Haki.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa suala la Sheria limepata ubora na ni haki na wajibu wa kila Binadamu kupatiwa, Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar iliandaa miswaada ya kusimamia na kuiwakilisha Serikali Mahkamani, kushiriki na kutoa ufafanuzi wa sheria hizo kwenye kamati za Baraza la Wawakilishi, pamoja na majukumu mengine ya kisheria na kiutawala.

Mhe. Spika**,** Kamati yetu inaliomba Baraza lako kupitisha kwa Program na fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika Taasisi hii.

OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Mhe. Spika, Dira ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni utawala wa haki ya jinai uliowazi, unaodumisha amani, utulivu na maendeleo ya Taifa. Lengo kuu ni kutoa huduma ya Mashtaka kwa niaba ya Watu na Serikali ya Zanzibar ambayo inajitegemea, iliyowazi, yenye nguvu, inayofanya kazi na yenye mafanikio.

Mhe. Spika, Kamati yetu imefanikiwa pia kupitia Bajeti ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kujadili propgram mbali mbali zilizopangwa kutumika kwa mwaka huu wa fedha pamoja kuona umuhimu wake katika kufikia hatua ya maendeleo endelevu.

Aidha, katika kufanikisha utaratibu wa kuendesha mashtaka kiraia, Kamati yetu inaishauri Ofisi kuendelea kuweka ofisi zake kila Wilaya ili kuweza kuwafikia Wananchi kiurahisi na kujenga mazoea ya kuzitumia ofisi hizo. Aidha, Kamati inatoa ushauri kwa ofisi hii kujenga ushirikiano wa karibu na jeshi la polisi na Idara ya Mahkama ili haki ipatikane kwa Wananchi wote na kwa wakati.

Mhe. Spika, kupitia kikao chako hiki adhim, Kamati yetu haina budi kupendekeza kupitishwa kwa program hizi na fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo kupitia Bajeti hii.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Mhe. Spika, Kamati imearifiwa kuwa katika mwaka uliotangulia, Tume ya Kurekebisha Sheria imezipitia sheria nne, na nyaraka zake kuzifanyia matayarisho kwa ajili ya kuziwasilisha katika kikao cha Makatibu wakuu. Sheria hizo ni sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, sheria ya Adhabu, sheria ya Mwenendo wa Madai na sheria ya Ushahidi.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine Tume imezifanyia mapitio sheria ya Usajili wa ndoa na Talaka za Waislam (sura ya 91/1936) na sheria za ufungaji na usajili za wasiokua waislam (sura ya 92/1915) na sheria ya usuluhishi (sura ya 27/193). Hatua iliyobaki kwa sasa ni kuziwasilisha kwa Wadau na kujadiliwa.
Mhe. Spika, Kamati yetu imekaa na kujadili kwa umahiri mkubwa kuhusu makadirio na matumizi ya fedha kwa mwaka huu wa 2016/2017 na kuona

kuwa, Tume hii ili iweze kukamilisha malengo na kazi zake, ambazo kwa sasa ni muendelezo wa kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati, hivyo ni vyema kwa Wajumbe wa Baraza lako kupitisha program zote zilizoainishwa pamoja na fungu la fedha lililowekwa katika bajeti hii.

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

Mhe. Spika, katika kuimarisha Utawala bora Zanzibar, Mamlaka ya kuzuia na kupamba na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ni muhimu sana kuwepo na kuwepo kwake imeweza kusaidia utendaji kazi pamoja na kujenga nidhamu kazini. Kamati yetu inapendekeza watendaji wa Taasisi hii waendelee kupatiwa mafunzo ili kujenga uwezo wa Taasisi na ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

Mhe. Spik**a,** Kamati yetu baada ya kukaa na kujadiliana na Idara husika imeona kuwa kiasi cha fedha kilichokadiriwa kinaweza kukidhi mahitaji endapo kitapatikana kwa wakati. Tukumbuke kuwa lengo la Mamlaka ya kuzuia rushwa kwa mwaka huu ni; “kuzuia rushwa kutokea na kukuza uelewa wa wananchi juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi”. Hivyo, Zanzibar bila Rushwa inawezekana.

KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Mhe. Spika, Kamati yetu imeelezwa kuwa katika mwaka wa bajeti wa 2015/2016, Kamisheni ilipokea na kushughulikia Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi kutoka Taasisi nne za Umma na Muundo wa Mshahara kutoka Taasisi moja. Aidha, ukaguzi maalum wa kuangalia masuala ya Mishahara na Maposho katika Wakala Tendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulifanyika.

Mhe. Spika, Kamati yetu inaomba Kamisheni ya Utumishi wa Umma kusimamia taratibu zote zinazotumiwa na Chuo cha Utumishi wa Umma *IPA* (Institute of Public Administration) katika utaratibu wake wa kupiga faini wanafunzi ambao wameshindwa kulipa ada za masomo. Kamati yetu imegundua kwamba utaratibu wa faini unaotumika chuoni hapo haukowazi. Aidha, Kamati inashauri chuo hiki kufuata taratibu zote za malipo kama wanavyofanya vyuo vyengine vya elimu za juu.

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Spika, lengo kuu la Tume ya Utumishi Serikalini ni Kuimarisha Utawala bora katika Utendaji wa Serikali. Aidha, Kamati yetu imekaa na kupitia Bajeti

yake na kuona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kupatikana fedha hizo kwa wakati.

Mhe. Spika, Kamati yetu inapendekeza kwa Tume ya Utumishi Serikalini kuliangalia vyema suala la ajira na kuhakikisha kwamba; Ajira zinapatikana kwa wote na kwa kuzingatia sifa za ajira husika. Aidha, Kamati inashauri kwamba ili kuondoa malalamiko ya watafutaji ajira ni vyema kuwe na uwazi katika utoaji wa ajira, pia sifa ya uzalendo iwe ni sehemu muhimu ya kuzingatiwa katika utoaji wa ajira hizo.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Kamati yetu inachukua nafasi hii kuliomba Baraza lako kufanya juhudi za kuvipitia vifungu vyote vya fedha vilivyoainishwa katika program mbali mbali za Wizara hii na kutoa mapendekezo yao ili kuiboresha na kuijenga bajeti ambayo ni muhimu katika utekelezaji wa shughuli za serikali na kuleta maslahi kwa mujibu wa dira ya maendeleo ya 2020 na ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 na mwishowe naomba waipitishe.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala katika Baraza lako. Sambamba na hili, pia niwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wakati wote wa kuwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa wizara hii inasimamiwa na kamati mbili, kwa hiyo sasa hivi nimwite Mhe. Salma Mussa Bilal ambaye atasoma kwa niaba ya Mwenyekiti maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Salma karibu.

Mhe. Salma Mussa Bilal (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC): Mhe. Naibu Spika, ahsante naomba kutoa hotuba ya maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, mwingi wa rehema ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, shukurani zangu za dhati pia zije kwako kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kutoa maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (*PAC*) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ni Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salma Mussa Bilal (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. Naibu Spika, samahani.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii vile vile, kumshukuru Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, Mhe. Haroun Ali Suleiman, Naibu Waziri wake ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe, Mhe. Khamis Juma Mwalim, Katibu Mkuu Ndugu Asha Ali Abdulla, na watendaji wengine wa wizara hii pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano yao ya dhati kwa kamati wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi hii ya kuchambua na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hii kwa mwaka 2016/ 2017.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nichukue fursa hii kutoa pongezi na shukurani maalum kwa Wajumbe wa Kamati ya *PAC*, kwa kuonesha umahiri na umakini mkubwa wa kuyachunguza na kuyachambua makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hii muhimu licha ya kuwa wengi wao ni wapya katika shughuli za kamati. Pongezi na shukrani hizi pia ziende kwa Makatibu wa Kamati hii kwa ushauri na maelekezo yao ya kitaalamu yaliyowawezesha wajumbe kutekeleza majukumu yao ya kupitia bajeti ya ofisi hii kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu wao kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya *PAC* kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - wenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamu Mwenyekiti.

3.	Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Mjumbe
4.	Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Mjumbe
6.	Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Mjumbe
7.	Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Mjumbe
8.	Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mjumbe
9.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Mjumbe
10.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
11.	Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, kama inavyofahamika kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ipo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu cha 112. Hata hivyo, utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii unaongozwa na Sheria ya Ukaguzi Nam. 11 ya mwaka 2003. Inayohusiana na uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Sheria ya Fedha Nam. 12 ya mwaka 2005, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 9 ya mwaka 2005 pamoja na sheria nyengine za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kuwa uzito wa majukumu ya ofisi hii kikatiba unapaswa uende sambamba na uzito wa bajeti inayopaswa kuingiziwa Ofisi ya Mdhibiti na Serikali ili ofisi hii iendelee kuwa ni chachu ya kujenga uadilifu katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na mali za umma.

Mhe. Naibu Spika, uwajibikaji, uwazi, uyakinifu na ufanisi katika matumizi ya mali na fedha za umma ni msingi muhimu katika serikali yoyote inayofuata misingi ya Sheria na Utawala Bora. Serikali hulazimika kuonesha uaminifu na uadilifu wake kwa walipa kodi kwa kupitia kwa wawakilishi wa wananchi au kwa wananchi wenyewe moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba ya uzinduzi wa Baraza hili la Tisa la Wawakilishi mnamo tarehe 5 Aprili, 2016 ambayo ndio dira ya utekelezaji wa kazi za serikali kwa kipindi hiki, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika ukurasa wa 66 alisema, naomba kunukuu;
"Serikali itahakikisha kuwa ubora wa miradi inayotekelezwa na ununuzi wa vifaa na huduma mbali mbali inazolingana na thamani ya fedha zilizotumika (*Value for Money*). Zipo taarifa kwamba kuna ubabaishaji mkubwa unaofanyika katika ununuzi wa vifaa na nyenzo."

Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kuwa kauli hii inatakiwa ichukuliwe na ofisi hii kwa uzito unaostahili kwa kujipanga vizuri zaidi katika utekelezaji wa kazi

zake ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za serikali pamoja na ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya fedha, ununuzi na uondoshaji wa, mali za umma unaoendelea kufanywa na baadhi ya watendaji wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo matokeo muhimu ya Ripoti za Ukaguzi za Mdhibiti yana mchango mkubwa katika kujenga taifa lenye misingi ya utawala bora. Kwa mtazamo huo taasisi za serikali zinapaswa kuchukua hatua za kutatua kasoro mbali mbali zinazobainishwa katika ripoti hizo. Kwa mnasaba huo viongozi wa taasisi za serikali wana dhima kubwa ya kusimamia vyema utekelezaji wa sheria na kanuni husika na kuhakikisha kuwa fedha na mali za umma zinatunzwa na kutumiwa kwa uadilifu ikiwa ni pamoja na kupambana na rushwa. Sambamba na hilo, ni vyema viongozi wa taasisi wakaachana kabisa na tabia ya kuwaachia watendaji wa serikali kukiuka taratibu kwa kisingizio kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ipo na itachunguza.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa majadiliano na ofisi hii, kamati yetu imebaini kuwa Ofisi ya Mdhibiti inakabiliwa na changamoto kubwa katika eneo la watendaji hususan wakaguzi ambao ndio kioo au msingi wa utendaji wa ofisi hii. Mhe. Naibu Spika, kwa kukadiria Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inahitaji wakaguzi wasiopungua hamsini (50) ambao kwa kiasi kikubwa wataongeza ufanisi wa kazi katika ofisi hii muhimu pindi wataajiriwa ingawa ofisi hii hivi sasa ina wakaguzi wasiopungua 80.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu mara ya mwisho imeajiri watendaji wapya mnamo mwaka 2009. Hivyo, bila shaka wapo watendaji (wakaguzi) ambao wamestaafu, wamefariki pamoja na walioihama ofisi hii kwa sababu moja au nyengine na kupelekea nafasi zao kuwa wazi. Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo na kwa unyeti wa Ofisi ya Mdhibiti, Kamati ya *PAC* inaiomba serikali kuiruhusu ofisi hii kuendelea na mchakato wa uajiri ambao iliuanza ili Ofisi ya Mdhibiti iweze kutekeleza jukumu lake hili kwa umahiri na ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu mbali ya ukaguzi wa kawaida wa kukagua Hesabu za Serikali kwa Mawizara na Mashirika ya SMZ tuliyozoea. Hivi sasa ofisi hii imepanua wigo katika shughuli hii ya ukaguzi na inafanya pia na ukaguzi mwengine kama vile. Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za SMZ, Ukaguzi wa Ukodishwaji wa Ardhi kwa Wawekezaji, Ukaguzi wa Hesabu kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara nakadhalika. Pia ofisi hii hufanya ukaguzi maalum kama itakavyoamriwa na Mhe. Rais wa Zanazibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo hayo, utaungana na Kamati ya *PAC* kuwa Ofisi ya Mdhibiti inahitaji kwa hali na mali kuruhusiwa kuajiri nafasi hizo kwa maendeleo ya ofisi hii na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, tunaelewa kuwa hivi sasa serikali imezuia ajira mpya na badala yake inawachukua watendaji ambao wizara zao zimevunjwa kwa lengo la kuwawezesha watendaji hao kuendelea kulitumikia taifa lao. Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Ofisi ya Mdhibiti imetakiwa ichague Wakaguzi wa Ndani (*Internal Auditors*) ambao walikuwa wanazitumikia wizara hizo.

Mhe. Naibu Spika, hilo sio wazo baya kwa taasisi za kawaida, lakini sio kwa ofisi muhimu kama hii. Hivyo, kwa heshima zote na kwa mara nyengine tena tunaiomba serikali kuiruhusu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea na mchakato wa ajira ambao iliuanza kwa lengo la kupata vijana madhubuti watakaoweza kuleta tija na kufanikisha malengo ya uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibiti.

Sambamba na kuziba pengo hili la nafasi za kazi katika taasisi hii kwa vile kuendelea kuwepo kwa pengo hilo kunaweza kuathiri utendaji kazi wa ofisi hii nyeti hapa nchini. Aidha, kamati hii inaikumbusha serikali kuwa kiwango cha juu cha ubora wa kazi za ofisi hii na utendaji wa kazi unaozingatia weledi vitaweza tu kufikiwa kwa kupata watumishi wenye sifa stahiki, maadili, na bidii ya kuchapa kazi na wanaoweza kwenda sambamba na kasi kubwa ya mageuzi katika sekta ya ukaguzi na fedha. Mhe. Naibu Spika, hivyo, serikali inapaswa kuhakikisha kuwa watumishi watakaofanya kazi katika ofisi hii wawe wamekidhi vigezo hivyo. Njia bora ya upimaji wa hilo ni kwa Mdhibiti kuwafanyia usaili (*interview*) na kuridhika na matokeo yao, jambo ambalo litakuwa sio busara kwa wale watendaji ambao tayari wameshatumikia taifa hili na leo wakafanyiwa usaili.

Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza serikali kwa kuiongezea mshahara Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hivi karibu. Pamoja na pongezi hizo bado nyongeza hiyo iliyofanywa haijakidhi haja kwani ofisi hii inawakagua watendaji ambao mshahara wao ni mkubwa ukilinganisha na mshahara wa Mkaguzi. Hali hii inaweza ikachochea vitendo vya rushwa na kuondosha kabisa dhamira ya kuanzishwa kwa ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inaiomba serikali kutekeleza kwa vitendo kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein ya kuwa mtu akipewa mzigo basi apewe na kata ya kubebea mzigo huo ili aweze kuubeba bila ya

matatizo na vishawishi vyovyote. Kwa msingi huo, tunaiomba serikali kulifikiria suala hili kwa umakini zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo kamati yangu inataka kujua ni vigezo gani vilivyotumiwa na wizara inayohusiana na masuala ya utumishi wakati ilivyofanya nyongeza hiyo ya mishahara kwa ofisi hii. Mhe. Naibu Spika, tunauliza hili kwa kuwa wakati Kamati ya *PAC* inafanya majadiliano na Ofisi ya Mdhibiti, ofisi hii ilishindwa kutoa jibu sahihi kwa kuwa wao walipelekewa orodha tu ya malipo inayoonesha nani atalipwa nini na nani atalipwa nini bila ya kujua mfumo (*formular*) iliyotumika.

Mhe. Naibu Spika, wakati Kamati ya *PAC* ilipokuwa ikichunguza na kupitia Fungu la Ofisi hii (G 06), ilibaini masuala kadhaa ikiwemo kupangwa kwa viwango vya fedha vinavyofanana katika shughuli tofauti. Kwa mfano, katika progarmu ndogo ya udhibiti na ukaguzi, Pemba kifungu 2206005 kinachohusiana na vifaa vya kompyuta kimekadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 3,500,000 na kifungu 6112208 kinachohusiana na ununuzi wa kompyuta pia kimekadiriwa kutumia kiwango hicho (Tsh 3,500,000).

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* imehisi kuwa kuweka makadirio ya viwango vya fedha vinavyolingana katika shughuli mbili tofauti ambazo kiuhalisia hazipaswi kuwa hivyo kunaweza kukaleta dhana na hisia za makadirio yenye mashaka. Hivyo, kamati hii inaishauri Ofisi ya Mdhibiti pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango katika miaka ijayo ya fedha kuyachunguza kwa makini makadirio yaliyopangwa katika kila shughuli ili makadirio hayo yalingane na uhalisia kwa lengo la kumuondoa mashaka mchambuzi wa bajeti.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikadiriwa kukusanya Tsh. 28,213,000 kutokana na ada ya ukaguzi wa hesabu ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016, fedha zilizokusanywa ni Tsh. 29, 000,000, sawa na asilimia 102 ya makadirio. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, ofisi hii inakadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 65,864,000.

Mhe. Naibu Spika, kamati inawapongeza sana watendaji wa ofisi hii kwa kazi kubwa waliyoifanya iliyopelekea kuvuka lengo la makusanyo ya mapato katika mwaka wa fedha unaomalizika. Aidha, kamati inawasihi watendaji hao kuendelea na moyo wao wa kuchapa kazi kwa bidii ili waweze kuendelea kuvuka lengo la makusanyo na kwa mwaka wa huu wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, hatuna budi kutamka kuwa, ni kweli Ofisi ya Mdhibiti ina dhamira ya kutekeleza malengo ya serikali ya kuongeza ukusanyaji wa mapato kama tulivyoelezwa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha hotuba yake mnamo tarehe 18 Mei, 2016 mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, tumetamka hili kwa kuwa Ofisi ya Mdhibiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imekadiriwa kukusanya zaidi ya asilimia 133 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa na Baraza lako tukufu kutumia jumla ya Tsh. 2,341,600,000 kwa kazi za kawaida ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016 fedha zilizopatikana zilikuwa ni Tsh. 1,800,451,750 sawa na asilimia 77. Aidha, takwimu za kibajeti zinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi hii iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 2,023,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2015, ofisi hii ilikuwa imeshaingiziwa jumla ya Tsh. 1,661,300,000 sawa na asilimia 82.1 ya fedha zilizoidhinishwa. Kwa msingi huo, ni wazi kuwa uingizaji wa fedha katika ofisi hii kutoka serikalini umekuwa wa kuridhisha ingawa itaonekana asilimia kama imeshuka kidogo. Hivyo, kamati inaipongeza sana serikali kwa kuuona umuhimu wa ofisi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imepangiwa kutekeleza Programu kuu mbili na Programu Ndogo mbili. Programu Kuu ya kwanza ni Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma ambayo programu yake ndogo ni hiyo hiyo. Programu kuu ya pili ni Utawala na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi,yenye programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi na Programu ya Udhibiti na Ukaguzi Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mujibu wa programu hizo, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 2,244,800,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (*PAC*), imeyaridhia na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 bila ya marekebisho yoyote.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwashukuru kwa upekee Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao wa kunisikiliza wakati wote nilipokuwa nawasilisha hotuba hii. Ni matarajio yangu kuwa, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza nao watatoa michango yao yenye tija na manufaa ya ofisi hii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. i(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru Mhe. Salma Mussa Bilali kwa niaba ya Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na nimepata wachangiaji sita, kwa muda tulionao tunaweza tukapata angalau watatu kati ya hao. Kwa hiyo naomba mwanzo nimkaribishe Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf atakayefuata atakuwa Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadae ajitayarishe Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Mhe. Naibu Spika ahsante, namshukuru Mwenyezi Mungu kwanza kwa kunipa uzima na kutupa uzima sisi sote kwa ujumla. Pia nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kwanza leo katika kuchangia hotuba hii ikiwa mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati hii. Pia napenda kuwapa pongezi na shukurani zangu za dhati wananchi wangu wa Jimbo la Chaani.

Mhe. Naibu Spika, natanguliza shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri wa wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa kututayarishia kitabu kizuri kinachofahamika na kueleweka, nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa mimi ni mjumbe lakini nitaomba sana na nina mada zangu kama nne hivi za kuchangia; nitaanza na kusimamia ajira katika sekta ya umma. Kwa kweli Zanzibar kuna upungufu mkubwa wa ajira hasa kwa wananchi Wazanzibari nikimaanisha Unguja na Pemba. Zanzibar ina utalii mkubwa, ina hoteli kubwa zaidi ya 200, ina biashara za *restaurant* zilizokuwa kubwa na ndogo. Ina biashara ya viwanda, ina biashara ya maduka makubwa na madogo, lakini cha ajabu sana kwamba kwenye sekta hizi nyingi tunaambiwa ati Wazanzibari hawawezi, ndio maana wanapewa Wakenya na watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana wizara hii ifuatilie kwenye kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar (Unguja na Pemba) wanapata *priority* kubwa sana ya kupata ajira kwenye *investment* yoyote itakayofanyika ndani ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye mahoteli, kwa sababu ndiko kwenye ajira nyingi Zanzibar na viwanda. Ukienda kwenye hizi hoteli nyingi hasa kubwa na *middle standard* kuanzia *three star* hadi *five star* watendaji wengi mle ndani unakuta nafasi nzuri zote wanashika wageni - Wakenya, Waganda, lakini Wazanzibari au Watanzania unaambiwa hawawezi kazi. Suala hili linakera kwa sababu Wazanzibari wanaweza kufanya kazi na wameendelea mapema kuliko hao wengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mimi mwenyewe nayafahamu mambo ya hoteli, kuna nafasi nyingi za kupata Wazanzibari hata waliokuwa hawajasoma darasa hata la nne na wakapata kazi ndani ya hoteli. Zipo nafasi sikatai kupewa Mzungu au kupewa Mtu wa East Africa, kama nafasi ya *manager*, *president* au *CEO* wa ile hoteli, ikiwa *operation manager*, *marketing manager*, akiwa *Front Office Manager* na *special chef* (*expert chef*) wa kupika kwenye hoteli kubwa. Nafasi hizi mimi sikatai akipewa mtu wa nje, lakini wasaidizi wa nafasi hizi Zanzibar tunaweza tukawapa hata waliokuwa hawana elimu kubwa wakatekeleza hii kazi vizuri, kuliko kuleta watu wengine kutoka Kenya na Uganda.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana wizara hii pamoja na kushirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Umaduni na Michezo wakahakikisha kwamba wanakwenda kwenye mahoteli na vitega uchumi vyote pamoja na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wakaangalia Wazanzibari wangapi wamepewa ajira katika vitega uchumi hivi. Kwa sababu hivi vitu ni vya Zanzbar na nchi yoyote duniani kitu cha mwanzo wanapewa wazalendo hawaletwi watu kutoka nje. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nimeshafanya utafiti mkubwa kwenye mahoteli na sehemu nyengine nyingi, kitu kikubwa wengine wanawekewa vikwazo vikubwa sana na hasa kwenye masuala ya dini, utaambiwa mtu labda hapewi kazi ya *waitress* au *housekeeping* ya kusafisha kwa kuwa amekataa kuvaa nguo fupi. Kwa sababu sisi Waisilamu hatuwezi kuvalishwa nguo fupi na watu wanaotaka kuweka sheria hii ya nguo fupi.

Mhe. Naibu Spika, kuna vitu lazima serikali viweke sheria kali kwa sababu watu wengi hawapati kazi kwa sababu ya mambo kama haya, wanadhalilishwa, wanaambiwa wewe huwezi kuvaa nguo fupi na Muisilamu mwanamke atavaaje nguo fupi akaonekana miguu yote. Ningeomba sana wizara hizi zikashirikiana kwenye kufanya utafiti wa hali ya juu kuhakikisha Wazanzibari wote wanapata kazi kwenye nafasi ya asilimia 80 ya biashara. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano Hoteli ya Kempinski ambayo sasa hivi inaitwa Melia, ile hoteli ina wafanyakazi karibu 370 kipindi cha nyuma lakini ukiangalia mle ndan sifikirii hata kama kuna Wazanzibari 15 wenye ajira. Ningeomba sana suala la ajira wizara zote tatu, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko; Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora zikahakikisha kwamba zinasimamia vya kutosha kwa wananchi wa Zanzibar wapewe ajira kwa njia zinazohusika.

Vikwazo vingi wanavipata hasa kwenye suala la unyanyasaji. Siku hizi watu hawapewi ajira wananyanyaswa hasa wanawake wanaokwenda kuomba kazi lazima wataletewa mambo ya mapenzi mwanzo ndio wapewe kazi. Mhe. Waziri namuomba sana waweke sheria ngumu kwenye masuala haya, kwa sababu inaonekana sheria zetu nyengine zinawalinda hawa wahalifu.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye Ofisi ya Mufti ambayo ipo chini ya wizara hii. Kwa kweli inasikitisha, Ofisi ya Mufti ipo lakini mpaka leo walimu wa vyuo wamekaa kama waliokufa hawakumbukwi kwa njia yoyote ile, walimu wa vyuoni hawalipwi mishahara, hawana nguvu yoyote ndani ya nchi hii zaidi ya walimu wa skuli ndio wanaojulikana. Ningeomba sana wizara hii na nina swali langu naomba kuuliza. Je, hii Ofisi ya Mufti imekaa lini hasa naomba Mhe. Waziri aje anijibu. Na hizi kamati za walimu wa vyuoni katika majimbo mji wa Zanzibar lini imekaa nao hasa kuhakikisha inatatua matatizo yao? Na lini wamekaa nao kufikiria vipi watawasaidia kwenye masuala ya elimu?

Kwa sababu leo hii nchi ina Waisilamu asilimia 99.7 tunataka tukangamizwe kwa njia nyengine za kinyume mimi hili sikubaliani nalo. Ningeomba sana Mhe. Mufti wa Zanzibar akae ashirikiane na walimu wote awaunge mkono aende kwenye mambo ya sheria waingizwe kwenye kulipwa mishahara japo kima kidogo.

Mhe. Naibu Spika, cha ajabu vyuo vya mjini walimu wanalipwa kila mwezi, wazee wanalipa kama shilingi 5,000 au 10,000 mwenye uwezo 20,000; lakini shamba mzee shilingi 500 hawezi kulipa. Ningeiomba sana serikali ingewakumbuka wale walimu hasa wa vyuo vya shamba kwa kila mwezi angalau wakawalipa shilingi 100,000/-, sio Ofisi ya Mufti, Ofisi ya Mufti itakaa tu isubiri ipelekewe *tender* kutoka Saudi Arabia shilingi 400,000,000 kila Mwezi wa Ramadhani hivyo hatutaki, wao wanatakiwa watoke. Mimi ushauri wangu Ofisi ya Mufti Mkuu itoke ndani ya ofisi yao waende nchi za nje kama serikali haina uwezo wa kulipa au haina dini watoke wao kama kamati ya

Kiisilamu wakaombe nchi kama Saudi Arabia, Iran na nchi za Kiarabu au nyengine zenye dini wakaombe msaada walipwe hawa walimu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia mshahara wala si mkubwa, watu wa shamba hawana makuu kama watu wengine wakipewa shilingi 100,000 walimu wataweza kuridhika kwa sababu hivi sasa hata shilingi 5,000 ya kununua sabuni hawapewi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sisi ni Waisilamu na Mtume Muhammad (*S.A.W*) kashushiwa wahai wa kuja kutufundisha sisi. Mimi suala la dini nitalizungumza hata kama serikali inasema haina dini lakini nitaliwekea kipaumbele. Kwa kweli tunajisahau, sisi sote humu ndani ni Waisilamu lakini kwenye suala la dini tumelipa, tusikae tukajadili walimu wa skuli tuna walimu wengine. Humu tukiletewa masuala mengine mbio tunaya-*support* hasa masuala ya sherehe na mambo ya mipira, lakini kweli tuna siku tuliozungumza masuala ya dini, hebu tukumbukeni kama sisi hapa tunapita tu, tutakwenda kwenda kujibu ndio huko. Mimi ningeomba sana walimu wafanyiwe maarifa yoyote watiliwe kwenye sheria hasa ikiwezekana kwamba na wao watambulikane walipwe.

Mhe. Naibu Spika, suala la sheria. Kwa kweli tuna sheria sisi wenyewe tunaziachia zinakuwa nyepesi. Sisi Wazanzibari kuna siku tunatakiwa tukakamae. Kuna suala la silaha, Dar es Salaam wana sehemu zinauzwa silaha Kikosi cha Mizinga sijui na kikosi gani, kikosi ni idara ya mtu binafsi, mmiliki mtu binafsi ameshirikiana na serikali kwenye kuuza zile silaha. Lakini cha ajabu kwamba Zanzibar inapewa leseni magobore, inatoa leseni ya *air gun*, inatoa hapo Ofisi Kuu ya Kamishna wa Polisi Zanzibar, lakini cha ajabu tunakwenda kununua Tanzania. Mimi naiomba serikali kwa kushirikiana na wizara hii nipo tayari kujenga kama walivyojenga Dar es Salaam na kuleta silaha za *air gun* na *shotgun* kuuza hapa Zanzibar tukapata wenyewe mapato.

Mhe. Naibu Spika, haiwezekani Wazanzibari tunatoa leseni wenyewe hapa lakini *shotgun* na *air gun* tukanunue Dar es Salaam mimi hilo suala siliungi mkono. Mimi niko tayari kufungua kwa kushirikiana na serikali mtaji kama ule waliofungua Dar es Salaam Serikali ya Zanzibar ikapata mapato, Wazanzibari wanaomiliki *shotgun* hapa Zanzibar wako zaidi ya 1,300 na kila *shotgun* moja Dar es Salaam ya rahisi inauzwa shilingi 800,000 au shilingi 1,200,000. Mimi niko tayari ku-*invest* na serikali hata shilingi bilioni mbili kufungua huo mtaji hapa, tusikae tu kila kitu tukanunue Dar es Salaam. Tungule tukanunue Dar es Salaam, vitunguu tukanuue huko basi mpaka hizo silaha, tunao uwezo wa kufungua sisi hapa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana wizara hii ingeweka sheria kali na ninaishauri serikali na wizara kwa wale wote wanaobaka watoto wadogo, wale wote wanaoleta unga, majambazi iweke sheria ya kuwanyonga wakikamatwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama hatujachukua hatua za kidikteta nyengine kwenye kukomesha hili, kama hatujawanyonga kama nchi ya Iran na Saud Arabia na China hawa watu wataendelea tuwanyonge hawa. Kila siku wanakaa wanafungwa halafu wanatoka unaambiwa ushahidi haupo hawa wakamatwe wanyongwe. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tafadhalini sana meza mtaziharibu tunazitaka hizo na mwakani na siku nyengine, mnavyopiga mnapiga sana. Waheshimiwa Wajumbe kwanza nikwambieni mnawaumiza wengine, wengine hawawezi kuchukua masikio yao hilo mlijue. Kwa hiyo, nawaomba sana kweli maneno anayosema Mheshimiwa yanafurahisha lakini tusiwaumize wengine na tusiziumize meza. Endelea Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana lakini kama nilivyoeleza kwamba wanasheria weti wawe wakakamavu washindane na wanasheria wa Tanzania. Kuna sheria tunao uwezo sisi wenyewe kuziweka tukafanya wenyewe Zanzibar, tusitegee kila kitu tukanunue Tanzania wakati sisi tunao uwezo wa kufungua mambo kama hayo, hakuna masikini huku sisi wenyewe ni matajiri vile vile wa kufanya hayo.

Mhe. Naibu Spika, inakera kweli kweli, mimi niko tayari kushirikiana na serikali kufungua hili suala hata kesho niko tayari. Kwa sababu sheria tunayo ya leseni hizo tumekaa tunakwenda kununua kule kuna usumbufu hajulikani Mheshimiwa nani hajulikani mtu wa kawaida nani tunasumbuka tu wengine.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ningeomba kuchangia suala la nyaraka. Mheshimiwa namsifu sana Mhe. Waziri pamoja na viongozi wake wote kwa suala la kuweka *Camera* kwenye vyumba vya nyaraka kwa ajili ya kurikodi na kuchunguza wale watu wote wanaoingia na kutoka. Nawapongeza sana kwa suala hili la *installation* za *CCTV Camera* ndani ya chumba kile. Kwa sababu naamini atakayepita, atakayekwenda itakuwa inamrekodi masaa yote na ni suala zuri.

Vile vile ningependelea kutoa ushauri kama ilivyo nafasi nyengine kwenye wizara nyengine watu wanaoajiriwa kuna wizara hasa inatakiwa mfano kama Ikulu ninavyofahamu mimi sio hapa, natolea mfano kwengine. Wafanyakazi

wa Ikulu hata anayefagia choo anatakiwa awe polisi. Sasa kwenye chumba cha nyaraka au wizara hii kwenye sehemu hii naomba waajiriwa wote wawe usalama wa taifa au polisi ndio wafanye kazi, wasiwe watu wa kawaida wakafanya mambo ya vurugu mechi ndani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kuwa ni Mjumbe wa Kamati hii nimeona nisichangie sana niseme haya tu, lakini naomba sana wizara zote nilizozitaja ziangaliwe vipi itawezekana. nashukuru sana na ninawapongeza wote naikubali asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli afisi hii ni pana sana kwa upana wake na naipongeza sana serikali kwa umahiri wake wa kuweka afisi kwa sababu ni afisi inayotuongoza katika mambo yetu ya Sheria na Utawala Bora. Kwa kweli nampongeza pia Rais wetu wa Zanzibar Dkt Ali Mohd Shein kwa jinsi anavyotuongoza katika nchi yetu pamoja na Utawala Bora ambao anauendeleza.

Kwa kweli nimeona mengi lakini mengine ambayo Utawala Bora ambao wa dhahiri umeonekana pia nawaambia Baraza zima hili la Wawakilishi wakaangalie Hospitali ya Mkoani jinsi ilivyojengwa kisasa na jinsi itakavyomaliza kwa muda wake. Huu ndio uongozi bora ambao kwa kweli tukifanya kitu kimalizike. Pale Dkt Ali Mohd Shein watu wake ambao amewakabidhi hospitali ile kwa kweli wanahitaji sifa sana.

Hilo nimshukuru zaidi na pia tuwe na mfano wa hapa mambo mengi walikuwa watu hawasemi lakini mnara wetu ulioko pale Michenzani watu hawakufikiria kama utajengwa. Lakini Dkt. Ali Mohd Shein alisema na ametenda na hii ndio sifa yake anasema anachoahidi ni kile ambacho anaweza akakitenda. Kwa hilo tumshukuruni sana Dkt Ali Mohd Shein ahadi zake ni za kweli. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na mimi niendelee katika kuwashukuru watu wangu wa Jimbo la Chake chake kwa kunileta hapa pia niendelee pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Sasa nianze katika hotuba yangu ya kuchangia Mhe. Naibu Spika, niendelee kwenye sehemu ya kuanza kwenye sehemu yetu ya Majaji katika kesi. Mhe. Naibu Spika, nafahamu umahiri wao wa Majaji wetu ambao wanaendeleza kesi

zetu na pia ni waaminifu kwa kiasi fulani wametufikisha pahali pazuri katika Utawala Bora.

Mimi kama ni wazo au ni jambo ni kwamba Waheshimiwa wale tunawapa kazi kubwa sana na wao wanataka kuhukumu haki ya mtu, wakati wao wale mawakili au wale watu ambao wanakuwa wanahojiwa Mhe. Waziri majaji wanakuwa na kazi ya kusikiliza wanakuwa na kazi ya kupima, wanakuwa na kazi ya kuandika.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningemshauri sana wale majaji wasiwe watu wa kuandika. Kwa sababu kukwambia kweli kazi ya kumsiliza mtu anacho kisema ukamsikiliza, ukampima baadae ukandaika kwa kweli ni kazi kubwa sana hata yeye hupati kumpima vizuri kwa sababu kuna vipimo vyengine ni vya kutizama uso. Unamtizama tu yule anasema unamjua tu kwamba huyu muuongo au huyu mkweli.

Sasa Jaji anapokaa pale hamtizami kazi yake ni kuandika tu mpaka mwisho wa kesi na baadae ndio anakuja kufanya majumuisho, kwa kweli kesi inampa tabu sana. Baadae inaweza kufika mwezi bado anaitafakari ile kesi kwa majukumu makubwa aliyopewa. Mimi ningeshauri sana serikali yangu tukufu ikawapa wasaidizi wale watu majaji wakapata kuandikiwa wao wakapata kupima wao wakapata kusoma kwa utulivu na pia akawa amepata upeo maalum wa kumuangalia yule mtu ambae alikuwa anahojiwa katika habari zile. Mhe. Naibu Spika, hilo nilitaka niliseme ili haki itende zaidi katika kituo kile.

Jengine nilikuwa nasema katika nchi za wenzetu mawakili hapa kufikia sasa hivi tumeshakuwa na mawakili wengi kweli kweli na tunaongezeka. Serikali tunaongezeka kwa hilo inazidi kuwasomesha tuna wanasheria wengi. Lakini Mheshimiwa hawa nataka niseme kidogo na wao watumie ujuzi wao mwengine kwa sababu wengi wanasuburi mahakama, wengi wanafungua afisi zao. Lakini kwa nchi za wenzetu mawakili anatafuta kesi za kujikimu mwenyewe anaenoa mtu huyu kaonewa anamuendea wanazungumza, basi yeye kama yeye anaichukuwa kesi ile anamtetea ule mtu mpaka haki yake inapatikana baadae wanagawana wanazungumza katika mpango ule, si tu mawakili lazima waajiriwe, lazima wawe na tabu hii.

Mimi nawashauri sana mawakili wetu wakawasaidia kuna watu wana matatizo ya chini, wana matatizo kwenye mambo yao ya ardhi, wanamatatizo chungu nzima. Lakini mawakili wetu wanakaa tu, wanakaa ndani, wanaona mpaka ukamuendee umpe pesa nyingi. Mimi ningeshauri kama kutakuwa na kitengo cha dhamana baina ya yule atakaekuwa anataka kusaidiwa basi si lazima awe

na pesa, wewe nenda ukafunge nae mikataba uendelee na ile kesi, ili umsaidie yule bwana kupata haki yake na wewe pia utapata riziki yako.

Ningeshauri sana hili kama mawakili wananifahamu, wamenisikia na nawaomba radhi kama nitakuwa nimewakosea ili nisicheze nao wale ni wasomi, mimi sie. Mimi nilikuwa nashauri tu kama itawezekana hilo ili liendelee.

Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa nazungumzia kuhusu siri za serikali. Mheshimiwa tunapiga makelele sana kwamba siri za serikali zinatoka nje, zinapatikana ovyo ovyo. Mimi nataka niseme kuna watu wawili katika serikali ni watu wazuri na ni watu wabaya. Mmoja dereva wa gari; maafisa viongozi wanaoingia kwenye magari mnawaona madereva mnaokaa nao ndio pa kusemea siri zenu; dereva anatia gia na huku anakusikiliza wewe, anavuta mafuta na huku anakusikiliza wewe. Siri zinaanza kutoka pale akishuka tu amekaa na madereva wenzake. Tuwe makini sana na suala hili. (*Makofi*)

Pia *type writers* wetu hawa walioko ofisini. Mhe. Naibu Spika, wale watu tumewaweka watu *simple,* tumewaweka tu Mheshimiwa siri inaanza kutoka pale imeandikwa *memo,* afisa amemwambiwa chapa anaitoa *copy* anapeleka pahala. Watu wale ni watu muhimu sana tunawadharau, tunawaona ni watu wadogo wadogo mpigaji chapa pale ndio panapoanza shughuli.

Mimi ningeshauri sana Maofisa mlioko pale mkachagua mpigaji chapa ambae anaenda pamoja na serikali, vyenginevyo kwa watu hawa itakuwa sisi hatuna siri na ndio wanavyosema wenzetu ikianguka shindano Ikulu tunaisikia, mawaziri ni nyinyi, wapigaji chapa ndio sisi. Kwa hivyo, ikitoka siri inatoka siri kila mmoja anaiona. Mhe. Naibu Spika, ningeshauri masuala hayo kidogo yaweze kuekewa utaratibu mzuri.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie pia sheria zetu za kuajiri; nilisema juzi nasemea tena. Mhe. Naibu Spika, kila mtu ambaye yuko katika nchi hii ana uhuru na ana upeo wa kuitumikia serikali yake kwa njia moja au nyengine. Mhe. Naibu Spika, kweli elimu hailingani, viungo havilingani, tabia hazilingani. Lakini kila mmoja ana uwezo wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme kwamba mtu wa darasa la saba huwezi kumlinganisha na mtu wa darasa la kumi wala kumi na mbili. Ningeshauri ajira zitakazotoka ili kila mmoja apate faida, wa darasa la saba wawekwe pao, wa darasa la kumi waweke pao na kumi na mbili wawekwe pao na Vyuo Vikuu wawekwe pao. Ningeshauri sana Mhe. Naibu Spika, hili likafanyiwa kazi

kwani wale watu wa chini ni wapiga kura wetu, wametupigia kura na wao wanahitaji kutoa mchango wao katika serikali hii. Usimwambie hana elimu asipokuwa na elimu ile atakuwa na nguvu kuna watu wanaelimu hawana nguvu, sasa hawezi kufanya kazi ile. Kwa hivyo, wale wenye nguvu watasaidia kazi za nguvu. Ningeshauri sana habari hiyo kidogo nayo ieleweke kwa ukarimu zaidi.

Pia nizungumzie pia hii sehemu ya mufti aliyoisema sheikh wangu Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf Al-Wardy pale na mimi naligusa kidogo. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi hata jana tuliweka hoja ya kuwa wenzetu wanaowafanyiwa vitendo, wana CCM walioko Pemba. Mhe. Naibu Spika, tumeizungumzia kwa kina. Kwa kweli mpaka sasa hivi kwa upande wa Zanzibar nilizungumzia tena kuwa bado ni ndugu na tutabaki kuwa ndugu.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ukanda huu wa mufti na mashekhe wanaupeo mkubwa wa kulimaliza suala hili bila ya hata serikali. Kwa sababu wanaofanya mambo haya takribani misikiti, ndiyo inayofanya mambo haya kwa kupitia mashekhe wake. Kwa hivyo, ningelishauri suala hili likapelekwa kwenye dini likasomeshwa vizuri tukaondokana jambo hili kwa salama na amani bila ya kuingia nguvu za dola.

Ningeshauri afisi hizi za Mufti pamoja na shekhe mkuu zikafanya ziara, zikatuliza masuala haya na wakawapa waidhi wakawapa mambo mengi mazuri ya duniani na akhera kuondokana na suala hili ambalo silioni kama lina tija katika nchi yetu zaidi ya hasara zinazotujia hasa kwa wanawake, watoto na wazee. Wanaume wanapiga mbio lakini hapa hali ikichafuka wanawake ndio wanaathirika watoto na wazee.

Mimi ninachotaka kusema Mhe. Naibu Spika, mtu yeyote ambae anahubiri vita ana mtoto, ana mama, ana mke basi mke wake hampendi wala mwanawe hampendi, wala mama yake hampendi na watu wake hawapendi.

Mtu ambae anahubiri vita akiwa na familia huyo Mheshimiwa kwa kusema kweli haipendi familia yake na hata akimwambia mke wangu *I love you* kama mwanamke anajua angemwambia kabisa kuwa wewe hunipendi. Hunipendi kabisa usingetafuta masuala haya. Hunipendi kwa mambo mawili; hunipendi unataka tubaguke mimi na wewe kwa sababu vita vikikamata hatukai tena mimi na wewe.

Pia hunipendi vita vikitokea basi watoto watakufa na mimi nitakufa. Mhe. Naibu Spika, ningeshauri sana masuala haya kama niliovyosema yaingie

kwenye suala la dini kidogo serikali iwape nguvu watu wa dini walirudishe hili suala liende, likazungumzwe kwa kina, kwa sababu hili ni usalama wetu na masuala haya kwa kweli yanahitaji mambo mengi.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niendelee tena kidogo, najua ukiachia sheria zetu, katiba yetu lakini tuna pia suala hili la uisilamu ambalo tuna mashekhe wetu wanatusaidia katika ndoa na katika matatizo yetu ya kibinafsi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wanafanya kazi nzuri mashekhe wetu, wanafanyakazi nzuri hizi mahakama zetu. Lakini nataka niwaambie kidogo kwa ushauri wangu wanatizama upande mmoja, hawatizami pande mbili. Wanatizama upande ule ambao wakati wa kuozesha utaona na vitabu. Lakini Mhe. Naibu Spika, juzi hapa kulikuwa na suala la Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto alilizungumza na alilitolea ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, suala la kubaka suala la kudharauliwa akina mama na watoto hasa suala la mama anapoachwa na watoto akasukumwa mitaani, mama mwenyewe anakosa hadhi mama mwenyewe umeshamfuja, lakini watoto wako ambao umewazaa mwyenyewe watakuwa watoto wa mitaani hawapati elimu na pia watoto wale ndio mateja ambao wanatufikia hapa au watoto wale ndio wezi wanaofika kuuliwa.

Sasa sisi kama Serikali na Utawala Bora tusikubali kupelekeshwa, huko watu hawa ambao wanatudhalilishia wake na wanatudhalilishia watoto. Mimi sikubaliani nao na naamini serikali haikubaliani nao na hata dini haikubali. Mhe. Naibu Spika, juzi kama nimesikiliza vizuri Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto alizungumza kwamba sheria hii ya kugawana mali na kupunguza matatizo haya imeshatengenezwa, Bara wenzetu wanayo ambayo tayari na kule mimi ninavyofahamu ni Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania na watu wale ni kwamba sisi tuna Wawakilishi ambao wako kule katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ningelishauri Baraza langu tukufu, ningekushauri Naibu Spika ulioko hapo, Makamu wa Pili na wote na hao mashekhe wenyewe ambao pia nahisi kwamba hii si urathi, hii ni fidia tunazokosana baada ya machafuko. Nikafikiria tu kwamba kama kuna uwezekano basi suala hili lipelekwe kwa mashekhe wakalingalie kwa kina na kwa kuwa sheria zimeshatungwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza letu tukufu hili la Wawakilishi basi nalo liridhie, ili tupitishe sheria na tukomeshe vitendo hivi kwa vile tunavihangaikia kwa muda mrefu sana.

Mhe. Naibu Spika, ningeliomba hilo tungelifanyia utaratibu wa kina ili kupunguza watoto wa mitaani. Wale watoto wa mitaani Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie hakuna asiyekuwa na baba, wote wana baba, lakini baba wenyewe ndio kama tunavyoona. Kama sheria haijachukua mkondo wake tutapata watoto wale siku zote. Ningeishauri serikali yetu ifanye utaratibu huo Mhe. Naibu Spika, wa suala zima hili ili mambo yetu kidogo yawe sawa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme suala la nyaraka; watu wetu, serikali yetu wafanyakazi wetu wa nyaraka wanajitahidi kutuwekea nyaraka vizuri sana. Lakini nataka nikwambie kwamba kuna baadhi ya watendaji wetu si waaminifu. Mimi nataka nikwambie nina ushahidi wangu mwenyewe Waziri akitaka mimi nitampa. Mimi nina nyumba ambayo nimerithi kwa baba yangu toka kainunua 1975, kuna mtu akatengeneza nyaraka nyengine ya mwaka 2010 mwezi wa 10, mtu huyo ambae alietaka kupewa hiyo nyumba, ili kwa kusema nyumba hiyo eti mimi hainihusu aliniuliza waraka wewe unao nikamwabia sina, akaenda kutengeneza wake wa 2010 cha kushangaza kwamba nyumba hiyo ilikuwa ya baba yake lakini cha kushangaza baba yake alikufa mwaka 2010 mwezi wa 6, saini aliitia baba yake huyo huyo aliekufa alitia 2010 mwezi wa 11, nikamuuliza jaji na Mwenyezi Mungu jaji alimpa kiwango cha juu babaake alifufuka akenda akatia saini na kurudi?

Sasa Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie walikuja watu wa Kamisheni ya Nyaraka waliko Pemba wakanambia eti waraka una namba, waraka una mihuri, una kila kitu wakasema namba ya waraka huu hawauoni. Wakaleta waraka waliotengeneza wao siku mbili nyuma. Nilishangaa sana na mimi nilikuwa kidogo nina maswali yangu niliyowauliza kuhusu ule waraka. Niliwauliza kama namba hii haiko, alipewa namba hii sasa hivi na nani, wakashindwa kunijibu.

Mhe. Naibu Spika, vitendo hivi vinafanyika sio kwangu tu vinafanyika na ndio matatizo ya ardhi na vitu vyengine hawa wanatusababishia na rushwa imekuwa nyingi. Matatizo haya yamekuwa makubwa kwenye serikali, imekuwa kwa kweli hawaaminiki, wanatufanyia mambo yaliokuwa hayana maana. Kwa pesa watatufikisha wapi nchi hii.

Mhe. Rais, anapiga kelele kila siku watu hawa kila mmoja akiwa masikini akiwa tajiri apate haki yake. Lakini leo haki inakwenda kwa tajiri ambaye atatoa pesa au mwenye uwezo. Hili Mhe. Waziri naomba mliangalie sana kwa sababu lina matatizo yake sana.

Mimi ningesema tena Mhe. Naibu Spika, wazee wale waliofikia miaka 70 ambao Dkt. Ali Mohd Shein pia ameleta mfuko wa kuwasaidia....

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika 4 za kumalizia.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Wale wazee waliofika miaka 70, mimi najua hili suala kalitoa kwa nia njema. Lakini Mheshimiwa nataka niseme kule Pemba matatizo yaliyojitokeza ni mengi, wazee waliofikia miaka 70 wapo wengi walioandikishwa na wakati wakiandikishwa akifika anamuuliza yule muandikishaji wewe mama una miaka mingani, hujibu aah wewe andika vyovyote tu hata 40 sasa watu wana miaka 70 wana miaka 80 ukimuangalia kwenye kitambulisho ana miaka 40. Mimi ningeshauri sana yale mambo yakatizamwa kwa kina jinsi wale wazee waliokwisha kufikia ile haki kutokana na maandishi na mambo, basi liweze kurekebishwa. Mhe. Naibu Spika, naenda *speed* sana kwa sababu ya muda.

Sasa mimi niseme maeneo jamani ya hospitali mengine ambayo yanakuwa yanategemea sana wananchi. Mhe. Naibu Spika, kwa sasa hivi pale pana rushwa mbili, kumejitokeza rushwa, namuomba waziri suala hili aliangalie sana. Kuna rushwa ya pesa na kuna rushwa ya chama. Mtu akiwa mwanachama wa chama chengine hashughulikiwi au kunakuwa na mashaka mengine au hana pesa hashughulikiwi. Mhe. Naibu Spika, mambo haya yalitaka tuyatizame kabisa ili tuangalie hatma ya matatizo yetu.

Nije kwenye Mashirika ya Umma, Mashirika yetu ya Umma yamekuwa na mashaka hayaji juu. Serikali inaanzisha Mashirika ya Umma kwa nia njema lakini wanaopewa hawafikii malengo wala hayaendi. Matokeo yake yakimaliza Mashirika ya Umma na najua mdhibiti wa serikali yupo na kila kitu kinafanywa, mahesabu yule jamaa ameharibu kila kitu, amevuruga utaratibu wote anaondoshwa kwa kulindana anaekwa sehemu nyengine akamalize serikali, akawamalize walipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, waliangalie sana wanaofanya vitendo hivi basi licha ya kuondoshwa na kushitakiwa. Kwa sababu wanatuharibia wengine kwenye sehemu za ununuzi sehemu za matengenezo, sehemu ya uuzaji, ukarabati rushwa imetawala. Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana masuala haya yaangaliwe kwa kina.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kidogo kwa *speed* sana lakini naomba usiniharakishe utanibabaisha kidogo. Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze kwamba wale watu ambao wamemaliza muda, kama mtu amefikia miaka 60

mpaka 65. Mheshimiwa mpaka afa serikali ndiyo anaonekana mchapa kazi. Mheshimiwa serikali inapiga kelele vya kutosha kwamba kwa kweli tuna watu tunatafuta mbinu za kuongeza ajira. Mheshimiwa mtu kama miaka 60 hajajipanga, hajajiamulia kwenye maisha yake. Mheshimiwa huyo tumuache ni *condemn*. Tumuache afanye kazi zake za kibinafsi, hatumzuii lakini serikalini aondoke. Unakwenda mwezi mzima unamtafuta afisa hayupo, leo mshipa, leo hajesha kuoga, sijui leo hakufanya nini. Maana yake hajiwezi mwenyewe. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa naomba umalize.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja na mimi naomba kusema naunga mkono hoja, sijamaliza lakini ahsante sana mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Sasa nimkaribishe mheshimiwa wetu wa mwisho kwa mchana huu Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Na mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa maneno mazuri aliyozungumza kwenye hotuba yake na ningependa mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu niweze kuichangia hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, suala la kwanza ambalo ningependa kulijua kwa sababu Utumishi wa Umma upo chini ya Wizara hii. Nilitaka kujua sare ambayo inayotumika kwa ajili ya wafanyakazi, kuanzia madereva, wafanyakazi wa chini mpaka watumishi serikalini. Unakwenda maeneo unakuta kwamba wamevaa buibui, kama wanavaa nguo tujue. Lakini pia unawakuta saa nyengine wafanyakazi wananukia udi, maharufu utafikiri wanakwenda harusini.

Pia unakuta mtu ana mapete ya dhahabu kila kona utafikiri anakwenda harusini, utakuta wengine wanaume wamevaa yao hayaendi na ile kazi ambayo wanayoifanya. Kwa hivyo ningependa kujua. Kwenye suala la mavazi juu ya Utumishi wa Umma ni mavazi gani wanatakiwa wafanyakazi wa Serikali wavae pale mtu anahitaji huduma anapokwenda serikalini. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Suala la pili, ambalo nilitaka kulizungumzia ni suala la Mahakama. Mahakama zetu kuna harufu ya rushwa na hasa katika masuala ya madawa ya kulevya. Ningependa kujua. Kati ya muda wa miaka mitatu mpaka mitano ni kesi ngapi

watu wamekamatwa, wangapi wameshitakiwa, wangapi wamehukumiwa na ngapi zipo Mahakamani ambazo sisi hapa hatuwezi kuzijadili wala kuzigusa. Lakini hapa patakuwa na kivumbi. Ninahitaji taarifa kamili wakati Mhe. Waziri anapokuja kufanya *summary* ya bajeti yake.

Pia nimeangalia katika suala la bajeti la Mahakama, kwenye suala la *other charges (OC).* Ukingalia kwa kawaida hawa wanahitaji katika milioni mia moja mpaka milioni moja na ishirini kwa mwezi. Lakini ukiangalia katika *registry* zao walizokuwa nazo zaidi ya arobaini na tano Unguja na Pemba. Ukiangalia bajeti ambayo miaka ya nyuma, walikuwa hadi miaka ya nyuma wakipata miaka mitatu nyuma bilioni moja na laki tano. Lakini kutokana na kwamba serikali inataka ifanye mambo mengi sasa hivi, kuboresha mambo mengi ya utawala bora.

Unapotaja bajeti ambayo tokea mwaka jana ilikaribia sijui bilioni moja na laki mbili au laki tatu ile. Sasa mwaka huu ukiangalia unakuta bilioni moja laki moja. Naona kama ni kinyume tunarudi nyuma. Sasa kutoka bilioni moja laki tano miaka ya nyuma, tunashuka sasa bilioni moja na laki moja na hawa wanatumia karatasi nyingi, wana matumizi mengi ya *tonner*, ku-*print*. Hivi sisi tuweze kupata huduma wananchi wetu katika haya mambo mazima. Kwa hivyo bajeti hii haitoshi na kwa nini, ni sababu gani ambazo zimepelekea kushusha bajeti kiasi hichi.

Pia ninataka nizungumze katika hotuba ya Mhe. Rais kwenye ukurasa wa 64, alizungumza kwamba patajengwa Mahakama Kuu katika mji mpya wa Tunguu. Lakini katika suala la bajeti hakuna sehemu inayo-*indicate* kwamba hii Mahakama itajengwa na katika mambo yote ambayo serikali inaazimia katika kufanya mambo mazuri kwa ajili ya wananchi wake, sasa lazima tuboreshe katika masuala ya Mahakama ili haya mambo yaweze kuwa.

Pia nilikuwa ninataka kujua kuhusu suala la Mahakama ya Biashara. Hii Mahakama ya Biashara imefikia wapi na nini kinachoendelea na hadi leo katika kwangu hii sheria imepitishwa na mambo yote. Kwa nini Mahakama ya Biashara haipo. Lakini ukifuatilia katika suala la G 02 kwenye suala la bajeti ya Mahakama, ninafikiria utaratibu unaotumika hawa wanatiliwa pesa kwa muda wanatiliwa kila mwezi. Lakini ninajua katika Ofisi ya *CAG* wanatiliwa fedha kila miezi mitatu na Mahakama ni pahala muhimu sana. Ni kwa nini hawa wasifanyiwe utaratibu kama wanaofanyiwa *CAG*. Ningependa kujua.

Pia pembeni hapa ya Mahakama ya Kazi kuna ile Mahakama ya Kazi ambayo ni *Industry Court*. Ule mjengo ni zaidi ya miaka ninafikiri sijui saba au nane

yaani mpaka mimi ninaanza kusahau lile jengo ni kwa ajili gani limeekwa pale. Ni kwa nini mpaka lile jengo bado limekaa vile na *Industry Court* inahitajika. Kwa vile sisi sasa tunakwenda mbele kwenye masuala ya biashara. Tumesema tunataka utalii, biashara na huduma. Makesi yatakuja mengi ya biashara. Sasa lazima tutahitaji huduma kama zile.

Ningependa pia kujua kwa upande mmoja. Sisi hapa tuna *Chief Justice* wetu, tuna Spika wetu na tuna Rais wetu na hii ni mihimili mitatu. Lakini nikimuona *Chief Justice* wetu, yule ninamuona anatembea peke yake. Mbona hana ulinzi ulinzi ambao ni stahiki yake anatakiwa apewe kama ni muhimili wa tatu. Lakini pia nikipita maeneo tofauti ninajua hapa ni Ikulu anakaa Rais wangu, hapa ni nyumba ya Spika. Lakini ningependa huyu *Chief Justice* anakaa wapi na nyumba yake analipiwa na serikali au kajengewa. Kwa nini kama hana basi utaratibu usifanyike ili na yeye akastahiki kwa heshima yake. Maana yake ukenda Tanzania Bara kwa wenzetu, Kenya na Uganda hawa watu ni watu muhimu na wana heshima kubwa sana. Kwa hivyo ningependa kujua suala hilo.

Kwenye Mahakama ya Rufaa. Ninajua kule sasa hivi kuna Majaji kumi na sita. Katika Majaji kumi na sita, Mzanzibari ni mmoja tu basi, naye Jaji Mbarouk. Ni mmoja kati ya kumi na sita. Ningependa nijue ni sababu gani ambazo zinasababisha hadi leo sisi tunakuwa na mtu mmoja kwenye *Court of Appeal*, wakati huku tayari kuna vijana wengi wamesomesha sheria na Katiba na wanakuja juu. Tunasema wanataka ajira na wengine wapate kwenda zao huko. Basi ningependa kujua, mimi ningependa kuona wawe watano. Lakini ningependa kufahamu ni sababu gani zinazosababisha tukawa na mtu mmoja kwenye *Court of Appeal.*

Halikadhalika suala *e-government* ningependa kujua. Nimekuwa ninalitafuta muda mrefu, ninataka kujua hii *e-government.* Ninajua Rais wangu alizindua, ninajua tulikopa pesa zaidi ya Dola milioni kumi na nane. Nimemuona katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango amesema kuna mpango wa pili. Ninataka kufahamu kwenye suala la *e-government*, pesa za wananchi tumefaidika vipi serikalini ni hatua gani zimechukuliwa. Ni mambo gani yanayofanyika na katika mpango wa pili huo wa *e-government* ni kipi kitakachofaidika. Ninarudia tena ninataka nijue suala la *e-government*, pesa za wananchi, utaratibu wake uliofanyika juzi, mradi mzima wa *e-government* tuzungumze kwa kina ili nielewe na sisi kama Wajumbe hapa tupate kufahamu vizuri hii *e-government* tumefaidika vipi. (*Makofi*)

Ninataka nigusie katika kazi ambazo hii Wizara inasimamia. Nimeoina huku kwenye ukurasa wa mwanzo kuwa moja pia utekelezaji wa Katiba ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia kuna suala zima ambalo ningependa kufahamu juu ya hizi sheria ambazo zipo zinazosimamiwa na hii Wizara ni nyeti kabisa. Ni suala la *deep sea fishing*, uvuvi katika bahari kuu. Ni kwa nini hadi leo sisi hatufaidiki na hii bahari kuu, tunakosa pesa, tunakosa pesa kwa ajili ya vijana wetu na sheria hii kama zipo, basi kama nitakuwa ninakosea Mhe. Waziri ninajua unaniangalia, lakini ninataka kujua faida yake.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kufahamu katika suala zima la utekelezaji wake wa deep sea fishing unakwendaje. Sambamba na hili kuna watu wawili wanaona ni watumishi wa umma na mara nyingi huwa wananitia kinyongo sana ni wale ambao wanafuatana na Mhe. Rais, wapiga picha wale. Huwa ninamuona yule jamaa jina lake limenitoka anapanda vespa. Mpiga picha wa Rais utamkuta anahangaika hatulii anapanda vespa. Wakati ukenda Tanzania Bara unamkuta Field Maro, Kengele, Muhidin Issa Michuzi wamependeza. Mpiga picha wetu amechoka. Kwa nini huyu stahiki zake anaangaliwa vipi, pamoja na yule anachukua *still picture* pamoja na yule anayechukua za *motion*. Hawa wote wanafaidika vipi ni watumishi muhimu ambao wanaandaa kumbukumbu za Rais. Baada ya miaka wapiga picha anakwenda nao kila pahala ni lazima watunzwe, wabembelezwe stahiki zao. Hawa ningependa kufahamu wanaangalia vipi hasa katika maeneo pia katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais watu hawa ni muhimu. Ningependa kuelewa hawa na katika sehemu nyengine ambao watu wenye sura mfanano wafanyakazi wa aina kama hawa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo machache ningependa nizungumze kidogo kwa undani suala la *CAG*. *CAG* amekuwa anafanya kazi ya kwenda kukagua taasisi za serikali. Amekwenda *ZRB*, *SUZA*, Bandari, amekwenda kote huko kwenye taasisi ambazo zile zinasimamia mapato kuweza kukusanya. Lakini katika ukaguzi wake huyu *CAG* amekuwa anapeleka anawa-*charge* fedha nyingi kabisa, mamilioni ya pesa lakini mapesa yale ambayo *CAG* anatakiwa alipwe kutokana na ukaguzi, zile taasisi hawajazipanga katika bajeti yao ya mwaka husika. Barua inakuja kwamba inatakiwa ile taasisi alipe zile fedha, akaguliwe lakini pia kuna fedha tozo inakwenda kwake kama *CAG*, ili kujenga *capacity building* ya wafanyakazi wake.

Ninataka kujua ni kwa nini hii Ofisi ya *CAG* haiajiri wafanyakazi ili kutafuta *consultant* kuweza kuwafundisha ili tuweze kuokoa haya mapesa. Taasisi kama *ZRB*, leo Wajumbe wa Baraza wakija kujua fedha zilizotumika *CAG* kulipwa wanaweza wakalia machozi hapa ya madamu kuona hizo ambazo tumezitumia.

Ninataka kujua jumla ya fedha ni kiasi gani *CAG* kapokea kwenye taasisi na katika zile matumizi yake ameyafanya, nijuulishe shilingi moja baada ya moja, ya pili na ya tatu na nini kazifanyia. Na zile pesa ambazo zimekwenda kwa *CAG* amezitumiaje yeye. Ninataka nielewe kwa undani kabisa. Kama sijui semina, tunataka kujua semina kafaidika semina vipi na hizo pesa, kama katafuta safari za nje, tunataka tunajua kwa nini kazitumia hizo pesa. (*Makofi*)

Baada ya hapo mimi mchango wangu mdogo. Ninashukuru sana Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona mimi. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja masuala yangu yote nijibiwe vizuri au kwa hiyo tutakuja hapa tutabanana hapa hapa leo.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Ninaunga hoja asimilia mia juu ya mia lakini kwa sababu masuala yangu yapate majibu.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said. Waheshimiwa Wajumbe tumebakisha wachangiaji kama kumi na tatu kwa muda wa jioni. Kwa hivyo ninawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kujipanga vizuri ili kwamba wale ambao nimekusudia kuyatoa yaweze kuchangia.

Kwa hivyo ninawaomba sana mujipange vizuri katika wale ambao wanataka kuchangia, ili waweze kuzitumia zile dakika kumi na tano ambazo hapa tulikubaliana. Hilo la kwanza.

Pia naomba niwataje wale ambao wa mwanzo ili wafike mapema kwa ajili ya kuanza kuchngia. Mchangiaji hao kwanza atakuwa ni Mhe. Miraji Khamis Mussa, mchangiaji wa pili atakuwa ni Mhe. Hassan Khamis, mchangiaji wetu wa tatu ni Mhe. Abdalla Ali na mchangiaji wa nne atakuwa ni Mhe. Hidaya Ali Makame. Kwa hivyo ningewaomba sana hawa wafike mapema kwa ajili ya kuweza kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuahirisha Baraza naomba nitoe tangazo. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunatangaziwa kuwa kesho tarehe 02/05/2016 kutakuwa na zoezi la upigaji wa picha kwa ajili ya kutayarisha *post card* kwa Wajumbe wote ambao hawaridhika na picha ambazo walipiga kwa madhumuni hayo. Zoezi hilo litaanza kuanzia saa nne na nusu asubuhi katika Chumba cha *Reading Room*. Tunasisitizwa ni muhimu kupiga picha hizo ili kuweza kufanikisha zoezi hilo.

Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa michango yenu pamoja na utulivu. Naahirisha kikao hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:51mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kuna wachangiaji 13 na niliwataja majina hapa, lakini kwa bahati mbaya wengine siwaoni nilisema kwamba wataanza wao. Sasa Mhe. Abdalla Ali Kombo yupo, Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, mimi bado najitayarisha kidogo, naomba mchangiaji mwengine aendelee tafadhali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kupata wasaa huu kuja kuchangia hotuba hii ya Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Mwalimu Haroun, kwa kweli tunapozungumza Mhe. Naibu Spika, suala zima la Utawala Bora basi wizara ndio hii, yeye pamoja na Naibu wake Mhe. Khamis Juma Mwalim, kwa kweli kwa kuanza vizuri sana na hiki kitabu tu sura yake kinaonesha kweli ni kitabu cha utawala bora. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza utawala bora kuna mambo yake ya msingi na yale mambo ya msingi yote yamo katika wizara hii ya Maalim Haroun, wizara hii kama nilivyosema ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora yote yamo humu. Nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuliona hili na akazimegua zile taasisi nyengine zote akaziweka pamoja.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia utawala bora, misingi yake tunazungumza; Kwanza suala zima la uwajibikaji, yaani *accountability*. Pili tunazungumzia suala zima la uwazi, yaani *transparent*. Tatu, tunazungumzia suala la ushirikishwaji yaani *participatory*, maamuzi yetu, utendaji wetu uwe

utendaji shirikishi, utendaji wa uwazi, utendaji wa kuwajibika, ujuwe kuwa unawajibika kwa taifa hili. Nne, Mhe. Naibu Spika, ni kudhibiti rushwa na vitendo vyote vya kuhujumu uchumi. Tano, Mhe. Naibu Spika, ni kuleta ufanisi na tija, yaani *effectiveness and efficient* katika utendaji wetu na utawala bora ni lazima tulenge kupata *efficiency* kwenye serikali, hilo ni jambo la msingi sana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile jambo la mwisho ambalo ni muhimu sana, ni kuzingatia matokeo ya wananchi, yaani *responsiveness to the people's needs.* Wananchi wanatarajia nini kwenye serikali yao, wanatarajia utendaji mwema, uliowajibika na ulio wazi. Ndio maana Mhe. Rais akasema serikali yetu tusiogope kuwa-*face* waandishi wa habari, tueleze mafanikio yetu, tueleze matatizo yetu, kila baada ya muda tuwaambie tutamke. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. Rais kwa kutuongoza vizuri kwenye masuala mazima ya utawala bora.

Sasa kumeundwa vyombo kama hii taasisi ama mamlaka ya kuzuia rushwa na udhibiti wa uchumi, ofisi ya *CAG* hiyo, juzi tu hapa kumeundwa tume ya maadili, hivi ni vyombo au taasisi ya kusimamia masuala mazima ya utawala bora. Sasa Mhe. Naibu Spika, *point* kubwa nataka kueleza kwa nini nimeanzia huko. Kuna vyombo kati ya hivi havifanyi kazi ipasavyo na tunarudisha nyuma ile dhana nzima ya utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie suala la mahakama; mahakama imekuwa inapigiwa kelele muda mwingi juu ya utendaji wake na ukiangalia Mhe. Naibu Spika, kwenye kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 55 mpaka 56, hasa 55 pale pana orodha za kesi, ufunguaji wa kesi mahakamani kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano kwenye Mahakama Kuu ya Vuga, jumla ya kesi zilizofunguliwa ni 150, kwa upande wa madai ni 32, lakini kesi iliyotolewa uamuzi ni moja tu kati ya kesi 32. Tuje tena katika hizo kesi 150 zilizofunguliwa za jinai ni 6, hakuna iliyotolewa uamuzi. Twende tena upande wa rufaa, kesi zilizofunguliwa ni 87, zilizotolewa uamuzi ni kesi 13. Mhe. Naibu Spika, tunakwenda wapi, kwa nini kesi zicheleweshwe hivyo zisitolewe uamuzi, na hicho ndicho kilio kikubwa cha wananchi wetu, panda shuka mahakamani panda shuka, ile misingi ya utawala bora haki haitendewi, haki haipo.

Mhe. Naibu Spika, hili jadweli ningemuomba sana Mhe Waziri najua yeye mwenyewe anaijua vilivyo, lakini ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe liangalieni sana hili jadweli kwa kweli utavunjika moyo.

Nije mfano wa Mahakama ya Mwanakwerekwe, ukurasa wa 56. Kesi zilizofunguliwa ni 151,000 na kwa upande wa madai zilizofunguliwa ni kesi 19 tu, zilizotolewa uamuzi ni kesi mbili kati ya 19. Kwa upande wa jinai, kesi zilizofunguliwa ni 132,000 na kesi zilizotolewa uamuzi ni 879.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio *trend*, sasa utawala bora uko wapi na sisi tunatarajia chombo hiki cha mahakama kiwe ndio *model* ya utawala bora, wawe wao ndio wako mstari wa mbele kutuonesha haki iko wapi, haki inapatikana vipi. Ndio maana wananchi wengi wame-*lose* ile imani yao, lazima tuseme ukweli kwa vyombo vyetu vya mahakama. Lakini *to the contrary* inafurahisha sana Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Mwera. Mfano, kesi zilizofunguliwa ni 227, zilizofunguliwa upande wa madai ni 8, lakini iliyotolewa uamuzi ni moja tu, upande wa jinai ni kesi 219 na zilizotolewa uamuzi ni 158, kidogo za wilaya angalau zinatia sura.

Sasa tujiulize kwa nini wilayani wana- *perform* vizuri *unlike* huku Vuga kwenye Mahakama Kuu kuna nini, kulikoni. Ningemuomba Mhe. Waziri hili alitafutie dawa afanye utafiti, ashirikiane na Mhe. Jaji Mkuu na Mwanasheria Mkuu, kidogo turudishe imani kwa watu wetu wamevunjika moyo sana na Mahakama Kuu hasa Vuga pale.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia upande huu wa utawala bora kwenye ukurasa wa 37, Mhe. Mwanasheria Mkuu pale katika ukurasa wa 39, anasema ofisi yake inatoa muongozo wa mikataba ya serikali na kuiwakilisha serikali mahakamani kwenye kesi za madai. Nampongeza sana mheshimiwa, kuna kesi nzito za nchi hii kuitetea na tumefanya vizuri tunatetea. Kuna jamaa wengi tu wanagubika kesi wanataka madai waitobowe serikali lakini hawafanikiwi, tunamshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kulisimamia hilo.

Pia ajabu kuna kesi nyengine za haya madai, serikali ikishtakiwa pale basi zile kesi ambazo serikali inashinda ni chache mno, kuna tatizo gani kwa mawakili wetu. Suala hili ningemuomba Mhe. Waziri alitizame, kuna baadhi ya mawakili kidogo hawatufanyii haki. Kuna kesi nyingi ndogo ndogo za ndani ndani, zile za kimataifa tunafanya vizuri, lakini hizi ndogo ndogo siku zote tunakuwa *defeated* kwa nini. Ningemuomba sana Mhe. Mwanasheria suala hili alitizame.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye upande wa Tume ya Kurekebisha Sheria. Kwa kweli niipongeze sana tume hii kwa kazi ambayo inatarajiwa izifanye. Kweli sheria zetu nyingi zimepitwa na wakati kwa kushirikiana na wizara mama, lazima waziri a-re*view* ili tuwe *update* na hali ya mabadiliko ya maisha. Lakini naona ile *speed* yao ni ndogo mno. Kwa hivyo, mimi ningemuomba tu Mhe.

Waziri aje atujulishe tu tokea kuanzishwa tume hii ni sheria ngapi zimekuwa *reviewed* na katika hizo zilizopitiwa ni ngapi zimesharekebishwa na zimeanza kutumika, ili utupe moyo na sisi tuzidi kwenda nayo sambamba itusaidie.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa makusanyo ya mapato ukurasa wa 53. Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kufurahisha kwamba upande wa Ofisi ya Mahakama hapa kwenye mapato kidogo imepindukia lengo, mwaka 2015/2016 lengo lilikuwa 150 milioni, wamekusanya 176,507,000/- asilimia 118, hiyo inatia moyo kidogo kwa upande wa mapato *Alhamdulillah* wanajitahidi. Lakini upande wa makadirio kosa dogo tu pale kwenye ukurasa wa 53 ya makadirio sio mwaka 2015/2016 tena, makadirio iwe mwaka 2016/2017 naomba turekebishe tu lile kosa.

Inatia moyo na ningeomba wakaze kamba hivyo hivyo. Lakini najiuliza kwa nini Ofisi ya *DPP* nayo kuna ma- *blank*, Ofisi ya CAG nayo kuna ma-*blank*, kwa nini haikutiwa na wao wana kodi wanakusanya mapato mazuri tu kwa kazi wanazozifanyia taasisi, kwa nini kuna ma- *blank* hapa au hazikupatikana *figures*. Basi utakapokuja kujumuisha Mhe. Waziri ningeomba kidogo utowe ufafanuzi, Ofisi ya Mdhabiti na Mkaguzi wanafanya vizuri wanakagua taasisi mbali mbali na wanalipwa vizuri sana na inachangia katika mapato ya serikali. Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri hili uje ulitizame ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla nimalizie kwa kusema kwamba katika wizara hii kwa kukusanya taasisi hizi za sheria, katiba ukiondoa utumishi wa umma na utawala bora, kwa kweli hii niseme ni *instrument* yetu kubwa kuionesha nchi kwamba na sisi tunafuata misingi ya utawala bora na iko wazi kabisa. Hivi leo hakuna mfungwa hata mmoja wa kisiasa aliyeko ndani ambaye hajafikishwa mahakamani, hiyo ni sifa sana ukilinganisha na nchi nyengine. Kama mfungwa wa kisiasa au mtu wa kisiasa akiwekwa leo basi kesho anafikishwa mahakamani, tofauti na nchi nyengine. Kwa kweli hilo ni suala la msingi tunahitaji kuipongeza serikali yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini naomba sana suala lile zima la mahakama yetu pale Kiinuamiguu *rumandees* ni wengi zaidi kuliko wale waliofungwa, kwa sababu kesi haziendi Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili alitafutie dawa katika kuendeleza ile sera yetu ya utawala bora kama ulivyo muono ule wa Mhe. Rais kwa mtizamo wake utawala bora uwe vipi katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nilisimama kuchukua nafasi za ambao tuliwatarajia waseme, kwa hivyo na mimi hivyo hivyo nilisimama kuokoa jahazi naunga

mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia kwa mada hii ya Mhe. Waziri nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mwinyihaji Makame, sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, na baada ya hapo atachangia Mhe. Abdalla Ali Kombo, halafu Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeniwezesha kusimama hapa, huu sio uwezo wangu, wala akili yangu wala maarifa yangu, ni neema yake Mwenyezi Mungu aliniazima pumzi zake hizi wala sijui wakati gani atazihitaji, hii ni neema kubwa ya kusema *Alhamdulillah*.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa safarini na nilifukuzia hasa bajeti ya wizara hii. Natanguliza kwamba sitoiunga mkono nisije nikasahau, nina sababu zangu za muhimu. Natanguliza tena sitoiunga mkono bajeti hii mkono wala mguu na nina sababu zangu, nimeifukuzia hii na Mwenyezi Mungu namshukuru kwa kuniwezesha kufika hapa, nilikuwa Dodoma na nimefika hapa muda huu.

Mhe. Naibu Spika, muhimili mkubwa katika nchi hii ni mahakama ndio chombo muhimu, lakini kwa bajeti iliyotengewa hii hatuwatendei haki mahakama. Siku zote Waheshimiwa Wawakilishi tunapiga kelele kuwalaumu mahakimu na majaji wanaonewa, watafanyaje kazi bila ya kuwa na uwezo. Bajeti ya mwaka jana pesa walizoingiziwa na ya bajeti hii imepunguzwa, mahakama ni muhimili mmoja mkubwa sana.

Kwa hapa nitahitaji maelezo ya kina, na hizo pesa zilizoombwa zimepunguzwa, mwaka jana ukiangalia ni 1.3 bilioni zimeingizwa sijui sijui kama asilimia 30 au 50 na mwaka huu zimepunguzwa kesi zitakwenda vipi, tutawalaumu bure sisi watendaji wa mahakama. Mahakama ile ukienda sasa hivi wakati mwengine umeme unakatwa, tunapiga kelele waheshimiwa tunawalaumu mahakimu, majaji na wakati hawawezeshwi.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mahakama ya Mfenesini na Mahakama ya Mwera karibu miezi miwili au mitatu zimesimama zimeingia maji kesi zitakwenda wapi. Hawana uwezo hawa, mwaka jana wametiliwa pesa zikaingizwa katika meli, mwaka huu zimepunguzwa. Mhe. Naibu Spika, kitu hiki sio cha masihara hata kidogo, nitahitaji maelezo. Waongezeni pesa hii bajeti walioingiziwa ni ndogo, wakitaka kukosekana waingiziwe kama mwaka jana, mtoto anakua.

Ng'ombe bila kumlisha vizuri usitegemee kupata maziwa, mahakama ni muhimili mmoja mkubwa sana, kwa bajeti hii iongezwe, hiyo kompyuta hamna mule, ukienda mahakamani *proceed* zitapatikana wapi. Kwa suala hili nitahitaji maelezo ya kina kabisa. Leo inafika Mahakama Kuu umeme unakatwa kwa deni.

Jengine Mhe. Waziri, mashahidi wanadai pesa zao na ma-*assessor* ni lini mtawalipa pesa hizi, nitahitaji maelezo ya kina nayo. Mahakamani mashahidi sasa hivi hawaji kwenye kesi za ubakaji kuja kutoa ushahidi, wanapoteza muda wao, mashahidi walikuwa wakilipwa. Kwa hili nitahitaji maelezo ya kina, mashahidi na ma-*assessor* lini watapewa haki yao, hatuwezi kwenda namna hii kwa kuchezea mahakama, peza zinazoingizwa ni kidogo maendeleo yatapatikana wapi. Leo Mahakama ya Mfenesini na Mahakama ya Mwanakwerekwe zimejaa maji kesi zitakwenda wapi, wananchi hatuwafanyii haki, hatuwezi kwenda namna hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nije katika ajira. Niiombe sana wizara kwa heshima kabisa ifikirie walimu wa sayansi waliostaafu wapewe mikataba, sasa imefika wakati. Walimu wa sayansi waliomaliza muda wao waitwe waongezwe mikataba, hatuwezi kwenda namna hii. Mwaka jana nafikiri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilitaka kuajiri walimu 900, matokeo yake walimu 90 ndio walioajiriwa, watasoma wapi watoto namna hii, hatuwezi kwenda namna hii. Wizara ipange fomula walimu wa sayansi waliostaafu warudishwe tena ili kwenda kuokoa jahazi hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika Sehemu ya Utawala, kwa masikitiko makubwa sana kuna msikiti huu uliojengwa Mombasa wamepewa kibali watu na wamepewa kila kitu, lakini sijui mtu katoka wapi msikiti ule usijengwe, kisingizio misikiti mingi Unguja, akaa! Namna gani, ikiwa mingi si ndio neema. Msikiti Mombasa mtu kajitolea unataka kujengwa, Wizara ishakubali, anatoka mtu anakuja kuzuia, ndio utawala bora huu? Siku zote tatu tunasikia utawala bora, utawala bora kwenye redio, huu si utawala bora, bali ni maonevu. Nitahitaji kwa nini msikiti huo umezuiwa mpaka leo hautaki kuendelea kujengwa na nijue nani aliyezuia msikiti huu vile vile uko Mombasa. Anavyo vibali vyake hivyo na ameshalipa Halmashauri risiti hii hapa na *payslip* ya *PBZ* hii hapa, ukiitaka Mhe. Waziri au Naibu Waziri nitaileta. Msikiti unataka kujengwa nyumba ya Mungu unasema misikiti imeshakuwa mingi, nani anasema misikiti mingi si ndio neema yenyewe hiyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapa nije na suala jengine la utawala bora kuhusu barabara ya Mkunazini kwenda skuli, wanafunzi wanapata shida

kipande kidogo, Serikali sijui imefikiria kwa msingi gani njia ile kuifunga, kuna watoto walemavu wanataka kupelekwa skuli, kuna huduma za benki, kipande kidogo unakwenda kuifunga barabara ile, kwa misingi gani, inabidi huu mji wetu tunapangiwa na mtu yuko Ulaya anatupangia nchi yetu tuendeshe vipi. Niombe Serikali kama ndio utawala bora hili liangaliwe, kipande kidogo na watoto wanachelewa skuli, watoto ambao wanapelekwa wengine walemavu, ni kitu cha kusikitisha sana, kuna benki, misikiti na makanisa kipande kidogo Serikali mnakifunga, huo si utawala bora bali hayo ni maonevu.

Mhe. Naibu Spika, nije suala jengine la kuhusu mavazi, kuna nguo hivi sasa zinazovaliwa huko nje ya nchi au za kuvaliwa usiku zinavaliwa mchana, tukizingatia tuna mwezi wa Ramadhani mtukufu keshokutwa, Serikali ilete sheria kuhusu nguo na mavazi, si wanawake tu na wanaume, mwanaume unawakuta kavaa 'katabuno' mkanda uko chini huko chupi inaonekana. Mhe. Waziri na Naibu Waziri, mtuletee sheria ya mavazi, hatuwezi kwenda namna kama hii.

Nije na Mkurugenzi wa Mashitaka ya *DPP*, *DPP* kwa kweli nae hatendewi haki, inafika wakati umeme unazimwa ofisini kwake, wafanyakazi wake wanamkimbia, maslahi mabovu, itakuwa tunasomesha watu, tunasafisha njia wanachukuliwa. Dkt. Mwinyihaji Makame alizungumza hapa tutashinda kesi namna gani, hatuwezi kushinda, walikuwa wakikaa ma-*DPP* usiku, kesi za rufaa wakikaa siku mbili ndani utafikiri wanadurusu namna gani, lakini umeme hakuna watasoma wapi, kwa mishumaa? Mhe. Dkt. Mwinyihaji usitegemee kuwa kesi tunaweza kushinda kwa muda huu, kwa sababu uwezo ni mdogo, *DPP* haikidhi, tutakuwa tunamlaumu na tutaendelea kumalumu, mafuta kwenda Mahakamani gari hawana wategemee wapi watashinda kesi, hatuwezi kushinda.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo Serikali niombe tena kuna Mwezi Mtukufu wa Ramadhani habari ya kula ovyo Serikali itoe kauli yake, habari ya mavazi Serikali itoe kauli yake, tuangalie.

Halafu nije katika suala la elimu ya kur-ani, hapa niiombe Serikali ifikirie, unajua Mheshimiwa vyuo vya mjini angalau vina uwezo vinachangisha walimu wanaweza ku-*survive* na mambo mengine, lakini walimu wetu wa vyuoni mashamba hasa vijijini wana wakati mgumu kutoka wanafunzi mpaka walimu, Serikali angalau ilikuwa ifikirie namna gani ya kuwezesha vyuo vya kiislam, tuangalie na mustakbali wetu wa akhera uko je. Serikali hili jambo iliangalie *at least* namna gani vya kuwafikiria lakini maslahi ya watu wa shamba vyuoni walimu hayaridhishi hata kidogo, ni pesa ya sababuni tu ya kuwasaidia, kwa

shilingi elfu thalathini au Hamsini vyuo hivi nafikiri Serikali ina uwezo huo, Serikali mkono wake mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, nasema nahitaji maelezo ya kina kuhusu suala la Mahakama, Mahakama haziridhishi na pesa wanazotiliwa chuu! wasubiri tena, chuu! wasubiri tena, haziwezi kwenda, Mahakama ni muhimili mmoja mkubwa sana na pia niwashukuru sana wanafanyakazi kwa kujituma, wanafika mapema Mahakamani ukenda, mimi nisingeyaona baada ya kupelekwa Mahakamani ndio nikayaona haya mambo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nipate maelezo ya kina, *any way* Waziri aniridhishe niweze kupitisha bajeti hii, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ambayo umenipa, mimi nitajikita sana katika kitabu hichi kwenye mambo ya nyaraka, kwenye kitabu hiki kimeandikwa vizuri sana jinsi ya nyaraka zinavyohifadhiwa kwa madhumuni ya Serikali yetu na madhumuni ya wananchi wetu. Lakini kumbukumbu zangu zinaonyesha kwamba kulikuwa na mjadala mkubwa sana wa nyaraka ambazo zimeibiwa katika Ofisi yetu ya Kilimani, ingawaje kuna *electronic*, milango ya chuma na nini lakini ndio zimekwenda.

Sasa mimi ningeomba tu wakati Waziri atakapokuja hapa atueleze nyaraka zilizoibiwa na kuahidiwa zipo, yaani zimerejeshwa na kama hazijarejeshwa mpaka leo na Serikali kuahidi ziko wapi? Hilo ni suala ambalo litatusaidia sisi kama Baraza lakini litaisaidia Serikali ambayo inawahudumia wananchi, kwa sababu nyaraka ni za wananchi.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, inaonekana kuna watu hawajali, hawana habari na uchumi na vitu muhimu vya nchi yetu kuthubutu kiongozi ambaye anasifiwa kwenye utawala bora, kwenye utumishi kwenye nini katika nchi yetu viongozi kama hawa mtanisamehe lakini nafananisha na mdudu mmoja anaitwa 'dumuzi', kwa bahati nzuri nimesoma kilimo. Mhe. Spika, mdugu huyu anatafuna ncha za minazi, kwa maana hiyo mnazi unakuwa haupo tena, sasa mtu kama huyu au watu kama hawa ni kwamba baadae hatutakuwa na nchi na vizazi vinavyokuja vitatulaumu sisi, kwa maana hiyo kama watu hawa hawajarejesha nyaraka zetu hizi. Mhe. Naibu Spika, kupitia kwako naomba Serikali kupitia Wizara itujuulishe nani ni mwizi na asitangazwe kwenye Baraza bali atangazwe kwenye vyombo vyetu vya habari ili wananchi wajue kwamba huyu ndie mwizi wa mali zetu.

Mhe. Naibu Spika, ikiwezekana sheria ichukue mkondo wake na si mkondo wa maneno, Serikali ya Muungano ambayo wengine wengi hapa tumepiga kura zetu kumpa Mhe. Rais John Pombe Magufuli amethubutu Mhe. Spika, kuwafukuza viongozi ambao wezi, viongozi ambao hawafai na kuna viongozi sasa hivi wanatumikia Taifa kwa kufagia *dispensary*. Kwa hivyo, naiomba Serikali kupitia Wizara hii tusione haya kuwapa adabu watu ambao hawastahiki kukaa na jamii.

Mhe. Naibu Spika, wakati Mzee Karume anatafuta uhuru kuna watu walikuwa wakitumia sana maneno na kujionyesha kwamba wao wana nguvu na walikuwa wakijiita 'Sharif', kila kitu Sharif, Sharif anachukua, Sharif, Sharif anachukua, sisi wenyewe Wanamapinduzi tunashindwa kuwahoji, sasa isijekuwa Sharifu wenyewe ndio hawa. Mlango ni wa *electronic* lakini tumeshindwa na Wanamapinduzi waliopindua nchi hii wanaotumia milango ya makuti kwa kamba hakuna kifaa kilichoibiwa. Kwa hivyo, Mheshimiwa, narejea tena Waziri akija hapa atueleze na lini sio atueleze tu, maana matatizo yetu huwa tunaelezana tu nitachukua hatu, nitachukua hatua, tuambiwe ni watu gani, lini zitarejeshwa na kama hazikurejeshwa Waziri atujuulishe tufanye nini.

Mhe. Spika, kwenye mkutano wa mchakato wa Bunge Maalum la Katiba UKAWA walidai hati ya Muungano, hati ya Muungano ilitafutwa na Watanzania wakaonyeshwa, na sisi tunaomba nyaraka hizi ziletwe na watu waonyeshwe, kama hazikuletwa Mhe. Spika, sitakubaliana na kitabu hiki, kwa sababu mchezo sasa utakuwa tutaleta, tutaleta, tutafuatilia. La kwana hilo.

Mhe. Naibu Spika, la pili, miaka mitatu iliyopita Wizara hii hii kulikuwa na pesa za Zaka, sasa sina uhakika kama mfuko huu bado upo ama haupo, lakini Waziri akija atusaidie kama huu mfuko upo au haupo na je, kama haupo zile pesa ambazo zilikuwa mkopo zimerejeshwa na kama hazijarejeshwa kuna *action* gani ambayo imechukuliwa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwanza mimi natoa shukurani zangu za dhati kwa wote walioshiriki katika kuipanga hotuba hii ikapangika vizuri, natoa shukurani zangu za dhati sana, sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niseme mengi nina vipengele vyangu vitatu vya ndani ya hotuba hii, kwanza ni kuhusu masuala ya rushwa. Mhe. Naibu Spika, rushwa kusema ukweli Zanzibar sijui tuseme tunaona kama ni

chai, maana asubuhi, mchana, jioni, usiku, hili suala la rushwa hili imekuwa ni vikwazo sana kwetu sie, ukipita humo mabarabarani unakuta polisi anafumbatiwa mkono na dereva hivi, wale ndio wanaosababisha rushwa kusema kweli, gari lina makosa, dereva hana leseni, gari halina bima, lakini arimradi kusema kweli rushwa isiondoke, ana hiari apewe shilingi elfu moja lakini asimkamate yule kumpeleka polisi na kwenda kuhukumiwa kwa makosa aliyonayo.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri, kwenye kitengo hichi cha rushwa ahakikishe vizuri sana kwamba suala hili linakomeshwa kwa sababu hawa hawa wafanyakazi kwenye kitengo hicho cha kuzuia rushwa sifikirii kama wote wana magari yao wanaokwenda ofisini, wengine wanaingia kwenye magari haya haya ya daladala na wanayakuta yale. Lakini nimuombe Mhe. Waziri hapa anipe majibu kwamba ni polisi wangapi wa *traffic* waliofikishwa Mahakamani kwa habari ya kuchukua rushwa zile shilingi elfu moja moja wanazopewa mule na madereva.

Jengine ni kuhusu suala la utumishi Serikalini. Mhe. Naibu Spika, suala la utumishi hususan kwenye masuala yale ya ajira, Zanzibar hutangazwa nafasi hizi za ajira, Pemba siku nyengine hutangazwa nafasi tatu lakini hushangaa kwamba hutoka watu hapa Unguja wakenda kule Pemba kuchukua nafasi zile za ajira hata kama ni za kulinda, sasa mie huwa najiuliza kule kweli Pemba hakuna vijana wanaoweza kulinda Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa mpaka atoke mtu Unguja, huwa napata kekefu hapa kusema la ukweli. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili aliangalie sana na huko huko kwenye masuala ya ajira kuna watu wanakuwa kama mtu wa wake; zikitoka nafasi hizi za ajiira mtu ana watu wake kumi, ahakikishe mwanawe, mjukuu wake, mkwewe, shangazi yake wote kawachukua kawaajiri kwa kupitia nafasi ile ile.

Kwa hivyo na hapa nimuombe Mhe. Waziri kwenye suala la kitengo cha ajira iwe makini sana, ikija nafasi ya Sulemani basi apewe Suleimani, ikija nafasi ya Shazume basi apewe Shazume, sio kwamba kwa kuwa mimi nimo kwenye ile tume nimchukue mtu wangu au shangazi yangu na ndugu yangu kumuweka pale hata kama zile sifa hana. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri na hili aliangalie sana katika wizara yake.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala la Mahakama, huko Mahakama Mhe. Jaku, amesema hapa kwamba bajeti haitoshi lakini kuna mengine kusema la ukweli si masuala yanayohitaji bajeti ni yale yale kwenye rushwa, kuna jirani yangu kule Ndagoni alikamatiwa n'ndu na mume wake kutaka kupigwa kesi iko

Mahakamani, kila siku akenda anatiwa kijunguni na kibiani, kijunguni na kibiani. Lile suala nikaliulizia kumbe kuna rushwa pale imeshapita.

Sasa wakati mwengine kusema la ukweli na Mahakama nayo iwe makini sana hata kama bajeti haitoshi lakini iangalie sana masuala haya ya kesi wasiwe kama mtu kuchukuliwa pale akawekwa muda wa miezi mitano, sita, kumi, miaka miwili kesi ile pale anadhalilishwa tu kwa kuwa aliyekwenda ana kitumbo ana pesa za karafuu, au ana pesa za madagaa akatoa pale kwa sababu yule mwenziwe hana kitu akadhalilishwa na hili nimuombe sana Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba linaondoka katika Mahakama.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, sitaki niseme mengi sana, mimi naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja na hamsini. Ahsante Mhe. Naibu Spika, (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii nikaweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, kwanza nampongeza sana kwa uteuzi wa wizara hii, lakini vile vile nampa pole sana kwa majukumu mazito aliyopewa, lakini namuahidi sisi tukiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambae na yeye pia ni Mwakilishi mwenzetu tena wa jimbo, tunaahidi tutamsaidia sana ili kuhakikisha kwamba yale mategemeo ya wananchi yanaweza kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, natanguliza kusema kwamba sitoiunga mkono bajeti hii mpaka nipewe maelezo ya kina na ya kuniridhisha ili niweze kumpa baraka zote Mhe. Waziri ili aende akatekeleze haya tunayoyahitaji.

Mhe. Naibu Spika, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna bahati kubwa sana kwa sababu sisi ni sehemu ya muhimili wa dola, nchi yetu au nchi zote za kidemokrasia zinaongozwa na mihimili kuna Serikali, Mahakama na Mabunge ambayo sisi tunajiita 'Baraza la Wawakilishi'. Lakini nilikuwa nataka kidogo Mhe. Waziri, kuna mambo hayaendi vizuri katika hii mihimili miwili; muhimili wa Baraza la Wawakilishi na Muhimili wa Mahakama. Sasa ili twende vizuri basi lazima tuhakikishe kwamba muhimili wa Mahakama na muhimili wa Baraza la Wawakilishi uwe unakwenda sambamba na muhimili wa serikali ili mambo yetu yawe sawia.

Mhe. Naibu Spika, serikali ndio inayoleta miswada ambayo jukumu la kuleta miswada kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa sheria ni kazi ya Baraza la

Wawakilishi. Sasa serikali tunawashukuru mnatusaidia kazi ya kutuletea miswada, lakini vile vile naiomba serikali na sisi tunapoleta miswada basi serikali iweze kuikubali vile vile. Nitaanza na suala la nyumbani Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, sisi ni wanachama wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, na ninaiomba sana Mhe. Naibu Spika, ofisi yako na salamu hizi umplekee Mhe. Spika, tunahitaji wajumbe hawa washiriki katika mikutano mbali mbali ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola ili wakajue haki zao na wajibu wao kama Wabunge wa Jumuiya ya Madola.

Mhe. Naibu Spika, kama hawakupata mafunzo haya na kama hawakushiriki katika mikutano hiyo, Mheshimiwa Waheshimiwa hawa watakuwa hawawezi kujua haki zao za msingi. Sasa nakuja katika hoja yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kama unakumbuka niliwahi kuleta mswada hapa Barazani na nikamuomba Mhe. Spika na aliniruhusu, lakini serikali iliniomba kwamba mswada ule wauchukue wao na watauleta ili Baraza la Wawakilishi liwe na sheria yake kama Kifungu cha 77 cha Katiba ya Zanzibar kilivyoitaka Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, ziko sheria nyingi zinatungwa, lakini Sheria ya Utumishi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi imeekewa nguvu ya kikatiba katika ibara hiyo, katika Kifungu hicho cha 77 cha Katiba ya Zanzibar na naomba wajumbe tumepewa tunzo ya kufanyia kazi, tumepewa Katiba na kanuni naomba muangalie Kifungu cha 77(4) ni namna gani kilivyotupa mamlaka Baraza la Wawakilishi kutunga Sheria ya Utumishi wa Baraza. Tena naomba bora nikinukuu ili kuweka *Hansard* sawa. Ibara ya 77 (4) inasema:-

"Baraza la Wawakilishi laweza kutunga sheria ya kuweka mfumo wa utawala na uendeshaji na mambo mengine yanayohusu Ofisi ya Baraza la Wawakilishi".

Inapozungumzwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ni Wawakilishi pamoja na watumishi wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, tumekaa vikao vingi na mswada ulitaka kuletwa, kwa sababu mswada tumeutengeneza sisi wenyewe tukawa hatukuridhika na yale ambayo yaliyoingizwa. Kwa sababu yale ambayo tuliyoyataka sisi, sio yale ambayo yaliyoingizwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri suala hili nililipigania nikalisimamia kidete na kwa bahati nzuri tukamuona mpaka na Mhe. Rais. Lakini kipindi kile tulipomuona Mhe. Rais katika hoja ya mswada huu kwa bahati kulikuwa kuna mabadiliko ya Wanasheria Wakuu. Yule Mwanasheria Mkuu wa mwanzo ambaye yeye ndiye tuliyekwenda nao katika mswada huu na tukafanya nae ziara, Wenyeviti wa Kamati za Baraza la Wawakilishi kwa bahati mbaya alikuwa ameshaondolewa. Kwa hiyo, ikawa Mwanasheria Mkuu wa sasa hivi ambaye kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu amemjaalia tena, amerejeshwa tena kama ni Mwanasheria wetu Mkuu, basi Mhe. Rais alitumia busara kubwa sana na mimi namshukuru sana. Akasema basi hebu nendeni kafanyeni utafiti na nikamwambia Mhe. Rais utafiti tumeshaufanya, akasema utafiti mlioufanya lakini kwa Mwanasheria Mkuu aliyepita, sasa nataka muende mukafanye utafiti na Mwanasheria Mkuu aliyekuwepo sasa hivi ili ikiletwa hiyo sheria yenu iwe tena haina matatizo.

Mhe. Naibu Spika, sasa naikumbusha ofisi yako lakini vile vile na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ambaye yeye ndiye anasimamia Katiba ya nchi hii. Tunaomba ziara ya mafunzo ya kujifunza katika Mabunge ya nchi mbali mbali ndani ya mwaka huu ili sheria hii Mhe. Naibu Spika, ikiwezekana katika kikao kinachokuja cha Oktoba au cha Januari au cha Februari basi sheria hii tuje tuisimike hapa Barazani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nataka nifanye *reference* na ndio maana nika-*quote* mikutano ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Mhe. Naibu Spika, kuna Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Madola ulifanyika Abuja Nigeria ulikuwa mwaka 2003 unaitwa *Latima House Principle*. Mhe. Naibu Spika, *document* hili ni kubwa sana kama ingelikuwa utaniruhusu nitumie zile dakika za kawaida ningelilisoma ili ikaonekana ni namna gani kuna uzito wa sheria hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, nitamsubiri Mhe. Waziri, atakapokuwa hakunikubalia hoja yangu wakati itakapokuwa tunapitisha vifungu ambapo kuna fungu nitalizuia, nitakuja kumsomea vifungu hivi ambapo katika huu mkutano wa Wakuu wa Nchi wametoa maazimio kwamba Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola yatakuwa *independent* katika kufanya shughuli zao tena mpaka katika masuala ya utawala wa fedha (*Financial Administration*).

Mhe. Naibu Spika, sisi leo mpaka hii leo bado Baraza la Wawakilishi katika kufanya shughuli zake bado linaekewa *ceiling* na serikali. Mhe. Naibu Spika, tulipendekeza na haya tuliyapata katika hizo ziara tulizofanya katika Mabunge mengine ya nchi nyengine. Katika kupanga bajeti kuu ya serikali, sio huu mfumo tunaoletewa sisi sasa hivi, sisi serikali inakaa halafu wanatuletea bajeti ambayo tayari imeshatengenezewa utaratibu kila kitu, hata nafasi ya kutia

mikono huna. Sasa Mhe. Naibu Spika, na kutokana na kwamba hatuna sheria yetu ya utawala wa Baraza ambapo sheria ile ingeliweza kuipa nguvu Baraza kuweza kuajiri wataalamu waliobobea wa uchumi na sheria ili wakaweza kukaa pamoja na wachumi wa serikali kuangalia keki ya taifa ikagawanywa katika mgawanyo gani.

Tena kwa bahati nzuri Mhe. Naibu Spika, katika ziara hizo nakumbuka kuna ziara moja tulimchukua Mhe. Waziri Maalum Haroun ambaye sasa hivi ni Waziri wa Katiba na Utawala Bora, kama kumbukumbu yangu iko sahihi. Na katika kila ziara Mhe. Naibu Spika, tuliwachukua mawaziri ili ile hoja yetu inapokwenda kwenye *Cabinet* waweze kuipa baraka zote, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo sheria ile imekwama. Lakini ninaamini kwa umahiri na usikivu wa Maalim Haroun Waziri wa Katiba na Sheria, basi atakuwa msikivu na hii sheria yetu tunategemea itaweza kuja Barazani na kuja kwenyewe bado tutaomba tupewe nguvu ya kisheria, ili hii sheria tuilete sisi ili tuweze kupata matakwa ya Katiba. Mhe. Naibu Spika, nataka niondoke katika huu utawala wetu wa muhimili wa Baraza.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika muhimili wa pili wa Mahakama. Mhe. Jaku, amezungumza Mbunge wetu, amezungumza vizuri sana kuhusu Mahakama kutiliwa pesa chwiri, chwiri, chwiri. Mheshimiwa, huu sio utawala bora, hii mihimili mitatu inatakiwa kila mmoja uweze kufanya shughuli zake kwa utulivu. Mahakamani Mhe. Naibu Spika, ni pahala ambapo wanyonge wanakwenda kudai haki zao, wanyonge wameshasokotwa huko na wenye uwezo wao wanakwenda kudai haki zao. Ina maana leo kama Mahakimu au Mahakama zinatiliwa pesa chwiri, chwiri, kesi zinalala sijui hakuna ma-*assessors*, hakuna nani, hakuna nani, haki hizi zitapatikana wapi.

Mhe. Naibu Spika, kuna kesi sasa hivi zinafika karibu miaka 7, hasa kesi zinazohusiana na masuala ya ardhi, watu wameshachukua ardhi za watu, wamezikalia, wanyonge wanakwenda wanapiga danadana. Kwa hiyo, tutakapokaa tukisheshapitisha hii sheria yetu ya Baraza la Wawakilishi, kwa sababu kutakuwa kuna sheria ambayo ya utawala na utumishi wa Baraza la Wawakilishi sambamba na Sheria ya utumishi na utawala wa Mahakama. Wenzetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wako mbali sasa hivi, Mahakama ina mfuko wao, leo sisi mpaka leo tunasubiri *OC* chwiri, chwiri. Mimi nafikiri kidogo si utaratibu mzuri, lakini tukishapitisha sheria hii, sheria hii ambayo itakwenda sambamba na Sheria ya utumishi wa Mahakama nadhani Mhe. Naibu Spika, mambo yatakwenda sawia na mihimili hii itafanya kazi zake *parallel* wala haitokuwa na mgongano wa aina yoyote.

Lakini katika suala la Mahakama Mhe. Naibu Spika, niliwahi kulizungumza sana wakati alikuwa Waziri Mhe. Abubakar Khamis Bakary, kuhusu maslahi ya Mahakama za mwanzo. Mhe. Naibu Spika, leo Mahakama zote zenye kesi zote zinazohukumu kesi chini ya milioni 20 zinaanzia kule, lakini kesi za waiba kuku, sijui nani, wale wavutaji bangi, zote katika eneo ambalo lina kesi nyingi Mhe. Naibu Spika, ni eneo la Mahakama za Mwanzo.

Lakini leo Mhe. Naibu Spika, sitaki kusema kuna ubaguzi, lakini kuna jambo ambalo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hawatendewi haki, ukiangalia mishahara yao na wale wa Mahakama wa Wilaya pamoja na Mahakama ya Mikoa Mhe. Naibu Spika, ni aibu. Haikaribiani wala hailingani na nimeshawahi kuzuia fungu katika bajeti ya Waziri wa Katiba na Sheria kipindi kile Mhe. Abubakar Khamis Bakary, lakini kwa kuwa nilikuwa namjua Abubakar alikuwa na mambo yake, alikuwa na malengo yake nilijua kwamba atalivuruga lile lisiwe na kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu na yeye kamjaalia hapa hakurudi tena. Sasa ninaamini stahiki za Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo kupitia waziri mpya wa Katiba na Sheria, naamini zitapewa ufumbuzi wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kipindi kile Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria aliniahidi kwamba mishara yao wataishughulikia, lakini vile vile ataweza kuwalipa mpaka *arrears* zao. Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki nimpe mzigo mkubwa sana Mhe. Waziri wangu mpya, mwalimu wangu kwamba leo waje wawalipe Mahakimu wa Mahakama za mwanzo pamoja na *arrears* zao, hizo *arrears* mimi nawaomba wazisamehe lakini alau watengenezewe mishahara yao itakayolingana na ile kazi ambayo wanaifanya.

Mhe. Naibu Spika, Mahakimu hawa wakiwa leo wanalipwa vishahara vidogo vidogo tunawatengenezea utaratibu wa kupokea mishahara ya ziada kwa wale waliokuja kuwashughulikia kesi zao. Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo lazima tuhakikishe kwamba Mahakimu hawa wanalipwa stahili zao vizuri, tena sio mishahara tu mpaka posho zao. Mheshimiwa si uzuri kutaja mishahara ya watu na posho za watu, lakini Mhe. Waziri najua atakwenda kuangalia na naomba akakae na leo naomba Mhe. Naibu Spika, bajeti hii leo isipite.Waziri akakae na watu wake ili wayachambue haya tuliowaambia wakija hapa watupe jawabu zitakazostahiki. Kwa kweli itakuwa si vizuri kuning'inia tai ya mwalimu wangu hapa ili bajeti isipite, kwa kweli sitofurahi sana na ninaamini Maalim Haroun kama nilivyosema ni mtu ambaye msikivu ataweza kusikiliza hoja zetu hizi…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiza dakika tatu malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hizi dakika tumejiumiza sisi wenyewe na mimi kesho nitakuja na hoja ya kutengua tena yale maamuzi yaliyofanywa na Baraza kurejesha ile kanuni yetu ya mwanzo ili kuhakikisha tunapata dakika 20 za kusema na serikali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie, aah, nachagua sasa Ofisi ya Mufti. Mimi nakubaliana na Waheshimiwa waliozungumza kwamba tuandae utaratibu walimu wa madrasa waweze alau na wao kupatiwa posho ya sabuni. Na hili serikali inaweza na mimi namsifu sana Mhe. Haroun katika mtu ambaye kichwa chake kina upeo mkubwa wa mipango ni Waziri huyu wa Katiba na Sheria wa sasa hivi, na kama serikali yetu tuliweza kujenga hoja ya wazee wetu kuweza kulipwa posho ya shilingi 20,000, leo naamini na wazo hili tunalipeleka kwa Waziri wetu wa Katiba na Sheria aangalie utaratibu na *formula* ambayo tunawalipa wazee shilingi 20,000 kila mwezi alau sasa na walimu wetu wa madrasa nao wao tuweze kuwalipa alau posho.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana na ndio maana nikasema leo nitakuwa na buti nyingi. Mhe. Naibu Spika, kuna suala la Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa. Mheshimiwa, sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa iko wazi, sheria ishakiukwa lakini bado kuna vyama vinafumbiwa macho, nitazuia fungu la wizara hii mpaka tuhakikishe kwamba sheria tunazozitunga hapa zinafuatwa.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Maadili ya Viongozi, naomba tume hii ipewe nguvu, sijui kama Mwenyekiti kama keshateuliwa au vipi, naomba tume hii na hii nasema kwa sababu na mimi ni kiongozi, tume hii itakuja kurudi kuangalia maadili ya viongozi. Leo Mhe. Naibu Spika, mimi kipindi kile nilikwenda kufanya *research* mpaka Bungeni, kwenda Bungeni nikarudi kwa Tume ile ya pale Jamhuri ya Muungano. Mheshimiwa, tume ile iko vizuri sana, Mheshimiwa, wewe unaitwa unaambiwa tangaza mali zako. Leo Mheshimiwa, wengine sisi tuna mali hata wenyewe tushazisahau na hatuzijui, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma hii ndio sheria ambayo tumeshaipitisha, hii tume ipewe meno, nguvu na fedha ili sasa iweze kutu-*screen* sisi viongozi ili tuweze kuwa waadilifu wa viongozi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa Mahakama masuala ya ubakaji yamezidi na yamefurutu ada. Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia hamsini mpaka asilimia hamsini nitakapojibiwa masuala yangu na mengine nitayaleta kwa maandishi ambayo niliyokuwa sikuwahi kuyasema. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza na mimi nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa kuweza kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima kwa sote. La pili, niwashukuru vijana wote wa Mkoa wa Kaskazini kwa kunipatia nafasi ya kuweza na mimi kushiriki katika chombo hiki cha utungaji wa sheria. Pia, niwashukuru wazazi wangu wote, familia yangu nzima kwa kuweza kuniunga mkono na mimi nikaweza kuingia katika nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika mada kwanza nitaanza kwa kuwaunga mkono wenzangu wote waliochangia suala linalohusu walimu wa vyuo. Ningeomba sheria hii kama haipo basi ipitishwe na ifanyiwe kazi ili walimu hawa waweze kusaidiwa kwa sababu sitosema waweze kupata mshahara, kusaidiwa tu pia inatosha kwa kila mwezi ili nao wajihisi wamo katika jamii hii ambayo inawahusu katika hali zote.

Kwa sababu tukiangalia walimu wa vyuo tunawaangalia katika uwanja mfupi, lakini walimu wa vyuo ni watu ambao wanaielimisha jamii tangu mwanzo na mpaka mwisho. Kwa sababu kama mwanafunzi hatoanza chuo cha kur-ani basi kama utampeleka skuli moja kwa moja basi tufahamu kwamba upeo wake unakuwa ni mfupi, lakini kama ataanzia kule kwenye madrasa akaanza kujua (a) na (b) basi upeo wake unapanuka zaidi na unakuwa mkubwa na unakuwa na ufahamu mkubwa zaidi.

Vile vile, nitaangalia suala jengine kuhusu suala la *programme* za *technology*. Kwanza na mimi naomba hapa nichangie kwamba katika Sheria za *technology*, kwenye suala la miamala kimtandao zaidi. Hapa nitazungumzia kuhusu suala la mitandao zaidi, inaonekana kuna matatizo kwamba sheria hii katika Baraza letu sisi haijapitishwa. Kwa hiyo, ningeomba Mhe. Waziri na sisi atwambie kuhusu suala hili ni lini na sisi tutaweza kulifanyia kazi na likapitishwa kwenye Baraza letu la Wawakilishi kama wenzetu wa Bungeni wanavyolitumia suala hili la *technology*.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia naomba nimuulize swali Mhe. Waziri kuhusu hili suala la *technology* kuhusu usimamizi na uendeshaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Kaeleza katika ukurasa wa 12 wa hotuba yake kwamba hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016, yaani mwaka huu tulionao taasisi 53 za serikali zimeunganishwa na nyengine 11zinashajihishwa. Lakini Mhe. Waziri katika suala hili pia hajatutajia ni taasisi gani. Kwa hiyo, ningemuomba wakati

atakapokuja kututolea maelezo ya hotuba hii atueleze ni taasisi gani ambazo zinashajihishwa na zimesajiliwa kwenye hili.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye suala la utumishi wa serikali na programu hii, lengo la kusimamia ajira. Mhe. Waziri, ameeleza kwamba lengo la kusimamia ajira na maadili na haki za utawala wa sheria kwamba zipo, lakini ningeomba kuwa hawa watu wanaopatiwa ajira hususan walimu au madaktari wengi wao kwa sasa hivi tunaona wameshakuwa watu wazima na umri wao tayari unaanza kufikia muda wa kustaafu. Kwa hiyo, ningeomba kama mimi katika hotuba yake hii wakati atapopitisha alitizame suala hili zaidi kwa wale watu ambao wapo wameshasoma hizi nafasi ili na wao waweze kupatiwa hizo ajira. Kwa sababu tunaona kwamba wale walimu wengi wao hasa waliokuwa wanaendelea na kusomesha sasa hivi wengi wanataka kustaafu, hususan katika kipindi hiki cha mwaka 2016 hadi 2020 watakuwa wengi wameshastaafu, tukiangalia kwamba walimu hawa bado ajira ni ndogo haijakuwa kubwa kiasi hicho. Wapo ambao wameshaomba hizo ajira, lakini bado hawajaajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna walimu hawapungui 900 ambao wameomba ajira lakini mpaka sasa hivi kuna walimu 90 ambao ndio wamepata ajira. Kwa hivyo, naomba katika bajeti hii ya Mhe. Waziri aweze kuliona suala hili la walimu waongezewe pato zaidi ili waweze kuajiriwa watu wengi zaidi katika wizara yao. *(Makofi)*

Pia, niende katika suala la Hatimiliki. Kuhusu suala hili ukurasa wa 20 hotuba ya Mhe. Waziri, imesema kwamba serikali itaangalia zaidi suala la vijana katika kazi zao na ajira, ambapo katika vyombo vya habari labda nitasema suala hili. Vijana wanapokuwa katika pirika zao za ajira katika kufanya kazi zao labda tuseme wanamuziki, wanapoingia kule kwenye vyombo vya habari suala hili linawakwaza katika malipo, kazi wanazofanya ni kubwa lakini malipo yao unayakuta ni madogo. Kwa hiyo, ningeomba Mhe. Waziri, aliangalie pia vijana kwa kuwapa nguvu ili waweze kufanya hizi kazi. Kwa sababu tukisubiri ajira ya serikali tunaona kwamba hamna. Hivyo, endapo wanatokea vijana kujiajiri wenyewe basi tunaomba wapewe kipaumbele na waweze kuwezeshwa zaidi ili waweze kufanya kazi zao ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia na mimi napenda niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsane sana Mhe. Hidaya Ali Makame, nakupa hongera kwa mara ya kwanza umechangia, ndivyo tunavyokuwa sote hivyo tukichangia kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, nakupongeza sana kwa kweli. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa kuwemo kwenye orodha ya wachangiaji wa Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hii G06 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Yapo maoni mengi mimi na kamati yangu tulishauri asubuhi ya leo, lakini pia nikaona mengine nije niyaseme moja kwa moja kupitia nafasi hii ambayo umenipa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niendelee kuwapongeza wafanyakazi na viongozi wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kufanya kazi kwa bidii, kufanya kazi ya kuokoa sehemu kubwa ya upotevu wa fedha katika matumizi ya serikali. Pia, niwapongeze wanaishauri serikali kwa wakati lakini zipo changamoto nyingi ambazo wanakabiliana nazo, zimo tulizozisema na ni vyema nikaendelea kuzisema zile ambazo pengine ufafanuzi wake haukupatikana vizuri kwenye kamati yetu hii.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe waziri aiangalie kwa jicho la huruma ofisi hii hasa kulingana na majukumu yake, wana majukumu mazito wakati mwengine yale ya kawaida ambayo wameachiwa kwa mujibu wa utaratibu, pia hutokezea kuongezewa majukumu kwa *special audit* pale ambapo inatokezea. Lakini kawaida hata huko nyuma tulikuwa tunaona wanakagua ofisi zote za serikali, mashirika ya serikali, lakini sasa kuna miradi ya maendeleo ya majimbo imeongezeka.

Mhe. Naibu Spika, changamoto hasa wanayoipata wenzetu hawa ni eneo la wafanyakazi na stahiki zao. Tulipokuwa tunapitisha maoni ya kamati na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kumetokea changamoto hii tokea mwaka 2009, wao wameomba kuajiri hawajapata nafasi, lakini wapo wafanyakazi wengi wamestaafu, wapo waliofariki, lakini wapo waliohamishwa kikazi. Majukumu tunawaongezea lakini wakitoka kwa kustaafu au kwa kufariki hawaajiri na ni ofisi moja inayobeba roho kubwa sana ya serikali.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu mambo yote yako kwake, taasisi hii iko kwake, ajira ziko kwake, sasa sijui kwa nini anawanyima na majukumu kila siku serikali inawaongezea. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, aliangalie hili kwa sababu kama tokea mwaka 2009 hawajaajiri na karibu wafanyakazi 40 wamestaafu, nafasi zao kwa kila aliyetoka palikuwa na kazi pale wanafanya. Kwa hiyo, majukumu haya yataongezeka kwa wafanyakazi waliopo.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine iko kwenye maslahi yao, wanafanya kazi nzito, wanaisaidia sana serikali, maana watu wanatumia huko wewe unakwenda kuwa-*audit* na unapeleka ripoti ya kuishauri serikali ni jukumu kubwa, wanakabiliana na mengi sana. Kwa sababu kazi yao fitina, mtihani, basi pia mtihani ambao tumewatwika hawa mwisho wa siku hata maslahi tunawanyima! Si haki katika utumishi tunaoutoa ndani ya nchi yetu.

Leo wafanyakazi wa pale katika hizo *scheme* walizotengenezewa kupata kwake *around* shilingi 700,000 au 800,000, lakini wanakwenda kuwachunguza watu ambao wana *OC* moja tu. Kama hawa wahasibu utakuta kuna ma-*internal auditors* wanakaribia shilingi 2,000,000 katika mishahara yao, hawa wanaokwenda kukagua kwa *OC* zaidi ya sita tunakwenda kuwanyima haki zao za msingi. Mhe. Waziri, atakapokuja kwenye jambo hili kabla sijaungana na wenzangu katika kutia shilingi lazima nipate majibu mazuri ili tuone basi utumishi huu na stahiki zao zinakwenda sambamba na majukumu ambayo tumewapa.

Mhe. Naibu Spika, G09, Tume ya Utumishi Serikali. Katika programu zake za usimamizi kwa uajiri na haki na nidhamu za watumishi, Mheshimiwa, kwenye kitabu hiki waziri amesema moja ya kazi za kawaida ni kupandisha mishahara na kada za watumishi.

Mhe. Naibu Spika, hapa pana malalamiko mengi kwa taasisi nyingi. Nimpongeze sana Mhe. Hamza Hassan Juma, amewazungumza Mahakimu na akasema hataki yeye kutaja sehemu ya mishahara yao, lakini panapo shida ya kumtetea mtu unaweza ukasema maana angalau watu wajue zile tafauti zao. Leo hii Mahakimu wetu wa Mahakama za Mwanzo na Mahakimu wa Mahakama za Wilaya, kwanza utaratibu wake hauko vizuri, leo sheria iliyopo inataka waajiriwe Mahakimu wa Mahakama za mwanzo wawe na *certificate* lakini wako Mahakimu wana *master* wamebakia Mahakama za Mwanzo, wako Mahakimu wana *degree* wamebakia Mahakama za Mwanzo, lakini Mahakama za Wilaya unawakuta Mahakimu wana *diploma*, Mahakama za Mkoa vile vile. Lakini unawakuta Mahakimu wa Mkoa pia wana *diploma* na unapokwenda kwenye stahiki zao na wote kazi yao kuhukumu tunawaonea sana Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

Mimi nasema tunawaonea kwa sababu kesi hizi zikianza huku baadae ndio zinakwenda katika ngazi ya wilaya, ziko zinazoanza wilaya moja kwa moja, lakini mimi niseme Mhe. Waziri kwenye jambo hili kwa sababu mambo yote haya yako kwake. Mahakama ziko kwake, watumishi wako kwake na *schemes* zinabadilishwa kwake.Inakuwaje leo Hakimu mmoja anapewa posho la shilingi

250,000 na huyu wa juu yake kidogo anapewa karibu shilingi 1,300,000, kwa misingi ipi na kwa utaratibu upi? Nchi hii tutafika pahala hata hao wafanyakazi waishi kwa matabaka, maana tunawatia unyonge hata hao Mahakimu wenyewe wa Mahakama za Mwanzo. Hata posho zao zile ni tafauti; huyu unakuja kumpa shilingi 200,000 na kitu hivi, mmoja unampa shilingi 1,200,000 ni *gape* kubwa. *Schemes* hizi wakati mwengine sisi tunajiuliza hizi tume za utumishi huku zinafanya nini au tuzifute tutafute *consultant* mwengine wa kutushauri vizuri, hatuwatendei haki,tutakuja kutengeneza mambo mengi ndani ya nchi hii, lazima tuwatetee watu wetu, tuwatetee Mahakimu wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi namuomba waziri kwenye jambo hili aliangalie sana, nimejaribu kutaja tu *highlight*, mishahara hasa sijaitaja, maana ningeitaja hapa! Lakini *highlight* yenyewe na mpishano wenyewe mkubwa na kada zenyewe zinavyopangwa mpaka sasa hatutambui, maneno ya kwetu kule nisingependa kutumia kauli hiyo, "vurugu vyogo". Lakini ndio mfumo uliokuwepo hapa haueleweki. Sasa *schemes* hizi hata katika taasisi nyengine unamkuta mtu huku hana taaluma yoyote kaajiriwa mwanzo tu kuliko yule ambaye kaja hivi karibuni ambaye ana elimu kubwa. Inawezekana anafagia au dereva anampita Afisa Mipango wa ile taasisi, lazima *schemes* hizi zinapotengenezwa na namna ya kupandishwa kada watu wake Mhe. Waziri, waangalie vizuri. Mimi nimekuwa mtumishi kwa muda karibu miaka 15 nimeona haya na mimi yamenikuta, lakini siwezi nikazungumza moja kwa moja.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kulizungumza suala la upotevu wa nyaraka. Nyaraka hizi ni hazina ya nchi yetu, ni historia ya nchi yetu na ni utu wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, unazungumzia suala ambalo tayari limeshafanyiwa maamuzi ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 59(4), labda nikusomee inavyosema.

Kifungu cha 59(4) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi kinasema kwamba:

"Ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kusema jambo lolote ambalo langojea uamuzi wa Mahakama, au ambalo lilijadiliwa na Mkutano wowote uliopita na ambalo halikuletwa rasmi kwa ajili ya mjadala unaoendelea na vile vile ni marufuku kwa Mjumbe kusema kwa kutaka kupinga au vyenginevyo".

Kwa hiyo, naomba kama una mengine ya kuzungumza uendelee na hayo na hili usilirudie tena. Kwa sababu kuna Mhe. Mjumbe mwengine amelizungumza vile vile. Kwa hiyo, naomba kwa hili bado liko katika mikono ya serikali,

hivyo, sidhani kama ni busara kulizungumza tena ambalo limeshazungumzwa kwa kipindi kirefu sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikubaliane na wewe na nikubaliane na kanuni iliyopo na mimi katika michango yangu sikutaka kuliulizia, nilitaka kuzungumza maazimio kwa sababu mpaka leo hayajafanyiwa kazi. Lakini naomba niliache kwa sababu maazimio yapo na yamewekwa na Baraza hili na serikali ipo. Sasa kwenye mambo ya msingi kama haya basi mimi naomba niende moja kwa moja kwa sasa niunge mkopno hoja kwa asilimia 95%, nabakisha 5 kwa ufafanuzi wa mambo yangu. Mhe. Naibu Spika, naomba kukushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo. Lakini pia kwa kutoa *fatwa*, kwamba tusilizungumze suala la nyaraka kwa sababu limeshaletwa Barazani. Sitaki kulizungumza Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hili suala limeshaletwa Barazani lakini suala lenyewe ni kubwa, ni urithi wa wazee wetu ambao wametuachia.

Lakini nilitaka kujua hatua gani imechukuliwa kwa sababu ripoti ninayo hapa mbele yangu ya hilo suala la nyaraka na ukiangalia hii ripoti ukweli ni kwamba tuliambiwa sie halafu sie sie baada ya "donda na msumari wa moto".

Mhe. Naibu Spika, umetukataza suala hili tusiliongee lakini lazima suala hili kwa sababu wazee wetu walitupindulia nchi na pia walituachia urithi wa nchi na *documents*.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, unalijadili na tumesema lisijadiliwe, naona sasa unalijadili, naomba uendelee na mambo mengine.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa muongozo wako mzuri kwa vile umenikataza nisiliongee naenda mada nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kitabu hichi ukurasa wa 18 kinazungumzia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mhe. Naibu Spika, ninavyojua Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina mali nyingi sana na inafanya kazi nzuri naiomba niipongeze. Lakini Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kuna harufu kwamba zile mali ambazo watu waliziacha kama ni mali ya amana kuna watu ambao wameziiba na kuna watu ambao wanazitumia kwa maslahi yao binafsi ndani ya nchi hii.

Kwa hiyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kwanza atujuze Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina mali ngapi na ngapi bado zinatumiwa kinyume na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kusudio lake hasa kutokana na hiyo harufu ambayo ipo.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 14 kuna usimamizi wa masuala la dini. Napenda kuchukuwa fursa hii kwanza pia kupongeza, naomba kusoma hapa kidogo; "Lengo la programu hii ya kuratibu na kusimamia shughuli zinazohusu Afisi ya Mufti kwa kutoa *fat-wa* na kutoa miongozo kuhusu masuala ya dini". Kwa heshima kubwa Mhe. Naibu Spika, niipongeze Afisi ya Mufti kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya na waendelee kufanya. Lakini nawaomba sana wawasimamie baadhi ya watu ambao wanakiuka misingi ya uislamu kama qur-ani na suna sahihi zilivyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 20, kuna Chuo cha Utawala wa Umma, Chuo kizuri kinatupa taaluma nzuri kinafanya vizuri. Lakini kuna siku mimi nilibahatika kutembelea chuo hicho, kuna mambo nikayagunduwa nikawa sijayapenda. Namuomba Mhe. Waziri akipitie hicho chuo na ayarekebishe. Kwanza kuna uvivu na uzembe pale chuoni, uchelewaji umezidi sana pale chuoni mpaka saa nne unakwenda wahusika hawapo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie, lakini pia anijuilishe Mhe. Waziri, anapokuja kuna harufu ya utotevu wa pesa pale chuoni. Je, yeye anajua kwa kiasi gani na kama ipo hatua gani imechukuliwa au hatua gani zinategemea kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 22 kuna Mahakama. Hapa ni pahali pa kupata haki ya kila mtu dunia nzima. Lakini Mahakama za Zanzibar zimekuwa kinyume chake hasa watumishi wa mahakamani wengi wao si wote ni watu wanaopenda rushwa, kwa kupenda kwao rushwa kunatufanya tukose haki zetu. Mhe. Naibu Spika, kitendo hichi namuomba Mhe. Waziri na yeye pia akitupie macho ya rehema na akiangalie sana.

Lakini pia ningeomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri akija anijibu kesi ngapi za udhalilishaji wa watoto wadogo zipo mpaka hii leo na ngapi zimehukumiwa?

Mhe. Naibu Spika, ukitoka hapo nakwenda ukurusa wa 24, kuna Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mhe. Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa kamati ya Habari, Utalii, Utangazaji, lakini pia ni Mjumbe wa kamati ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Tulipokuwa tunazungumza na watendaji wa wizara walisema wanashindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wameshapeleka maombi ya kurekebishwa baadhi ya sheria hasa Sheria za uzalilishaji wa watoto lakini bado hazijafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atwambie hizi sheria zilizopelekwa ambazo zinahitaji marekebisho lini zitafanyiwa kazi ili hawa watu wanaoendelea kudhalilisha watoto nchi hii wapelekwe katika vyombo vya sheria na ikiwezekana wanyongwe.

Mhe. Naibu Spika, nchi hii ni Zanzibar na tegemeo langu wafanyakazi wote kama hawapati maslahi sawa sawa, lakini wapate maslahi yanayolingana hasa wakiwa ni watendaji wa serikali. Mhe. Naibu Spika, kuna Mashirika ya Serikali na kuna Wafanyakazi wa Serikali wa wizara. Kuna mashirika ile mishahara yake inakithiri ada utamkuta mfagiaji wa shirika anampita mtu mwenye *PhD* wa wizara, unamkuta dereva wa shirika anampita mtu mwenye *PhD* wa wizara.

Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri, wanatumia vigezo na viwango gani katika kupanga mishahara hii hasa ya mashirika na mawizara wakawaacha kama si wafanyakazi wa serikali na wote hawa ni watendaji wa serikali lazima kuwe na uwiano kwa mishahara. Kwa sababu kitendo hicho kinasababisha mambo mawili; kunasababisha sisi Zanzibar tunasomesha watu halafu watu wengi wanakimbia nchi kwa sababu ya mishahara midogo inayopatikana hasa kunako taasisi za serikali kwani mashirika wanapata mishahara mingi.

Mfano mzuri Mhe. Naibu Spika, Afisi ya *DPP*. Afisi ya *DPP* inapata mshahara mdogo na wataalamu wengi kutoka afisi ile wamekuwa wanakimbia na wanakimbilia Bara kutokana na mishahara midogo wanayolipwa ukizingatia kuna mashirika ambayo dereva anapata mshahara mkubwa kuliko mtendaji wa serikali ambao wote wanafanyakazi serikalini. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atwambie viwango gani vinatumika.

Kadhalika Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na sheria ipo sheria ya kuongezwa muda. Lakini sheria hii Mhe. Naibu Spika, ilikuwa ni ya zamani wakati huo msomi wa Zanzibar akifika kidato cha sita nchi nzima inajua kuwa huyu kidato cha sita. Lakini leo una *PhD* hapa Zanzibar hakutambui mtu kwa sababu watu wote wamekwenda skuli, ndio maana ikawekwa hii sheria ya kuongezwa muda. Lakini leo Mhe. Naibu Spika, na wakati huo watu walikuwa wengi kuliko vijana, lakini leo vijana wengi kuliko watu wengi, vijana ni asilimia 65 ya *population* ya dunia. Lakini unashangaa kuona mtu wala hana kada maalum anaengezwa kazi miaka miwili, akitoka miwili anaongezwa tena miwili kwa

kisingizio kwamba anasaidiwa eti hajajipanga. Ikiwa miaka 42 kafanyakazi hajajipanga kujipanga yake ni kaburi tu huyo hajipangi tena Mhe. Naibu Spika, ajipange kwa kaburi.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana sheria hii iletwe tuibadilishe ili vijana wapate fursa ya kufanyakazi, vijana ni wengi na ndio tunaowategemea, unamkuta mpaka mfagiaji anasaidiwa kuongezwa muda eti kwa sababu apate kujipanga miaka 42 hajajipanga tangu alikuwa miaka 19 kaingia kazini hawezi kujipanga. Kwa hivyo, Sheria hii imepitwa na wakati, tunaiomba iletwe tena, suala la kuengezwa muda lazima kwa mfano awe daktari au mtu fulani, dunia nzima ndivyo inavyofanya hatuwezi kuongeza muda kiholela, amemaliza akajipange kwa kufa ndicho kilichabakia, tena asiwanyime watu wengine fursa ya kufanya kazi. Mhe. Naibu Spika, kwa hili nalisemea kwa ukali, vijana wetu masikini ya Mungu wanashindwa kupata nafasi za kazi kwa sababu watu hawataki kuacha nafasi badala yake wanaengezwa muda kisingizio, najua sheria ipo, lakini sheria hii imepitwa na wakati.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Fedha Chwaka, kuna mwananchi wangu mmoja ameniletea malalamiko, anasema Chuo cha Fedha Chwaka watumishi wake bado mpaka leo wanaostahiki kwa mfano Wahasibu na wengine kuongezwa mishahara hawajaengezwa na wameshasema sana, na wao ni wananchi na wenzao wameshaengezwa, pia, wanafanyakazi mpaka saa nne ya usiku hadi tano hawalipwi muda wa saa za ziada. Kama mimi ndio mtumishi wao wa jimbo na walikuwa karibu 7 walikuja kwangu na mimi naliwasilisha hapa. Mhe. Waziri alichukuwe na alitizame.

Mhe. Naibu Spika, kadhalika kuna Tume ya kuzuia Rushwa. Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuja na wazo la kuanzisha Tume hii ya kuzuia Rushwa. Lakini mimi napata wasi wasi kidogo hii tume ipo, ina watendaji, wanalipwa mshahara, wanafanyakazi lakini huoni *outcome*. Sasa Mhe. Waziri, hebu anijibu au bado tunaoneana muhali na kubebana hapa Zanzibar, mimi naona wala rushwa wapo na wamo wengi lakini humsikii kufungwa wala kufanywa chochote, ukiendelea unamkuta pale pale. Anambie Mhe. Waziri kesi ngapi mpaka leo hii Tume ya kuzuia Rushwa wanazo na watu wangapi wameshachukuwa na kufungwa tangu tume hii imeanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, kunako suala la ajira hapa Zanzibar utashangaa, ukipita pale *Airport* kuna Muhindi ndie meneja wa kupika chai. Sasa najiuliza aah! mtu atoke India aje hapa kuwa Meneja tu kwa kufanya mambo ya kupika chai, hapa hakuna watu wanaoweza kufanya kazi ile. Tunakubali kuna sekta ambazo

hakuna wataalamu, lakini sifikirii kama hatuna mpaka wataalamu wanaoweza kusimamia kupata pesa za kupikwa chai.

Mhe. Naibu Spika, hii hatuwezi kuikubali lazima hili hili suala liangaliwe vizuri kwamba zile kada zote ambazo Mzanzibari anaweza kufanya aifanye Mzanzibari, mgeni iwe marufuku, *unless* iwe hawawezi kufanya, kada hizo zipo nyingi. Lakini unakuta Mzanzibari haajiriwi unapewa sababu hata si za msingi, sababu unaambiwa Wazanzibari wavivu, Wazanzibari wavivu wangezaa, uvivu huo umetokea wapi? Hii mimi naona ni makusudi inapangwa kwa sababu ya kuwakandamiza Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Waheshimiwa Wazanzibari, vijana ni wengi na hawana ajira na wanahitaji ajira, lazima tuletewe sheria kabisa inayowapa kipaumbele ajira vijana wetu, ndugu zetu wa Kizanzibari na sio mgeni nchi hii, lazima iwe mzalendo mwanzo, mgeni baadae.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, umenikataza nisiongee kuhusu nyaraka nimekubali. Lakini sijui nina uwezo gani kutumia kuhusu nyaraka hizi za Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, siungi mkono bajeti hii mpaka nijibiwe masuala yangu hayo nitaiunga mkono. Baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kinipatia fursa hii jioni hii ya leo nikaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambae ameniwezesha jioni hii kusimama mbele ya Baraza hili tukufu.

nhMhe. Naibu Spika, nianze na mchango wangu kwa kuanzia Tume ya Utumishi Serikalini. Mhe. Naibu Spika, Tume hii ya Utumishi Serikalini Waheshimiwa wengi wameigusia. Lakini kwa vile walionileta hapa ndani ya Baraza hili tukufu ni vijana na vijana wengi ndio wanaolalamika na Tume hii ya Utumishi Serikalini. Hakuna kikao hata kimoja ambacho kuwa utazungumza na vijana suala hili la Tume ya Utumishi serikalini wasiweze kuligusia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Tume hii ya Utumishi ina matatizo yake na tena mengi, kwa sababu huwa tunasikia kwenye vyombo vya habari zinatangazwa nafasi za ajira. Vijana wengi wanaomba nafasi zile za ajira lakini cha kusikitisha baada ya kushakutolewa tangazo lile la ajira kuwa Wizara fulani

inatangaza nafasi za ajira kada fulani na kada fulani. Lakini la kusikitisha na la kutia huzuni hawa wanaoajiriwa huwa hawaitwi hapa kwenye *interview*.

Vijana wetu wanabakia kwenye kulalamika siku hadi siku, matokeo yake tunaambiwa Zanzibar kuna upungufu wa ajira. Ni kweli tatizo la ajira lipo Zanzibar, lakini kwa nini Tume hii ya Utumishi ikawa ina ubaguzi wa ajira, ni sifa gani ambazo kuwa zinatakiwa ili kila kijana ambae anaomba nafasi basi anabakia kulalamika, hata nafasi ya *orderly* unaambiwa sijui uwe na elimu ya kidato cha tano, cha sita, hivi kweli kijana wa kidato cha nne hawezi kufanya nafasi hii ya *orderly* au nafasi ya kufagia Manispaa.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wengi wamezungumzia kuhusu Tume hii ya Utumishi kuhusu suala la Ajira. Kijana anafanyakazi mpaka anafikia umri wa kustaafu, lakini bado ameshafikia miaka 60 *still* anaengezewa ajira za mkataba. Hivi vijana wote wanaosoma hapa Zanzibar hakuna wenye taaluma ambazo kuwa za hawa ambao wanaoengezewa mkataba wanaweza kuzifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Tanzania Bara tayari wameshafanya uchunguzi ya wafanyakazi hewa. Tunaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ifanye uchunguzi ya wafanyakazi hewa. Na hapa Zanzibar wafanyakazi hewa wapo. Kama vijana wa Zanzibar tunaiomba Serikali ijifanye uchunguzi ya wafanyakazi hewa. Vijana wetu wengi wamo mitaani, wanazurura, wameshasoma lakini matokeo yake wanabakia kukaa vibarazani. Vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa hili na bila ya vijana basi nchi haiwezi kuendelea. Ni kweli tunawasaidia vijana kujiwezesha lakini bado, serikali ifanye jitihada zake ya kuweza kuwasaidia vijana na kuwakwamua katika matatizo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar. Ofisi hii ya Mufti Mkuu wa Zanzibar inajitahidi sana. Mwaka jana ilifanya mikutano yake kwa kupitia wafadhili wa *UNDP* Unguja na Pemba kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba, kwa kuwashirikisha wahusika mbali mbali ili kuendeleza amani iliopo hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha kabisa hivi karibuni kuna mtu ambaye alifariki katika Kijiji cha Wingwi Wilaya ya Micheweni Pemba. Lakini Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha maiti huyu wakati anatayarishwa anatoka ndani na kwenda kusaliwa katika Msikiti basi Msikiti ambao uliokuwepo kwenye kijiji kile, alitokea Sheikh mmoja akaweza kuutia kufuli. Na maiti yule hakusaliwa kwenye Msikiti mpaka alitoka Mkuu wa Wilaya ya Micheweni wakenda pale kwenye kijiji kile, Msikiti ule kufuli yake ilivunjwa. Baadae maiti yule ndipo alipoingizwa Msikitini na kuweza kusaliwa.

Niiomba Ofisi hii ya Mufti Mkuu wa Zanzibar. Hii Ofisi ndiyo inayosimamia mambo ya Misikiti na hawa Masheikh wote, Uislamu unakataza mabaya, haya mambo ya siasa tusiyaingize katika Dini. Kuna watu wanajiita wao ni Waislamu lakini sasa hivi wanaichukua siasa wanaingiza katika Dini. Ni ipi faida yao. Niiomba Ofisi ya Mufti walifuatilie suala hili lililotokea katika kijiji hichi na huyu Sheikh ambaye kuwa aliufunga Msikiti huu aweze kuchukuliwa hatua. (*Makofi*)

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, Uislamu haisemi kama mtu wa chama fulani kafariki basi Misikiti ianzwe kutiwa kufuli. Wafanye mikutano tena na Masheikh wote hasa Pemba ili waweze kuwaelimisha waachane na vitendo hivi vya udhalilishaji kwenye Dini. Sasa hivi watu hawazikani, wananchi hawauziani biashara na wakati Zanzibar inaambiwa nchi hii ni nchi ya Waislamu. Tuseme sasa basi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Mahakama. Mhe. Naibu Spika, kila siku ukifungua redio unasikia Mahakama ya Wilaya ya Mfenesini imemfunga kijana miezi sita kaiba nazi mbili au tatu, au kaiba kuku miaka miwili. Lakini kuna kesi ambazo kuwa za udhalilishaji, wanadhalilishwa vijana wetu, watoto wetu, mama zetu, kesi zile zinabiruliwa na zinafunikizwa. Lakini mwizi aliyeiba kuku au shina la muhogo au chana ya ndizi anafungwa miezi sita. Kwa nini kesi hizi za udhalilishaji Zanzibar hazishughulikiwi. Na kesi hizi zinakuwa zinaendelea siku hadi siku. Tumechoka. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi sitounga mkono bajeti hii mpaka Mhe. Waziri atakapokuja kuniambia ni kesi ngapi za udhalilishaji ambazo zinahukumiwa katika mwaka wa 2015 mpaka tarehe ya leo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niishie hapo nitaunga mkono baada ya kupata majibu yangu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru sana Mhe. Viwe Khamis. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Mussa Foum Mussa, atafutwa na Mhe. Shehe Hamad na baada ya hapo atakuja Mhe. Zulfa Mmaka Omar.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kupata fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, na mimi vile vile kwanza niipongeze hotuba hii kwa mpangiko mzuri na wenye kufahamika.

Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja kwanza niende kwenye mada, na mimi nitaanzia hii Kamisheni ya Wakfu na Mali Amana kwenye ukurasa wa 43. Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba ninukuu kidogo ili nipate maelezo vizuri. Mhe. Naibu Spika, "Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamisheni imejipanga kuendesha tilka elfu moja mia moja na hamsini zenye thamani ya bilioni nane, kukagua nyumba mia tatu na moja, kukusanya kodi ya shilingi milioni mia sita na thamanini na mbili, laki nane na ishirini na nne, mia nne na tisini na mbili katika nyumba za Wakfu shilingi za Kitanzania milioni mia nne na sabini na saba, laki nane na kumi na mbili na kumi na sita katika nyumba za Amana za kuzifanyia matengenezo nyumba tatu, kukusanya zakka shilingi milioni kumi na mbili". Hapa kidogo ndiyo mada sasa ninayotaka kuichangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza ninataka nifahamishwe kwa sababu ninavyofahamu mimi kwamba sisi Wazanzibari wengi wetu ni Waislamu lakini kima kilichotajwa hapa ukilinganisha na tulivyo ni kidogo sana. Shilingi milioni kumi na mbili za zakka. Sasa sijui kwamba zakka hii ni zakka ipi? Kwa sababu hii mitiririko ya zakka ni mafungu mengi. Kuna *Zakatul Fitr,* kuna zakka ya biashara, kuna zakka ya kilimo.Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atufahamishe kwamba je, zakka ya milioni kumi na mbili kama sikosei ni zakka ya aina gani. Na ikiwa ni kama hivyo ninavyoifahamu mimi kwamba zakka iliyotajwa kwa makundi yote ya zakka ni kima kidogo.

Ninadhani mimi ningeishauri serikali kwa kupitia hii Kamisheni ya Wakfu na Mali Amana. Kama zamani ilivyokuwa Kamisheni hii ikipeleka watu kwenda kuhiji Makka. Lakini baadae ikafika pahala kukawa na mashirika mbali mbali yanayopeleka watu. Sasa inawezekana hawa watu wa zakka ikawa wana wasi wasi pengine kuzipeleka pesa zao serikalini kwa kuliwa. Kwa hivyo, ni vyema wakaunda *NGO's* mbali mbali ambazo zitashughulikia mambo haya ili kuona kwamba hili jambo la kutoa zakka linaelimishwa kwa Wazanzibari wote ili kuweza kutoa, kwa sababu Wazanzibari ukiangalia milioni kumi na mbili inawezekana pengine, hata huyo mtu mmoja zakka yake ikazidi kwa wafanyabiashara tulionao wakubwa tu. Lakini kima cha zakka kinachotolewa sijui kwamba watu hawana uelewa au kidogo tuna ugumu wa kutoa hii zakka.

Sasa ninadhani naomba suala hili tufahamishwe vizuri ili tujue na wananchi wetu wapate kuelimishwa vizuri kuona kwamba tunayo haki, kwa sababu kutoa zakka ni katika sehemu ya nguzo tano za Kiislamu. Lakini tabia yetu unaweza ukamuona mtu anakwenda Makka lakini hatoi zakka. Sasa unakwenda kurukia juu huku chini unakuacha. Sasa ni vyema wananchi wetu wakaelimishwa vizuri ili kuona kwamba jambo hili linaenda vizuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, pia, vile vile niende kwenye suala la Mahakama. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamezungumza vizuri sana kuhusu Mahakama na kiukweli tuipongeze kwa upande mmoja Mahakama yetu, tunakwenda vizuri katika hilo suala la Mahakama, wengine Waheshimiwa Wajumbe wamezungumza kwamba pesa wanazotengewa ni kidogo, ni kweli kidogo. Lakini licha ya hivyo, hicho hicho kidogo tulicho nacho ni kwamba kile tunachokifanya basi kieleweke.

Mhe. Naibu Spika, kiukweli katika kesi ambazo kuwa zinapelekwa zaidi za udhalilishaji zimekuwa zikisuasua kwa muda mrefu. Na kiukweli wananchi wetu wanafika pahala wanavunja moyo kwa sababu wadhalilishaji wengine ni watu ambao ni taathira, yaani inawezekana wengine wakawa taathira. Kwa hivyo, kiukweli hali inakuwa nzito. Ni vyema Mahakama zetu zikachukua jitihada za kuziendesha kesi kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa ili kuona kwamba mwenye haki apewe ili nchi yetu iende vizuri katika yale masuala ya utawala bora. Kwa hivyo, tunaiomba serikali na kumuomba Mhe. Waziri, hili suala alisimamia vizuri ili kuona alau masuala ya udhalilishaji yanapungua katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia, niende kwenye suala la Ajira. Suala la ajira kiukweli katika nchi yetu hasa ukilinganisha katika ajira za serikali limekuwa na upungufu mkubwa. Lakini mimi ninataka niseme hivi kwamba, inapotokea hiyo ajira, hivyo, ni vyema ikaangalia zile sehemu ambazo kuwa zina mahitaji zaidi. Kwa mfano nitoe mfano pengine katika jimbo langu. Tuna upungufu wa walimu lakini itakapotokea ile ajira ni vyema tukaangalia ile sehemu iliyokuwa na matatizo. Basi ikiwa yale mahitaji na vijana tunao waliokuwa na masharti yale, basi ni vyema wale vijana wakatoka pale kuliko kutoka sehemu nyengine iliyo mbali tukaleta usumbufu ule ule. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ni vyema tukaangalia ile sehemu ambayo kuwa ina tatizo na yale matakwa ya ile ajira, basi wakapewa kipaumbele sehemu ile. Nitoe mfano katika Skuli yangu ya Muambe, hivi karibuni aliajiriwa mtu pengine kutoka Mkoani au Kangani. Lakini ukiangalia pale tunao vijana wamemaliza kusoma ualimu wenye diploma na wapo wa aina zote, wameachwa katoka kule. Anakuja skuli, pengine anafika pale saa tatu na saa nne ilihali ya kuwa vijana tunao pale. Hivyo, ninaomba zikitoka nafasi kama hizo iangaliwe ile sehemu ambayo ina mahitaji makubwa ndiyo ipewe kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi ninataka niseme kwamba suala la ajira tusiliangalie sana na tukalichukua katika suala la Upemba na Unguja. Sote Wapemba na Waunguja ni wamoja. Sote tupo pamoja. Cha msingi ni kuangalia

mahitaji na ile sifa inayotakiwa je, imepatikana. Kwa sababu Wapemba tupo Unguja. Waunguja wapo Pemba. Zinatokea ajira Unguja, Wapemba tunapata, zinatokea ajira Pemba Waunguja wapate. Huo ndiyo utaratibu. Lakini tukija tukihoji kwamba lazima ile ya Pemba asipate Muunguja na itakuja hivyo hivyo za Unguja, Mpemba asipate. Sasa haya yatatufikisha pahala pabaya. Sasa mimi ningeliliomba suala hili tukaangalia mahitaji. Haya yote ni yetu. Ni vyema tukashirikiana na tukenda katika msururu uliokuwa mzuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, vile vile, niende katika suala la usimamizi wa masuala ya Dini. Hapa yameelezwa masuala ya Dini kwamba yatashughulikia zaidi Misikiti na vile Vyuo vya kusomeshea kur-an. Mimi ninataka niseme kwanza niwapongeze kwa mpango wao huu mzuri. Kama walivyosema wenzangu kwamba ni vyema tukawaangalia walimu wa Vyuo. Walimu wa Vyuo wanapata shida sana lakini maslahi hamna. Hivyo ni vyema na wao wakaangaliwa kwa jicho la huruma.

Mhe. Naibu Spika, na Mhe. Waziri kama tunavyomfahamu ni mtu mwenye huruma. Kwa hivyo, tuna mategemeo makubwa kama walivyofanyiwa wazee ambao waliofikia miaka 70 na hawa walimu wa Vyuo vya Kur-an, kwa vile hawatokuwa wengi kama wazee na wao tunategemea kwamba wafanyiwe huruma ili tuone kuwa alau na wao wanapata sabuni kila mwisho wa mwezi. (*Makofi*)

Lakini vile vile nielezee kwamba Masheikh watakapotembelea katika Misikiti kulingana na hali tuliyonayo hivi sasa, ni vyema wakawa wanafanya vikao na kuelezea hali halisi ya mambo yetu tuliyonayo. Kwa sababu Dini yetu ni ya Kiislamu. Dini yetu inazungumza umoja na mshikamano. Lakini leo tumefika pahala sisi Waislamu kwa Waislamu tunaitana Makafiri. Hili si jambo zuri na hiyo inakuja ni kwa sababu ya siasa. Kabla ya siasa mambo hayo hayakuwepo hapa ya kuitana Makafiri, hali ya kuwa wewe Kafiri humjui. Inawezekana wewe unayemwita mwenzio Kafiri, ndiyo Kafiri mkubwa. (*Makofi*)

Sasa ni vyema watakapokuwa wanatembelea kwenye Misikiti haya masuala yaelezwe kuwa siyo mazuri. Siasa isitufikishe pahala pakubaguana mpaka tukafikia pahala pakuitana Makafiri. Sisi ni Waislamu na Mwenyezi Mungu anayemjua kwamba huyu nani, huyu nani ni yeye, hakuna mwengine. Kwa hivyo, ni vyema Masheik wetu watakapokuwa wanatembelea haya masuala wayaeleze na wasifiche. Kwa sababu mpaka baadhi ya Misikiti, kwenye hotuba za Ijumaa wanaleta mitafaruki namna ya kusababisha watu kufarikiana.

Leo Muislamu anakufa, Waislamu wanakimbia kwa sababu ya siasa. Kwenye shughuli zetu za harusi watu hawatembeleani au hawaendi kwa sababu ya siasa, Waislamu hao! Sasa sijui tutakwenda kusema vipi na wanaofanya hivyo ni watu wenyekujua na ni watu wenye kutegemewa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano, Imamu wa Msikti fulani yeye ndiye wa mwanzo anayeanza kukimbia walioko nyuma wataona aah, Imamu kaondoka, je, sisi tufanye nini. Kwa hivyo, ni vyema wakaonesha hizi athari zinazojitokeza kuwa baadae zitatufikisha pahali pabaya.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nizungumzie suala la Idara ya Nyaraka na kumbukumbu za kitaifa. Mimi nizungumzie tu habari ya vyeti. Mhe. Naibu Spika, tumekuwa na tatizo kubwa katika wilaya zetu za upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Suala hili limekuwa ni tatizo kubwa na inawezekana kukaa kwa muda mrefu sana, pengine miaka minne, mitano au sita hakijapatikana, sijui kwa sababu gani. Sasa nadhani tungemuomba Mhe. Waziri, hili suala akalifanyia kazi, kwa sababu hivi sasa imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu juu ya upatikanaji wa vyeti hivi. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri, atakapokuja atueleze kuna sababu gani zinazocheleweshe upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mimi naunga mkono hoja hii na naunga mkono bajeti hii ipite kwa asilimia mia juu ya mia, baada tu ya kupata maelezo yale ya Zakka ili tumpe fursa Mhe. Waziri, apate kutekeleza yale yote ambayo ameyakusudia kuyatekeleza kwa mwaka huu, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mussa Foum Mussa, Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Shehe Hamad Mattar, na baada ya hapo atakuja Mhe. Zulfa Mmaka Omar, kama muda utatosha tutampa nafasi Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi sina budi kukupongeza kwa kunipa nafasi hii na mimi nitowe maoni yangu kidogo na kutaka ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yamenikaa moyoni mwangu na wananchi wengine wanahitaji kuyajua maana yake.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana na nimshukuru Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na Naibu Waziri wake na niwapongeze kwa kuchaguliwa kwao kupewa wizara hii ambayo ni kubwa sana na ina kazi ngumu, namuomba awe mstahamilivu na awe na busara kubwa katika kulea wizara hii, wizara ambayo imechanganyishwa wizara mbili

sasa imekuwa ni moja. Namuomba awe na busara nyingi katika kuiongoza wizara hii.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika upande wa Mahakama. Tumekuwa tukilalamika Mahakama haitendi haki au haitekelezi majukumu, kesi ni nyingi zimerundikana, lakini kuna sababu kama wenzangu walivyosema fedha ni kidogo wanazopewa Mahakama. Mahakama majukumu yake ni makubwa ya kusimamia sheria na haki za watu, ili waweze kufanya majukumu hayo ni lazima waweze kupewa fedha ambazo zinahitaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfao, kesi haiwezi kwenda kama haina mashahidi, mashahidi hawa wanatoka sehemu mbali mbali, wakija pale mashahidi kila siku unapokea kikaratasi kile unaweka kwenye *file* unamwambia nenda. Kwa mfano, hakimu anatoka kama kule Pemba, hakimu anatoka Fundo kwenda kutoa ushahidi wa kesi ilioko Chake Chake Pemba, ni vyombo vingapi anavyovipanda mpaka kufikia kule na akirudi hana fedha ya nauli wala posho ya juisi hana, hili ni tatizo.

Kwa hivyo, mimi namuomba sana waziri asimamie kupewa fedha hizi, lakini Wizara ya Fedha imuongeze pale ambapo itakuwa kuna nafasi. Lakini hii bajeti yake ya Mahakama basi ipewe asilimia juu ya mia, hili nashauri sana kwa sababu tutaweza kumuona ni vipi alivyoweza kutekeleza majukumu yake Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea upande huo huo wa Mahakama kuna masuala ya utumishi na maslahi ya wafanyakazi. Wenzangu waliotangulia walinifilisi kidogo, lakini na mimi nipigie mchapuo kidogo kuhusu hili suala la Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Kwa kweli mahakimu hawa wana kazi kubwa sana, Jaji Mkuu hawezi kufanyakazi kama Hakimu wa Mwanzo hajaweza kuanza kazi hii, kwa hivyo, mwanzo wa kesi inaanza hapa. Sasa leo ikiwa huyu ambaye anatayarisha jambo hili la kumfanya Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama Kuu kuweza kufanya kazi yake, ambayo analipwa mshahara mkubwa huyu tunamdharau na tunamdogosha sana kiasi ambacho hatoweza kufanya kazi zake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, tunasema pasiwe na rushwa, lakini bado tunaikaribisha rushwa, akitizama pesa anazitaka, kesi iko pale ameshawekewa donge kule, kwa kweli sijui utamuweza vipi kumzuwia mtu huyo asichukuwe rushwa. Kwa hivyo, watu hawa malalamiko yao ni makubwa na kilio chao ni kikubwa na mimi walinieleza na leo ndio nawasemea.

Mhe. Naibu Spika, wapewe ile mishahara ambayo waliahidiwa. Miaka mitatu nyuma mahakimu hawa wakiwa katika Sherehe ya Siku ya Sheria duniani na Mhe. Rais akiwa hapo, basi waliahidiwa kwamba watu hawa watapewa haki hizo, lakini hadi leo Mhe. Waziri, watu hawa hawajapewa haki hiyo. Mimi nagombania sana haki hiyo wapewe ili waweze kufanyakazi zao kwa vizuri sana. Ukizingatia sheria ni hiyo hiyo na tume ni hiyo hiyo iliyowapa hao mahakimu wengine wa mkoa na wilaya na hawa ndio watu wa mwanzo wa kuanzisha kesi. Naomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja atuambie ni kitu gani kilichokwama mpaka leo ikawa hawajaweza kupatiwa mishahara yao wanaendelea kuteseka na kusononeka.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kutetea haki na wajibu kwa wafanyakazi katika vyombo vyetu hivi ambavyo tunasema ni mihimili ya serikali au ni mihimili ya dola, ya Mahakama na Baraza la Wawakilishi na vyombo vyengine. Kuna wafanyakazi Mhe. Naibu Spika, ambao wako katika kada ya uhasibu wanaitwa Wasaidizi Wahasibu Wakuu Pemba, wasaidizi hawa wana madai ambayo hadi leo hayajafanyiwa ufumbuzi wake, mishahara yao watu hawa walidai na Wizara ya Fedha inaelewa na walishaambiwa kwamba mara tu watakapotengenezewa mishahara yao ma-*internal auditors* wa wizara wale, basi na hawa Wasaidizi Wahasibu Wakuu walioko Pemba na wao watafanyiwa.

Mhe. Naibu Spika, watu hawa wana *votes* ambazo wanasimamia kama hivi wanavyosimamia huku Wahasimu Wakuu, wale ndio wasaidizi wao; wanasimamia mapato na wanasimamia matumizi. Ni kwa nini hadi leo watu hawa hawajaweza kupata mishahara yao inayotakiwa. Kama vile Mkurugenzi wa Mashtaka, Baraza la Wawakilishi, Mahakama wenyewe, Idara ya Ukaguzi wa Hesabu na Tume ya Uchaguzi. Hizi ni taasisi ambazo kuwa hadi leo wasaidizi wahasibu hawa hawajapata malipo hayo bado na wao wanasononeka. Tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwa nini mpaka leo watu hawa hawajapatiwa mishahara yao.

Mhe. Naibu Spika, niende katika haki au ni fursa, hii naomba sana Mhe. Waziri aiangalie sana kuhusu wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, Pemba mazingira yake ya usafiri ni ngumu sana, kutoka kazini na kurudi. Mfanyakazi anayetoka Wete kwenda kufanyakazi Chake na Chake kwenda Mkoani ni masafa makubwa na nauli zake ni kubwa. Kuna watu mwaka wa 30 huu au na zaidi wanafanyakazi katika sehemu hizo wanasumbuka kwa usafiri. Namshauri sana Mhe. Waziri, awaangalie wafanyakazi hawa kwa kupitia kwa Wizara ya Fedha, angalau kuwekewa usafiri unaotoka Wete kwenda Chake Chake na Chake Chake kwenda Mkoani, kuweza kuwachukua wafanyakazi hawa.

Mhe. Naibu Spika, nawaonea huruma, wanasumbuka sana na ukitizama mishahara yao hawawezi kukidhi kutoa nauli kila siku. Nauli ya kwenda Chake Chake na kurudi ni shilingi 3,000/- hapo hujaweza kupata hata kikombe cha chai, si hivyo utafika kazini saa 4:00 kwa kusubiri dezo, yaani gari ya bure, jambo ambalo linarudisha nyuma utendaji wa kazi. Ikifika saa 8:00 tayari unaanza kutazama ni gari gani inayotoka mapema, hao wote walioko huko ni wafanyakazi wa chini walio wengi, maana kama ingekuwa ni Maafisa Wadhamini wana usafiri wao, na akitokeza Afisa Mdhamini itakuwa ni kigari kimoja hicho wafanyakazi wanafika 30 wanarukia gari. Mtu anakwenda kazini anatoka nyumbani vizuri nanguo zake, lakini likipita gari la mawe haya, la saruji anapanda, kwa kweli hali sio nzuri anapofika kazini na utendaji wake inakuwa hauko vizuri. Namuomba sana Mhe. Waziri, jambo hili aliangalie kwa moyo wa huruma ili aweze kuwasaidia watumishi wetu hawa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika masuala ya wafanyakazi ambao wamefika kustaafu. Jambo hili limeshazungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe waliokwishatangulia, lakini na mimi naliongelea tena hili. Kwa kweli mimi sijui ni sababu vipi za msingi zinazofanya kwamba leo mfanyakazi ameshafika miaka 60 anaombewa tena miaka mitano au miaka miwili, na huku tunapiga kelele ajira. Kuna nafasi ambazo hata ukiambiwa wameongezewa muda zinaingia akilini, lakini kwa sababu ya viongozi tunalindana basi tunaendelea kumpa nafasi yule. Kijana amemaliza kusoma na ametumia pesa ya serikali kusomeshwa, lakini bado anatembea mitaani na elimu yake.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema watu hawa tuwachanganye, tuwachukuwe na wao tuwatie katika ajira wale wazee wabakie pembeni, wakikosa maarifa wale vijana watakwenda kwao na waweke milango wazi, kwamba jamani mimi naondoka lakini mtakaposhindwa njooni chukuweni mafundisho huku. Kama tunavyoona hapa Mzee wetu Spika wa Baraza la Wawakilishi alipokuwa anatuaga aliweza kumshauri Spika wetu mpya kwamba atakapoona anahitaji msaada basi aende akachukuwe msaada wa maelekezo na watu kama hawa Mhe. Naibu Spika, naomba wasipewe nafasi tena kama hakuna umuhimu.

Mhe. Naibu Spika, nafasi hizi, nasema hivi kwamba hasa viongozi mpaka leo mtu anafika hadi kujengewa ofisi hawezi kupanda juu, hawezi kwenda lakini awepo. Kama ni maarifa kama Mwenyezi Mungu akimjaalia uhai tutakwenda kuchukua hekima zake zile, lakini sio vyema kuendelea mtu yule, na huku tukamuona kijana ana elimu ambayo kuwa na kazi ile anaweza kuifanya. Pengine pale kitini anawekwa tu hata kuifanya ile kazi hawezi tena, lakini ilimradi ndio hivyo tunamlea, tutamlea mpaka lini.

Mhe. Naibu Spika, jana sijui juzi tulikuwa tukimwambia mwanafunzi yule au mtoto yule akiwa shuleni tulimwambia wewe ndio kiongozi wa kesho, kesho kesho hii haifiki? Siku zote itakuwa kesho hiyo haifiki na yule ataendelea kubakia pembeni na mzee yule hatimaye ataondoka duniani, maarifa aliyonayo hayapatikani. Naomba hapa tubadilike, serikali ibadilike kwa mtindo huu.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, naomba nifahamishwe katika masuala ya usimamizi wa masuala ya dini. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze vizuri Chuo cha Kiislamu cha Zanzibar kiko wapi? Na kama kipo kinafanyakazi vipi? Chuo hiki tokea hapo nyuma kilipoanzishwa ninavyojua kilikuwa kinatoa makazi, mashehe na walimu mbali mbali ambao kuwa hivi sasa ndio wanaotusomeshea skuli zetu za *primary* na *secondary*, lakini leo naona chuo hiki kama kinayumba, sijui kama kipo au kipo kinatumiwa vipi. Tutawapata wapi tena masheikh kama hao kama chuo hicho hakipo au kama kimetumiwa vinginevyo. Naomba sana atakapokuja Mhe. Waziri, anieleze au aelezee Baraza hili chuo hichi kiko wapi na kinafanyakazi vipi.

Mhe. Naibu Spika, kuna vijana wa mchipuo walikuwa zamani wakitoka mashuleni wakipelekwa hapa, wanakaa miaka saba hapa baadae wanapatiwa nafasi kwenda nje ikiwa Misri, ikiwa Saudia, hatimaye watu hawa leo ndio wanaoanzisha madrasa katika Misikiti yetu, katika miji yetu lakini chuo hiki sijui kinakwenda vipi. Mimi naomba nipate maelezo hapa ili niweze kujiridhisha na wenzangu wasikie huko kwamba chuo hiki kiko wapi.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Hii ni idara ambayo kuwa ni jicho la serikali, tunaitizama hii kwa kutukagulia mahesabu yetu, kuchungulia mali zetu ambazo kuwa zimo katika taasisi zetu hizi, lakini tuna kilio hichi cha wafanyakazi na bado hatujakipa kipaumbele. Naomba sana lile dai lao ambalo walidai la wafanyakazi wapewe, kwa sababu leo ukitizama ripoti ya mkaguzi kuna mwaka 2013/2014 mwaka mzima umepita na huu wa pili utakuwa tayari, unaendelea mwaka wa pili huu, ni kutokana na kwamba watendaji wa shughuli hizi hawapo, lakini wapo nje ya ajira.

Mhe. Naibu Spika, kuna vijana wamemaliza mpaka *degree* katika ngazi hii ya uhasibu na uboharia, lakini wako pembeni. Naomba sana yale madai yao waliodai wapewe vijana hawa waajiriwe na sio kuhaulisha, wanataka wapewe damu changa kabisa, wakija wanafundishwa jambo hili, kuliko kuchukua wale wanaotoka katika taasisi nyengine wakawekwa pale wameshazowea mbinu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hawa ni kiasi cha kupewa msasa tu mafunzo wameshapata, kwa sababu wanatokea Chwaka na vyuo vyengine vya uhasibu, ni imani yangu kwamba wakipewa kazi hii wataifanya ipasavyo vizuri na tutaweza kupata ripoti zetu zitakwenda kwa wakati, badala ya kungojea miaka miwili nyuma mahesabu hayajakaguliwa, naomba sana Mhe. Waziri, atakapofika wakati wake basi na hili alipe kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana nielewe jambo jengine la katika Tume ya Utumishi Serikalini. Kuna matatizo ambayo wakati mwengine hujui uyafanye nini na yanasumbua ndani ya roho na yanarudisha utendaji wa kazi. Kama watu wana kiwango kimoja cha elimu, lakini leo wanapitana. Kwa mfano, *degree* ya madaktari, wote ni *degree* lakini na muuguzi ana *degree*, lakini wanapitana kimaslahi. Ukitizama muuguzi ana kazi kubwa sana, muda mwingi anakaa na mgonjwa ndio yeye anayemuhudumia, tuangalie majumbani tu kazi ya uuguzi ni vipi, sikuambii leo kazi ya hospitali ya uuguzi.

Mhe. Naibu Spika, kama mtu huyu tunataka afanye kazi vizuri basi na yeye tumuangalie vizuri. Kama ana *degree*, na daktari ana *degree*, basi maslahi yao yasipitane, tutizame na hii kazi anayoifanya, tusimbebeshe kazi lakini maslahi hakuna. Nawaombea sana watu kama hawa na wengine kwenye taasisi kama hizi na wenye kiwango kama hiki waweze kuangaliwa, ili kutekeleza ufanisi mzuri wa kazi zetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niliona nichangie hayo, naunga mkono hoja hiyo, lakini maelezo niliyotoa kwa Mhe. Waziri, naomba atufahamishe. Lakini moja nimelisahau naomba nilielekeze.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, muda wako umekwisha.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru Mhe. Shehe Hamad Mattar, sasa atafuata Mhe. Zulfa Mmaka Omar, na kama nilivyosema mwanzo kama muda utatosha basi Mhe. Abdalla Maulid Diwani, atachangia.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii kuchagia hotuba hii. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri, nakupongeza kwa kufanyakazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, wizara zake ni nyingi na nzito lakini nampongeza kwa kuifanyakazi kwa umahiri na kutuletea kitabu hiki kidogo

kilichojaa maneno mazuri, matamu na mimi naamini kwamba Rais atakupongeza kwa kitabu chako hiki kidogo kilichobeba mambo mazuri, hongera. *(Makofi)*

Pia, nampongeza Mhe. Rais kwa kumteuwa *CAG* wetu mzuri ambaye ni mwanamke. Mhe. Naibu Spika, huyu mama anaweza bila ya kuwezeshwa. Huyu mama kazi zake ni nzito sana, jinsia yake ni mwanamke, lakini kazi zake anazozifanya, mimi naweza kukuambia kwamba anawashinda wanaume. Kwa sababu kazi ya kufichua majika mapevu ni nzito sana na inataka umahiri, huyu mama anafanya kazi ya kuuza roho yake, lakini hajali hivyo, yeye yupo kwa nia ya kusaidia Serikali yetu kuinua nchi yetu na kuwafichua majoka hao, mimi nampa pongezi Rais, pia, nampa pongezi huyu mama, aendelee kufanya kazi kwa moyo wake mmoja na sisi tupo pamoja nae. (*Makofi*)

Lakini pia ningeiomba Serikali huyu mama atafutiwe ulinzi kwa sababu kazi yake ni mbaya sana, kazi yake ina fitna na siku zote fitna inakuwa ni adui wa haki, mtu yeyote utakayemfichua na maovu mimi naamini hawezi kukufurahikia anakujengea chuki katika roho yake, kwa hivyo, naiomba Serikali huyu mama apatiwe ulinzi ambao utastahiki ili na yeye awe huru katika matembezi yake asiwe anajificha, uhuru wa mwanadamu unatakikana, kwa hivyo, ningeomba Serikali kidogo huyu mama awekewe ulinzi.

Pia, nikiende katika Wizara hii, Mhe. Waziri, watu wa Wizara hii wana kazi nzito sana tuliyowabebesha na Rais wetu alitoa kauli akasema; 'mtu akipewa mzigo mzito basi apewe na kata ya kubebea mzigo huo', hawa watendaji katika Wizara hii wanaenda huko katika Serikali kwenda kututolea maovu na kuyafichua, lakini sasa stahiki zao ni ndogo, wanalalamika kwamba mishahara ni midogo kutokana na kazi zao. Mheshimiwa, huwezi kwenda kumpeleka mtu ukamwambia kwamba kalinde chakula kile kisiliwe wakati yeye ana njaa, ninaamini kwa imani yangu watakapowezeshwa hao watajua kwamba sisi Serikali imetujali na imetuwezesha, wakienda kuona zile pesa kule ambazo wanazifuatilia hata akipewa anasema hatutaki, sisi tumekuja kwa kazi moja. Lakini hawa tukianza kuwadharau na kuwapa mishahara midogo basi wanaweza kudanganyika kwa urahisi, kwa sababu kile kitu wao wanakitaka na sisi hatuwapatii na wale majoka wanawapa, mimi naamini wanaweza kukipokea. Kwa hivyo, mimi ningekuomba Mhe. Waziri, hawa watu waangaliwe kwa jicho la imani kama wao wanavyoiangalia Serikali jicho la imani kufichua hayo majoka.

Mhe. Spika, niende katika Mamlaka ya kuzuia rushwa, hichi chombo ni chombo kikubwa sana na chombo maalum, mimi ningekuomba pia na wao

katika Wizara hii iangaliwe kimaslahi, mishahara yao iwe ni tofauti na wafanyakazi wa Wizara nyengine ndogo ndogo, mishahara yao ni midogo kwa sababu wao pia wana kazi hiyo hiyo ya kutafuta rushwa na kuzileta mbele yetu. Kwa hivyo, pia na wao hao wenye kazi nzito mimi ningelipenda kwamba waangaliwe kwa mamcho makali sana, pia, mamlaka hii hii jengo lake sio zuri, halina hadhi na kazi ambayo wanaifanya, jengo lao ni baya halifai na kazi ni kubwa sana.

Mhe. Waziri, mimi naamini kuwa jengo hili unalijua tukipita pale tunaliona jengo hili kwamba kuta zake ni ndogo na mbovu, kwa hivyo, lolote ambalo linatendeka ndani pale Mheshimiwa, ukipita unaona Zulfa yule leo kaingia kwenye ofisi ile utamfanyia shaka jamani anakwenda kupeleka umbeya gani. Lakini naamini Mheshimiwa, watu hao wakitafutiwa eneo zuri la kujificha basi watu wengi sana watakwenda kuwapeleka hao wala rushwa kwa kuwataja kwa kujiamini, lakini pale eneo ambapo lipo, lipo sehemu mbaya, ningekuomba Mhe. Waziri, uliangalie.

Pia, Mhe. Waziri, naomba watumishi katika Wizara ile wapatiwe elimu, elimu zao ni ndogo, Ofisa wa pale ana elimu ya *Form Six*, mimi ningeomba tu uwachukue maofisa wale uwapatie elimu ikiwezekana hata kwenda nje kujifunza kiutalam zaidi ili wakija chini wawe wana moyo au utaalam wa kazi yao ambayo wanaifanya.

Mhe. Waziri, mimi nataka nigusie katika suala la sheria, zipitiwe sheria zilizopitwa na wakati. Mheshimiwa, nakuomba katika chombo chako zipitiwe hizi sheria ambazo zimepitwa na wakati na kuzifanya za kisasa kwa sababu ulimwengu wa sasa tunakwenda na wakati, kwa hivyo, Mheshimiwa, nahisi kuwa kuna sheria zimepitwa na wakati, naomba hizi tuzipitie. Pia, sheria zetu zilizopo zilingane na mahitaji ya kiuchumi kwa mfano zao la nazi, ni eneo kubwa la kuimarisha kiuchumi lakini halina sheria.

Mhe. Waziri, enzi zenu kulikuwa kuna sheria maalum ya kuhusu zao la nazi, ilikuwa hawaruhusiwi kuuza madafu tu kiholela holela mpaka madafu yawe ya mnazi wa kitamli, lakini sasa hivi tunaona madafu yanauzwa tu kila sehemu, sasa haya madafu yanahujumu huu uchumi na wanafanya hivyo kwa sababu hakuna sheria ambayo inawafunga. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri, utuletee hiyo sheria hapa katika Baraza letu hili tuipitishe ili kunusuru zao lile la nazi lisiharibiwe.

Sasa naomba niende katika vipaumbele, upatikanaji wa haki za utawala kwa masikitiko kwamba kesi zinacheleweshwa sana na hilo ndio tatizo letu kubwa

sana ambalo tunalipigia kelele, mimi naamini kwamba majaji hili suala kwao wao ni dogo, kwa sababu kuna kesi ambazo zinaweza kupelelezwa kwa muda mfupi na kumaliza, suala hili nikilisemea kwa upande wa Pemba suala hili limelala, kwa sababu kwanza utakwenda pale utaambiwa kwamba leo kesi yako haitaendeshwa kwa sababu Jaji Mkuu hajaja.

Mhe. Naibu Spika, inatuumiza sana Pemba. Kwa hivyo, mimi ningemuomba Mhe. Waziri, atuambie ni lini atatuletea jaji mkaazi katika kisiwa chetu cha Pemba ili na sisi haki itendeke, ningeomba uniletee hilo jibu, ni lini kilio chetu hichi utakinyamazisha, naamini kwamba unaweza, na utakavyofanya hivyo naamini kwamba utazuia pesa za Serikali zisitumike kiholela kwa sababu yule Jaji anapoletwa Pemba kuna pesa nyingi sana ambazo zinatumika kuletwa pale, mimi naamini hakuna sababu ya kutokuletwa jaji Pemba kwa sababu tukisehema kwamba sehemu ya kukaa wanalipwa maposho ya kukaa.

Mimi naamini kwamba kila njia ipo ya jaji kuletwa Pemba, mimi nakuomba Mheshimiwa, nakuomba sana huyu Jaji Mkaazi utuletee Pemba ili na sisi tusiilaumu Serikali kwamba haituletei jaji, tulaumu kwamba jaji hafanyi kazi zake kiukamilifu, kutokana na hayo yakishakutendeka mimi sina tatizo. Pia, niseme naiunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuchangia kwa maelezo yako nitakuwa mchangiaji wa mwisho, vile vile, napenda kumshukuru au kumpa pongezi Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mujibu wa alivyotuwasilisha hotuba yake ya Matumizi, kwa kuwa ni mwalimu wetu basi hongera sana maalim kwa hotuba nzuri iliyopangika na yenye muono wa wapi inakotupeleka Zanzibar. Na vile vile kuwapongeza watendaji wako wote aliokupa hotuba hii.

Lakini kabla ya kuendelea mbele Mhe. Naibu Spika, napenda kunukuu Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ibara ya 13(2), inayosema;

> "Kila mtu ana haki ya kuishi na kupata kutokana na njia ya hifadhi maisha yake kwa mujibu wa sheria, ni marufuku Ibara ya tatu, ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazoweza kumdhalilisha".

Nimesema hayo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu upande wa Jeshi letu la Polisi hii sheria nafikiri hawaielewi na hii Sheria ni halali kwa Zanzibar imetungwa hapa, watu wamepoteza muda wao mwingi sana wa kutunga hii sheria,

nathubutu kusema hawaelewi kwa sababu haya mambo yaliyokatazwa humu wao ndio wanayoyafanya sasa hivi, wanatesa watu, wanapiga watu na kutoza nguvu.

Nikiendelea mbele katika Ibara ya 14, inasema;

"Kila mtu anayo haki ya kuishi kwa uhuru na kuishi kama mtu huru".

Mhe. Naibu Spika, nina maana gani kwa kusema hayo, nimesema hayo kwa sababu hivi sasa ndani ya jimbo langu nina mtu ambaye ameniletea malalamiko kwamba kapigwa na Polisi mpaka kutiwa shoti za umeme bila ya koa, nathubutu kusema bila ya kosa kwa sababu kaja kuchukuliwa tu Maskani kenda kule Polisi kwa chuki zake tu 'kamwambia nitakuonyesha wewe' sasa ile haki ya binaadamu ya kuishi iko wapi. Sasa Mheshimiwa, kama unasimamia Katiba na utawala bora nafikiri hapa hapana Katiba wala Utawala bora, sasa mimi nakuwa wazi kabisa sitokuwa tayari kuunga mkono hotuba yako kama hujanieleza majibu mazuri kuhusu haya mambo wanayoyafanya Polisi kwa raia wetu ambao hawana hatia.

Vile vile, katika suala hilo hilo nathubutu kusema Mhe. Naibu Spika, wiki mbili zilizopita katika Chuo chako cha Mafunzo Zanzibar kuna jirani yangu mmoja aligombana na mfungwa mwenziwe pale akampiga msumari kakaa muda wa wiki mbili Hospitali ya Mnazi Mmoja na amefariki, ni wafungwa hao Mheshimiwa, sasa sijui utawala bora huu unakuwa uko ndani tu na nje hauko, nafikiri baadae uje unielekeze na huyo kijana naweza kumtaja hata jina anaitwa Rashid Halfan, ndio aliyefariki baada ya kupigwa na mfungwa mwenziwe katika jela ya kiinua miguu. Sasa sijui wale wanapata silaha vipi mpaka wanafika kupigana na kupoteza maisha.

Lakini nikiendelea mbele Mhe. Naibu Spika, nakwenda juu ya suala la *IPA*, yaani Chuo cha Utumishi wa Umma, Chuo hiki kimefunguliwa kwa nia safi kabisa katika kuwasaidia ajira na kuwasomesha taaluma wananchi wetu wa Zanzibar, ni kweli wananchi wanapata taaluma nzuri hususan kupitia *Human Resource* na kwa mujibu wa maelezo yako kuna wanafunzi zaidi ya 1,290 ambao wamepata taaluma hiyo katika ngazi mbali mbali Stashahada, Shahada na Cheti. Lakini Mhe. Waziri, nitakuuliza ni wahitimu wangapi waliohitimu mafunzo yao pale ambao sasa hivi wanafanya kazi *Humam Resource* katika taasisi zetu za *Private sectors*. Nina maana kusema hivyo kwa sababu taasisi zile zimebebwa na wageni kutoka sehemu mbali mbali ya nchi yetu kuanzia Kenya, Uganda wanafanya kazi za *Human Resource* wakati sisi tuna chuo kizima pale kinasomesha wananchi wetu.

Sasa sijui ina maana gani tumeweka chuo au nyenzo ya kuwasaidia watu wetu kupata elimu ili kwenda kufanya kazi lakini zile nafasi za kazi hawapewi na wanapewa watu wengine kutoka Kenya, Ugana, Tanzania Bara japokuwa ni wenzetu Tanzania lakini *privilege* sio kama tumeweka chuo basi kile chuo kionyeshe ufanisi wake kwamba kinatoa watu na wanakwenda kufanya kazi katika sehemu zetu kuleta tija katika nchi yetu. Sasa ndio maana nikazungumza kwamba sitounga mkono hoja moja kwa moja kwa sababu mpaka hizi agenda zangu nipate majibu ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nitakweda katika Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana katika Idara ya Mufti, nafikiri wale ni wasimamizi wa shughuli zote za mambo ya dini ya kiislam kwa Zanzibar, lakini Mhe. Naibu Spika, kwa hali ilivyo hivi sasa nafikiri ile taasisi inaangalia sana talaka, kutoa barua au pengine sadaka, yaani nyama ya kondoo imekuja, lakini mambo mengine ya msingi katika nchi hii hawasimamii, nina maana gani kusema hivyo Mhe. Naibu Spika, kama mnavyofahamu nyote humu ndani hali ya nchi yetu sasa hivi haiko vizuri sana na hususan upande wapi wa kisiwa cha Unguja, imefika watu wanasusiana maiti, wanafukuzana misikitini, yale mambo ambayo yamekatazwa katika Dini ya Kiislam ndio wameshika bendera wanawafanyia waislam na Ofisi ya Mufti sijawahi kusikia hata siku moja ikikemea, sasa kama Ofisi ipo sijui inafanya kazi gani baada ya kutangaza ile sadara na hotuba za ijumaa na talaka, nafikiri hili suala la kukemea maovu yanayofanyika kule Pemba si kazi yao au vipi.

Kwa hivyo, nitaomba Mhe. Waziri, utakapokuja unambie na kama imekemea, imekemea kwa asilimia ngapi au mpaka sasa hivi tokea kukemea tumepata afueni gani, kwa sababu Dini ya Kiislam inasema muislam baada ya kufa afanyiwe mambo matatu, akoshwe, asaliwe na azikwe. Sasa leo baadhi ya watu wanasema mambo yote yale asifanyiwe, sasa sijui uislamu huo uko namna gani na wakati tuna taasisi nzima ya Mufti au Wakfu na Mali ya Amana.

Mhe. Naibu Spika, katika hiyo hiyo Wakfu na Mali ya Amana kuna mali za wakfu nyingi sana ambapo kwa upeo wangu mdogo najua nyengine zimeuzwa, sijui taratibu gani zilizosababisha mpaka ziweze kuuzwa kuhusiana na majengo, mimi nina jengo moja kubwa sana tu ambalo limeuzwa na hivi juzi juzi tayari hilo jumba limeshakuwa la Ghorofa, ni jumba la Wakfu na Malia ya Amana, sijui wamepitia taratibu gani mpaka ile mali ya Wakfu ikauzwa. Kwa mujibu wa maelezo mali ya Wakfu ni mali ambayo haiuziki na wala haiwezi kuuzwa, sasa mpaka linabomoka, sasa hivi kuna jumba limeuzwa kabisa na hivi sasa kunajengwa jumba la ghorofa zuri tu pale. Sasa nathubutu Mhe. Waziri utakapokuja unijibu suala langu hili.

Vile vile, nabaki hapa hapa kwenye Wakfu na Mali ya Amana, hichi ni chombo ambacho kinaratibu shughuli nzima za safari za Hijja, sasa hivi Mhe. Naibu Spika, biashara za Hijja imekuwa biashara kubwa sana, sasa hivi Mzanzibari kama huna Dola 4000 kuanzia mpaka 4500 huwezi kwenda kuhiji Makka, nafikiri kama Wakfu na Mali ya Amana wali-*control* hili suala, kwa sababu ni biashara, sasa hivi mashirika yapo mengi, kwa mujibu wa maelezo yako kuna mashirika kumi na sita yanashughulikia mambo ya safari za Hijja.

Ina maana kuna ushindani wa bei, uhalisia bei imekuwa kubwa sana, wananchi wetu wanatozwa pesa nyingi sana kutokana na biashara wakati zamani ilikuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Wakfu na Mali ya Amana walikuwa wanaratibu shughuli nzima kusafirisha mahujaji *as* Serikali ya Zanzibar, sijui kimetokea kitu gani, najua pengine upungufu wa fedha katika Serikali ya Zanzibar ndio ikawa hili suala huria kwa wafanyabiashara wajitolee kutafuta makampuni mbali mbali ya ndege kuja kuchukua Mahujaji wetu kupeleka Saudi Arabia. Pamoja na changamoto wanazozipata nyingi nyingi, lakini ilikuwa raha zaidi Serikali inge-*play a part* katika sehemu kubwa sana hata kuwapangia bei maalum wale watu ukawepo uwiano ili na sisi kwa sababu Zanzibar ni kisiwa cha Kiislam karibuni asilimia 98 au 99 waislam. Basi twende kidogo upatikane unafuu ili watu wengi sana wananchi wetu wapate fursa hiyo ya kwenda kuhiji Makka kwa bei nafuu.

Mheshimiwa, milioni kumi, kumi na moja si pesa ndogo kwa wanyonge na kila usiku ukicha wanatwambia huduma zinapanda, lakini masafa kutoka Makka na Zanzibar ni yale yale hayapandi. Sasa naomba vile vile uje unieleweshe kulikoni inakuwa hivyo Mhe. Naibu Waziri.

Halafu narudia tena juu ya suala zima la Chuo cha *IPA*, chuo cha *IPA* Mhe. Waziri, kuna mgogoro mkubwa sana uliopelekea mpaka baadhi ya wafanyakazi 35 kuandika waraka wa kutokuwa na imani na mrajis wa chuo kile kutokana na utendaji wake wa kazi, nathubutu kusema hahudhurii kazini ipasavyo, kuna kushindana kwa kutunishiana vifua baina ya Mrajis wa Chuo na Mkurugenzi wa *IPA*, hapa nilipo nina waraka kamili huu ambao kuna baadhi ya majina ya watu na mpaka saini zao wametia hapa, niko tayari kukuonyesha ikusaidie ili iwe kisaidizi chako ili utakapokuja unambie umefikia hatua gani katika mgogoro ule pale ulioko kwenye Chuo cha *IPA*. Tunakusudia chuo kile kitoe wasomi wetu wengi sana, lakini inapokuwa katika ngazi za ungozi watu hawaelewani na hawafanyi kazi ipasavyo, sijui kama kweli wataweza kuzalisha wataalam ipasavyo.

Vile vile, napenda kuzungumzia suala la Mahakama, pamoja na malalamiko mengi au pongezi nyingi sana kwa namna moja au nyengine tuwapongeze wafanyakazi wetu wa Mahakama, wapo wenye moyo thabiti kuifanyia kazi Zanzibar katika fani zao za sheria bila ya rushwa, lakini kujitolea kwao kule isiwe sababu tena tukawabeza kwamba zile stahiki zao zikawa hazipatikani pale ipasavyo, imefika wakati wafanyakazi wanafika kuhamishwa Unguja kwenda Sehemu ya pili ile gharama ya usafiri wa kusafisha sehemu moja na nyengine inachelewa mtu hapati ndani ya muda wake, unamwambia tu kuanzia tarehe fulani unatakiwa uwe umeshafika kwenye kituo chako cha kazi Pemba bila ya kujali yule mtu ataondoka vipi Unguja kuelekea Pemba.

Kwa hivyo, lazima Mhe. Waziri hili suala uliangalie vizuri kwa sababu yule mtu anakwenda katika fani ya sheria na sheria ni sehemu pekee ambayo watu wanapata haki zao, vyenginevyo vyovyote ile haki inaweza kupindishwa baada ya kupata vishawishi viwili vitatu akawa hatendi haki, lakini naamini kwamba vijana wetu wanafanya kazi vizuri na wanahukumu vizuri pamoja na wenzangu nyuma waliosema kwamba siku zote wanaposikia habari kutoka Mahakamani basi inakuwa kesi za Mfenesini, Mwera; kaiba ndizi, kaiba kuku na masuala mengine.

Lakini zile kesi ambazo zinazopigiwa kelele kila siku ya Mungu katika kisiwa hichi hazihukumiwi, kesi zenyewe kama kesi za udhalilishaji, udhalilishaji Mhe. Naibu Spika, umekithiri sana na kesi Mahakamani zipo nyingi sana pamoja na wenzangu wameshamtaka Mhe. Waziri akija awaeleze mpaka sasa hivi kuna kesi ngapi za udhalilishaji na ngapi ambazo zimetolewa maamuzi, na ngapi hazijatolewa maamuzi na kwa sababu gani hazijatolewa maamuzim nataka nimwambie na mimi naungana nao hao utapokuja kufanya majumuisho yako nipate taarifa hiyo, kwa sababu kila usiku ukicha tunakuta kesi zinazidi tu. Hususan unapokwenda Kaskazini Unguja kule inasemakana kwa ajili ya Takwimu kule ndio wameshika bendera.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, napenda kuchangia katika suala la Mwanasheria, alizungumzwa kwamba Ofisi ya Mwanasheria kuna sheria zimepitwa na wakati ni kweli kabisa, kwa mujibu wa maelezo yake juzi alisema kuna Sheria ya udhalilishaji wa ubakaji ina miaka mia moja ikifika 2017 miaka mia sheria mpaka leo haijarekebisha, nafikiri ni mwanya mzuri kwa hawa 'vitangi' kufanya mambo kwa sababu ile sheria kidogo inawapa nafasi ambayo hawezi kukamatwa *read-handed* wakapatikana na hatia.

Kwa hivyo, ningeomba Wizara yako Mhe. Waziri, ifanye haraka iwezekanavyo ilete mswada wa kurekebisha sheria hiyo ili zile kesi zitakapokuja na kwenda

kule Mahakamani kuwe kuna sheria kali za kutolea maamuzi haraka iwezekanavyo baada ya zile sheria za zamani kupitwa na wakati, sheria zaidi ya miaka mia sisi sote hatujazaliwa sheria ile imetungwa, nafiri haiendani na usasa, sasa tuko katika *Digital* lakini sheria iko kwenye *Analogue* huko. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri, afanye haraka iwezekanavyo na utuahidi hasa katika Baraza hili lini utaletwa mswada wa sheria ile kubadilishwa Sheria ya udhalilishaji ili kuwarudishia imani wananchi wetu ambao wengi wao sasa hivi wanaamua kuyamaliza nje ya Mahakama ambavyo si sheria, linapotokea suala la udhalilishaji lazima lipite katika mkono wake...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa Mhe. Spika, mimi kama muda umekwisha nathubutu kutamka kwamba hotuba hii siiungi mkono mpaka Mhe. Waziri, ataponiridhisha na masuali yangu ama maelezo yangu, basi nitamuunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu pamoja na michango yetu na mpaka tulipofikia hapa naahirisha kikao hadi kesho tarehe 2/06/2016.

(Saa 1.37 usiku kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 02/06/2016 Saa 3.00 asubuhi)